# TUONANE DURBAN

# richard MWAMBE

**JAMVI LA SIMULIZI**

+255 672 160016 / +255 766 974865

jamvibooks@gmail.com

© Richard R. Mwambe (Amata Ric)

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili wala kuitumia kazi hii kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya mwandishi. Kutekeleza kinyume chake itakuwa ni kosa na sheria itachukua mkondo wake pasi na kujali cheo, umri wala aina ya mtu.

## KITABU CHA 1

# MKATABA WA KIFO

(Jiue Mwenyewe)

## UTANGULIZI

Saa moja usiku huo, vijana wa TSA wakiwa *full package* walikuwa hewani na chopa la kijeshi ambalo daima hulitumia kwa kazi zao, wakielekea huko. Scoba kama kawaida yake, alikuwa akiliongoza *chuma* hilo. Walihakikisha wanapita upande ambao watu wanaowataka wasishtuke. Daima Chiba alikuwa akiwaangalia kupitia kompyuta yake katika mfumo wa satellite.

"Tafuta sehemu ya kutua, tumeshawaacha nyuma!" Chiba akamwambia Scoba. Hesabu zao hazikuwa haba. Tayari walikuwa juu ya Mto Ruaha. Scoba akatafuta eneo zuri ambalo kwalo angeweza kushusha ile chopa. Akalipata. Katika uwanja mdogo wa kijiji cha Igagala, wakatua. Dakika tatu zilizofuata tayari walikuwa nje wakiwasubiri, bunduki nzito zilikuwa vifuani mwa Kamanda Amata na Chiba na Gina huku wakiwa wamevalia mavazi ya kijeshi. Siku mojamoja walipenda kuvaa namna hii.

Kutoka kwenye moja ya kona zilizo pembezoni mwa milima hiyo ya Tao la Mashariki, mwanga wa taa za magari yaliyokuwa yakija ili kupita eneo hilo ulionekana. Baada ya kupita lori la mafuta na mizigo. Amata na Chiba waliingia

barabarani na kusimama katikati. Naam, Landrover Count, mbili, nyeusi ziliibuka.

"Haohao!" Chiba akawaambia wenzake. Wakaziweka bunduki zao tayari. Scoba akasogea na kuwasimamisha. Yale magari yakatii amri na kusimama. Scoba akaliendea lile la mbele na kugonga kioo huku akitoa ishara ya kufunguliwa kioo hicho. Kikashushwa.

"Washa taa za ndani!" akawaamuru. Yule dereva akatii. Ndani ya lile gari mulikuwa na watu watatu, Wazungu; wawili wanaume na mmoja mwanamke. Scoba akawaangalia vizuri. Akawahoji maswali kadhaa kasha akawataka kushuka kufungua sehemu ya nyuma ya magari hayo.

"Mnataka nini?" Mzungu aliyekuwa akiendesha akauliza.

"Ukaguzi! Tunataka kukagua magari yenu! Shuka haraka!" Scoba akamwambia na yule jamaa akashuka akifuatiwa na wenzake. Katika gari la nyuma, kulikuwa na wengine wawili. Magari yale yote mawili upande wa nyuma yalifungwa barabara. Mtu wa nje hasingeweza kuona vilivyomo ndani.

"Sawa!" yule jamaa akajibu na kuzunguka nyuma ya lile gari huku Scoba akimfuata nyuma na bunduki yake ikiwa

tayari kwa lolote. Amata na Chiba nao walifuata upande huu na ule. Katika gari la pili, hakuna aliyeshuka, lakini tayari waliona hali ya pale haina amani.

“Fungua!” Scoba akamwamuru yule jamaa naye akafungua ule mlango. “Weka mikono juu! Mtie pingu!” Scoba akamwambia Chiba. Scoba aliamuru baada ya kuona shehena ya bunduki hatari zilizopangwa kwenye rafu za chuma. Yule jamaa akatiwa pingu, na waliobaki nao wakashushwa na kutiwa pingu. Kutoka gari la pili wakajiandaa kwa mashambulizi. Mmoja wa wale waliokuwamo humo akaandaa bastola, tayari. Akampatia mwenzake na kumweka tayari. Wakati Scoba, Chiba na Amata wakishughulika na wale watu waliowakamata hawa jamaa wawili waliobaki kwenye gari jingine walitoka ghafla ili kuanzisha mashambulizi. Aliyekuwa nyuma ya usukani alipokanyaga ardhi tu, hata kabla hajakanyaga vizuri ardhi, yule jamaa alijikuta akitupwa upande mwingine na kuanguka kama mzigo. Roho yake ikauacha mwili. Risasi iliyopigwa kutoka mafichoni kwenya vichaka ilimaliza kazi iliyotumwa. Yule mtu wa pili alipoona mwenzake damu zikimruka akajua tayari, kumekucha, alicofanikiwa ni kufyatua risasi moja ambayo badala ya kumpata mlengwa ambaye ni Scoba, ikadidimia shingoni mwa mwenzake aliyekuwa na pingu mikononi. Kiwewe!

“Nooooo!” akapiga kelele na kujitoa kwenye ule mlango huku akifyatua risasi ovyo. Kabla hajaleta madhara, alijikuta akipaishwa juu na kubwagwa ukingoni mwa gema kubwa linaloelekea mto Ruaha. Gina alijitokeza lutoka kwenye moja ya kichaka akipiga mluzi.

“Hongera mwanamke!” Amata akamwampongeza.

“Asante!”

Nusu saa baadae gari la polisi likawasili mahali pale. Askari kutoka Mikumi, wakawasili wakiwa wametimia kwa zana. Wakatakiwa kufanya wanaloweza yale magari mawili yafikishwe kituoni kabla hayajarudishwa Dar es salaam. Zile maiti mbili na wale wengine wakapakiwa kwenye lile chopa na safari ya Dar es salaam ikaanza.

# 1

## Miaka minne iliyopita

## Saa 3:21 asubuhi

NDANI YA JENGO refu kuliko yote, linalojulikana kwa jina Monte Blanc, lililojengwa katika jiji la Durban ni mtu mmoja alikuwa akiwindwa kwa udi na uvumba. Ni mara sita kama si tano mtu huyo kukoswakoswa na wauaji hatari waliokuwa wakikodiwa na adui zake. Alitakiwa kufa. Kwa nini? Hii ilikuwa ni siri ya mtu mmoja tu mwenye pesa ndani ya nchi ya Canada. Hakuona gharama kukodi muuaji yeyote anayemtaka ili akamilishe kazi yake, lakini hakufanikiwa kuitwaa roho ya mtu huyo.

Safari hii hakutaka kufanya makosa hata kidogo, alihakikisha anajiandaa kikamilifu, anapanda mbegu, inamea, anaipalilia na kuitunza ili ikomae na kumpa matunda. Robinson Quebec, tajiri kati ya matajiri, mmiliki wa migodi ya madini anuai sehemu mbalimbali za ulimwengu husussani

Afrika, alikuwa kondoo ndani ya ngozi ya mbwa mwitu. Kwenye pesa, hakutaka utani hata kidogo. Falsafa yake ya 'tumia pesa upate pesa' ilijijenga vyema moyoni mwake. Atakuja kwako, yeye na timu yake aliyoisambaza katika pepo zote za dunia, watakushawishi, na huwezi kukataa abadan. Ukikubali kufanya naye biashara kama mbia wako, umeumia. Atakuhesabia miaka na faida yako kana kwamba biashara hiyo ni yake. Muda ukifika, atausimamisha moyo wako na kuiondoa roho yako, kisha yeye mkataba utamlinda na kummilikisha biashara hiyo.

Baada ya kushindwa mara kadhaa jaribio la kumuua tajiri wa Afrika Kusini aliyejulikana kwa jina Great Khumalo, aliamua kutuliza akili na kutafuta mbinu nyingine. Akafanikiwa.

* * *

Alijua anawindwa, alijiwekea ulinzi wa kutosha wa vijana wenye weledi ambao aliwalipa mshahara mnono. Vijana hao wenye mafunzo stahiki kwa kazi hiyo waliifanya kazi yao vyema na kwa moyo wote. Alikuwa ni mgane mwenye mtoto mmoja tu wa kike, aliyemsomesha kwa gharama kubwa ili tu amrithishe migodi yake pindi muda wake wa kuwapo duniani ukifika tamati. Vijana hawa shupavu, walimwokoa mara kadhaa tajiri wao dhidi ya

majaribio ya kuuawa ndani nan je ya Afrika Kusini. Hata ndani ya nchi yake mwenyewe, hakutakiwa kutembea ovyo au kuonekana hadharani kwa kuwa kati ya adui zake ilikuwa jumuia ya siri ya watu wa magharibi yenye makao ndani ya Johanesburg ambayo Robinson alikuwa mshirika wao ikimtafuta kwa hali na mali.

Siku hii haikuwa yenye jua kali, hali ya mvua ilitamalaki ilhali haikunyesha. Wingu lenye weusi wa wastani liliifunika Durban na kufanya hata bahari yake itulie. Asubuhi hiyo ya saa tatu *Lamborghini Veneno*, gari la kifahari na gharama kabisa duniani iliegeshwa taratibu katika maegesho ya jengo hilo la Monte Blanc. Nyuma yake likasimama gari jingine, BMW jeusi. Kutoka kwenye lile BMW vijana wanne wakakamavu waliovalia suti nyeusi zilizotanguliwa na mashati meupe huku shingoni mwao kila mmoja kulining'inizwa tai ndefu nyeusi. Macho yao yalifichwa na miwani ya jua iliyochangia kuuweka hadharani utanashati wao. Walikuwa kikazi zaidi; macho yao yakitazama kila upande kwa umakini wa hali ya juu, mmoja wao aliliendea lile Lamborghini, akaufungua mlango na kuukinga upande wa juu kwa kiganja cha mkono wake wa kushoto ili atokaye ndani asijigonge. Kwa mtindo huo ilionekana aliye ndani ya gari hilo ni mheshimiwa sana, *a delicate person*.

Alitoka nje ya gari lile na kuliweka vizuri koti la suti yake ya gharama. Mkono wake wa kulia ulienda kwenye kifundo cha tai ili kuirekebisha. Alipohakikisha yuko sawa, akavuta hatua ndogo ndogo kulielekea jengo hilo. Vijana wake walitembelea kwa mpango maalum. Mmoja alikuwa mbele, wawili waligawana upande huu na ule nay eye mwenyewe kumuweka kati. Nyuma kulikuwa na kijana mwingine. Ilikuwa ngumu kumgusa mtu huyu tajiri katika jiji la Durban. Nani asiyemjua Khumalo? Hakuna shule au hospitali ambayo hajawahi kufadhili katika jiji hilo. Alishiriki na kuchangia pesa katika shughuli mbalimbali za kijamii. Alijulikana. Akapendwa. Macho ya watu  yalimtazama kama lulu.

Alijulikana kwa jina jepesi tu, Gervas Khumalo aliyezaliwa na kukulia katika kitongoji cha Berea. Akalelewa katika familia yenye maisha ya kati, lakini iliyoweza kumlipia masomo yake ndani na nje ya nchi mpaka akawa mtu mkubwa.

Hatua zake zilimfikisha katika mlango mkubwa wa jengo hilo. Ukafunguliwa kwani yeye hakutakiwa kushika sehemu yoyote kwa kuhofia usalama wake. Kila mtu alimhusudu, lakini hakukuwa na nafasi ya kumpa hata mkono kwani alikuwa akilindwa vilivyo. Moja kwa moja

wakaingia katika lifti ili kupanda juu katika ofisi moja ya jengo hilo.

Monte Blanc, jengo lenye urefu wa mita mia moja na thelathini na tatu zilizobeba sakafu arobaini, lililojengwa mwaka 1985. Ndani ya lifti hiyo alizungukwa pande zote na vijana wake waliosheheni silaha hatari ndani ya makoti yao.

Mmoja wao alibofya kitufe chenye namba ishirini na tatu kilicho katika kuta ya dude hilo na mara tu likaanza kupanda juu. Lilipofika mahala lilipoamriwa, likasimama. Kengele hafifu ikasikika kwa pigo moja laini. Mlango ukafunguka. Wakateremka na kutembea kuelekea ofisi hiyo waliyoihitaji. Wakaipita milango kadhaa na kila waliyekutana naye koridoni humo alipisha tajiri huyo apite.

*'KwaZULU Beauty and Massage'.*

Wakasimama hapo. Mlango wa kioo ukafunguka, wawili kati yao wakaingia na tajiri huyo katika ofisi ile na waliobaki wakangoja mlangoni kuhakikisha usalama upo. Khumalo moja kwa moja alienda katika kochi kubwa na kulikalia mara baada ya vijana wake kulihakikisha kuwa halina shida. Punde tu mrembo mweusi wa Kiafrika alijitokeza kwenye mapazia yaliyokuwa na nakshi za kumetameta. Ndani ya ofisi hiyo pana na nzuri kulikuwa na wasichana wanne waliokuwa katika kazi zao za kila siku;

mmoja mapokezi, mwingine kupokea pesa na kutoa risiti. Wa tatu usafi na aliyebaki, kuongoza wageni kule wanakotakiwa kwenda.

"Karibu sana," yule mwanamke akamsalimu. Ukimwangalia alivyo, utasema ni Malaika kashushwa kutoka mbinguni lakini alikuwa ni binadamu kama wengine. Alitabasamu daima, ngozi yake mwororo haikuwa hata na doa seuze chunusi.

"Asante sana," akaitikia huku akiachia tabasamu lake la pesa-pesa. Haikuwa mara ya kwanza kwa tajiri huyo na matajiri wengine wengi kufika sehemu hiyo. Wote walifika hapa kwa minajiri ya kupata huduma ya kukandwa mwili, ili kuirudisha miili yao katika hali nzuri ya kiafya. Bwana Khumalo alikwishazoea mara nyingi kuja mahala hapo kwa ajili ya huduma hiyo. Alikuwa na ratiba kabisa ya kufanyiwa jambo hilo.

Yule mwanadada akampa ishara ya kuwa amfuate, akafanya hivyo. Wakaingia katika mlango ule wa mapazia na kufuata korido ndefu. Waliipita milango mingi ya vioo ambayo ndani yake kulikuwa na wanawake waliokuwa wakifanyiwa urembo wa mwili na nywele. Vyumba vingine vilikuwa ni vya mazoezi ya viungo, kulikuwa na mabafu

maalum kwa ajili ya wanaotaka kuusafisha mwili kwa mvuke na kadhalika.

Baada ya mwendo wa kama dakika moja na sekunde chache hivi, walifika kwenye moja ya milango ambayo daima huingia hapo. Wale walinzi wakasimama nje ya mlango na bosi wao akaingia ndani pamoja na yule mwanamke kwa ajili ya kumpa huduma hiyo. Juu ya mlango ule kuliandikwa V.I.P.

# 1ii

## Saa 16 zilizopita

BOEING 747 ya shirika la ndege la Amerika ilikanyaga barabara za uwanja wa ndege wa kimataifa wa Louis Botha jijini Durban. Kwa mwendo wa maringo ilisimamaa kandokando ya jengo kubwa na zuri la kupendeza. Ngazi zikasogezwa na punde tu abiria wakateremka mmoja baada ya mwingine. Katikati ya wasafiri hao alikuwa mwanamke mmoja wa kizungu, aliyezifunga nywele zake kwa mpira nyuma ya kichwa chake, akiteremka taratibu kana kwamba anaogopa kuzikanyaga ngazi hizo. Alikuwa mrefu, mwenye mwili mkakamavu, miwani myeusi ya kumkinga jua ilitulia sawia usoni mwake ijapokuwa jua halikuwa kali kwa kuwa tayari Maghalibi ilifika.

Kwa hatua za hesabu na mwendo wa maringo aliiacha ngazi hiyo na kutembea kwa haraka kidogo kuingia ndani ya jengo kubwa la kupokelea wasafiri. Hakuwa na mizigo zaidi ya kibegi kidogo kilichotulia mgongoni mwake, akafanya

itifaki za uhamiaji kisha akatoka nje. Moja kwa moja akaziendea taksi zilizosimama nje hapo, akafungua mlango wa mojawapo na kuingia.

"Hard Rock Café," akamwambia dereva wa ile taksi. Naye hakuuliza mara mbili aliwasha gari na kuifuata barabara kuu, akakaza mguu mpaka katikati ya mji mbele ya mgahawa huo maarufu kabisa katika miji mingi mikubwa duniani.

Tracy Tasha, akamlipa dereva na kumuomba kadi yake ya kibiashara. Bila kinyongo yule dereva akampatia. Tracy akazikwea ngazi na kuingia kwenye mgahawa huo uliosheheni Wazungu. Ndani ya mgahawa huo hakuona mtu mweusi zaidi ya wafanyakazi wachache waliokuwa hapo. Hakuamini macho yake. Alipotupa macho upande wa pili aliona kumejaa watu weusi wengi sana wake kwa waume pamoja na familia zao.

*Ubaguzi hauwezi kwisha nchi hii,* akajiwazia huku akitoa noti ya Randi Hamsini na kuagiza kinywaji cha matunda. Kwa jinsi alivyokaa jioni hiyo katika mgahawa huo, alikuwa akitazama upande wa barabara, na ng'ambo ya barabara hiyo kulikuwa na jengo kubwa la takribani ghorofa kumi hivi, likipambwa na maandishi makubwa meusi yaliyobandikwa

kwenye ukuta. Maandishi hayo yalisomeka *KHUMALO TOWER*.

*…Saa 2:00 usiku milango yote hujifunga kwa mitambo maalum ya kiusalama, ukisogelea mita kumi na tano tu taarifa hupelekwa panapohusika…*

Aliikumbuka sauti ya mteja wake Bwana Robinson kutoka Canada alipokuwa akimpa maagizo akimwelekeza eneo ambalo atampata mbaya wake.

Jaribio la mwisho la kumuua tajiri Khumalo lilifanyika Uingereza baada ya tajiri huyo kupigwa risasi mwilini mwake. Bahati nzuri alikuwa na vazi la kuzuia risasi hivyo hazikumdhuru. Miezi kumi na moja baadae, Robinson Quebec alimkodi mwanamke huyo na kumuahidi kitita. Tracy, alimhakikishia kazi nzuri tajiri wake, akamjaza matumaini na kumfanya atabasamu. Kutokana na sifa ambazo Quebec alipatiwa na watu kadhaa wenye kazi kama hizo, hakuwa na shaka. Tracy alikuwa muuaji mahiri mwenye mikono myepesi inayofanya kazi kwa haraka zaidi kuliko ubongo wake. Alikuwa mwepesi wa kuua kwa mikono yake na kutoroka bila kujulikana. Alikuwa mweledi wa kucheza na kamera za usalama na kuziadaa daima. Alikuwa mjanja.

*…Utaweza?...*

Swali lililompa utata sana ambalo mteja wake alimuuliza.

*Nitaweza tu, kama nilivyoweza kwa wengine!* Akajibu mwenyewe ndani ya moyo wake. Punde si punde giza likaikabili Durban, Tracy akainua macho yake na kuona taa za barabarani zimeupendezesha mji huo. Akanyanyuka taratibu na kutoka nje, akavuka barabara kubwa na kufika upande ule wenye lile jengo alilolikusudia, watu walikuwa wakitoka ndani yake kwani muda wa kazi ulikuwa umekwisha. Alifika mlangoni na kuingia ndani akipishana na wafanyakazi wa maofisi mbalimbali ambao walitakiwa kuliacha jengo hilo kabla ya saa mbili kamili usiku.

"Fanya haraka uwahi kutoka bado dakika arobaini tu," sauti ya mlinzi ilimwambia mwanamke huyo ambaye tayari alikuwa ameifikia lifti ya jengo hilo na kuingia. Akabonya kitufe namba kumi, lakini lengo lake lilikuwa ni kufika ghorofa ya saba ambapo ndipo zilipo ofisi za tajiri, mmiliki wa jengo hilo, Great Khumalo. Akili yake ilicheza haraka sana, alijua wazi akibofya kitufe namba saba walinzi wangemshtukia kwa kuwa ghorofa hiyo mtu huenda kwa miadi maalum, hivyo akaenda gholofa ya  kumi kisha akashika ngazi kurudi alipopataka. Akakutana na mlango wa kioo uliofungwa, akajaribu kuugusa na kuutikisa,

haukutikisika, kitasa chake kilifungwa kwa ndani, akashusha mkoba wake chini akafungua na kutoa kifaa kinachojulikana kama *Circular Glass Cutter* chenye ncha ya almasi katika mwisho wake. Akakibandika upande mmoja katika ule mlango na ile ncha akaizungusha vizuri kabisa alipotoa kile kifaa akatoka na kipande cha kioo katika mtindo wa duara. Kikaacha pale tundu, akapenyeza mkono na kufungua kile kitasa kisha akaingia ndani kwa mwendo wa polepole akiangalia kila upande, mpaka alipoufikia mlango wa ofisi iliyoandikwa kwa maansidhi ya dhahabu *Grevas Khumalo*. Akachukua funguo yake katika mikono iliyovikwa soksi maalumu za ili kutoacha alama mahala popote. Akaufungua taratibu nao wala haukumpa shida.

Akaingia, na moja kwa moja aliielekea meza kubwa iliyo tanguliwa na kiti kikubwa cha kuzunguka. Hakika ilikuwa ofisi ya kisasa mithili ya ile ya rais. Akatupa jicho mezani na kuona kile alichotaka, kitabu kikubwa cha kumbukumbu, akakipekua mpaka tarehe ya siku hiyo, akatazama tazama na kuona vyote viliandikwa kwa lugha ya kwao ki-zulu, katika tarehe inayofuata, akaona alichofikiri kingemfaa.

*'KwaZulu Natal Beauty and Massage, saa 3:30 asubuhi kesho'.*

Ilikuwa ni miadi ya kila mwezi. Tracy akatikisa kichwa kwa mtindo wa juu chini, akaafikiana na kilichoandikwa. Akafunga kitabu hicho na kutoka ndani ya ofisi ile, akafunga ule mlango wa kioo na kukirudisha kile kipande cha kioo kwa gundi kali sana ambayo huwezi kugundua kirahisi kama palikatwa. Akatoka na kukwea ngazi mpaka ghorofa ya kumi akaingia kwenye lifti na kuteremka chini.

* * *

Mwanamke aliyekuwa ameandaliwa kwa ajili ya kazi ya kumfanyia *massage* alikuwa akimsubiri mteja wake kama alivyoelekekezwa na bosi wake, na daima ni yeye tu aliyekuwa akimfanyia kazi hiyo kwa maana baada ya kumaliza zoezi hilo basi ndani ya vyumba hivyo Khumalo alipeana mapenzi mazito na mwanamke huyo.

Kabla tajiri huyo hajaingia katika chumba hicho walinzi wake walikikagua na kuhakikisha usalama. Ndani ya chumba kile kulikuwa na mwanamke mmoja tu kwa ajili ya kazi hiyo, wakatoka ili kumruhusu bosi wao aendelee na starehe zake. Bwana Khumalo akaingia ndani ya kile chumba na kuingia tena katika kijichumba kingine kwa ajili ya kutoa nguo zake na kuvaa taulo.

Khumalo akalala kifudifudi kwenye kile kitanda cha kufanyiwa *massage*, yule mwanadada akasogea na kibweta cha

mafuta na kuanza kumpaka mgongoni tayari kwa kazi. Mikono laini ya mwanamke yule ambayo ilishazoelewa na tajiri huyo ilifanya kazi yake.

“*Yesss* Beibi, fanya kama siku zote, mmmmmmhhh!” Khumalo alianza kuguna kwa ule mtomaso laini wa yule mwanadada. Mwanadada yule alianza kuongeza manjonjo kwa kumpigapiga vijingumi kwenye sehemu zake za mbavu, mgongo akipanda mpaka karibu na mabega na kushuka mpaka katikati ya mgongo.

Tracy Tasha alikuwa kimya kabisa kajificha katika bafu la chumba hicho, alipoona dakika kumi zimepita akajua sasa ndio wakati wa kutekeleza azma yake, kutekeleza kazi yake.

*Siku zako zimekwisha!* Akajiambia. Akatoka taratibu kutoka katika lile bafu na kusogea mpaka pale kitandani nyuma ya yule mwanadada aliyekuwa akiendelea na kazi yake. Akamsogelea na kusimama pembeni yake, yule mwanamke akamuona Tracy. Alijikuta kama kakutana na mzimu kwa sababu ndani ya chumba kile alikuwa peke yake. Huyu kaingiaje? Alipopigwa na bumbuazi, Tracy alimuoneshea ishara ya *‘kimya’* kwa kuweka kidole chake cha shahada juu ya midomo yake. Kabla yule mwana dada hajaondoa mkono wake pale mgongoni mwa Khumalo

Tracy tayari alikuwa ameweka wa kwake, kisha akamsogeza nyuma yule mwanamke.

"Ooh *sweetie*, vipi mbona umesita?" Khumalo akauliza.

"Hapana, nipo naendelea na kazi, we tulia tu," Tracy alijibu. Khumalo alishtuka kwa sauti ile ngeni akataka kugeuka kuona ni nani huyo. Akachelewa. Tracy kwa nguvu zote za mkono wake wa kulia alipiga pigo moja la '*finger*' kwenye uti wa mgongo (*lumber vertebrae),* kwa vidole vyake viwili; cha gumba na cha kati. Alikamata uti wa mgongo na kuuvuta juu. Akatenganisha pingili zake. Khumalo, alikuwa kama kapigwa shoti ya umeme. Aliganda, macho yamemtoka na kinywa kimeachama. Mwanamke yule alipohakikisha mtu wake hana uhai, na zile pingili zilizoachana zimetokeza juu lakini bado ziko ndani ya ngozi. Akapiga kapigo ka wastani kwa kutumia kiganja cha mkono zikarudi kama zilivyokuwa. Khumalo akalala kimya, Tracy alikuwa amevunja pingili za uti wake wa mgongo na kukata kabisa *spinal cord* upande wa juu kama unakuja shingoni. Ganzi kali ikampanda Khumalo, uhai wake ukaondoka ndani ya sekunde kumi tu za shambulizi hilo.

Tracy akageuka na kumuona yule mwanamke akiwa amechanganyikiwa hajui afanye nini. Akatabasamu. Akamchukua na kumwingiza kwenye chumba cha

kubadilishia nguo. Akamfungia kwa nje, akatoka na kuufungua mlango, akawakuta wale askari wawili pale nje. Akajua akiondoka tu mambo yatabadilika. Akawaita ndani, akawaambia kuna shida. Wakaingia. Kosa! Aliwakamata na kuwagonganisha vichwa kwa nguvu wakaanguka chini hawana fahamu. Akatoka mlangoni na kuufunga kwa nje, taratibu akatoka mpaka mapokezi na mwisho nje wa jengo lile. Ile taksi ilikuwa imefika, akapanda na moja kwa moja akaelekea Uwanja wa ndege. Kazi imeisha.

"*Boss*, nimemaliza kazi kwa mkono wangu bila vurugu kabisa," alimwambia Bwana Robinson kwa simu.

"Oh, hongera sana mwanamke, fika haraka Ontario, nakusubiri," Robinson akamjibu.

Saa nne na nusu ndege ya shirika la ndege la Amerika iliiacha ardhi ya Durban na kuondoka zake huku ndani yake ikiwa imetorosha muuaji hatari bila kujua.

* * *

"Nani anaiweza hiyo kazi?" waliulizana.

"Hatuna budi kuwa wapole hapa," mwingine alijibu, "kwa sababu inatubidi tupitie orodha ya wauaji makini duniani na wengi ni wale ambao hata sisi tunawasaka kwa

tukio moja au jingine, lakini sasa hatuna budi kufanya nao urafiki kwanza, je watatuamini?" utata ulianzia hapo.

Hayo yote yalijadiliwa wiki mbili kabla ya Bwana Touzony kukutana hapo katika mnara wa Eiffel na marafiki zake hao.

Iliwashwa kompyuta yenye makabrasha ya siri, jina lililowadondokea wote ni la huyu mwanamke Tracy Tasha aliyeonekana kwenye picha akiwa mrembo, aliyevaa bikini na kujilaza juu ya mchanga wa fukwe Fulani huko duniani. Walipochambua rekodi yake waliona mauaji mbalimbali aliyowahi kuyafanya. Mauaji ya kitaalamu zaidi, kati ya yote ni asilimia ndogo tu ya hayo alitumia bunduki lakini yaliyobaki alitumia mikono, sumu, kemikali na silaha ndogo ndogo. Hapa ndipo walipoona mauaji ya mwisho aliyoyafanya kule Durban miezi sita iliyopita. Wakamhusudu. Wazo likaja la kumtumia mwanamke huyo. Waliona kwa uanamke wake ingekuwa rahisi kumnasa mbaya wao. Majadiliano yakaendelea kwa muda wakakubaliana la kufanya. Tracy atafutwe apewe kazi.

"Usimwambie kama umetumwa na hii idara, we mpe picha mwambie cha kufanya," sauti nzito ya mkuu wa taasisi hiyo ya kijasusi ya KGB ilimpa maagizo kijana mmoja shababi ambaye ilibidi aonane na Tracy uso kwa uso.

*   *   *

Nje ya mji wa Florida huko Marekani, katika mashamba makubwa ya mahindi na ngano, nyumba moja ndogo iliyojengwa katikati ya shamba hilo iliwahifadhi watu wawili wa jinsia tofauti juu ya kitanda chenye ukubwa wa wastani. Mvua ya rasharasha ilikuwa ikiendelea huko nje, baridi kali lilishika hatamu na kufanya nje kutotokeka. Tracy alikuwa na mpenzi wake wakipeana mapenzi mazito wakipambana na baridi hiyo.

Ni wakati wakiwa katikati ya mahaba mazito, simu ya mezani ikaita kwa fujo. Mwanamke huyo akanyosha mkono wake na kuinyakuwa. Akaiweka sikioni tayari kusikia nani anapiga na nini anasema.

“Hellow!” aliita kwa sauti ya mahaba kiasi kwamba mtu wa upande wa pili alichelewa kujibu labda kwa ganzi iliyopenya mwilini mwake.

*“Yeah, unaongea na Laurent kutoka Ujerumani,”* sauti ilisema.

“Biashara au mapenzi?” Tracy aliuliza.

*“Biashara,”* akajibiwa.

“Wapi?” akauliza

*"Paris,"*

"Baada ya saa kumi kutoka sasa, nitakuwa kwenye Metro kutoka London kuelekea Paris, unipe maelekezo, kama nitavyokupa maelekezo … usisahau hundi ya Paundi za Kiingereza iliyoshiba na kutakata," akakata simu.

*   *   *

Treni ya kutumia umeme kutoka London kwenda Paris ilikuwa katika kasi ya ajabu. Treni hiyo iliondoka London saa moja baada ya ndege ya America Airline kumteremsha Tacey. Laurent alikuwa ndani yake ameketi peke, kiti cha mbele yake ambacho alitegemea kuketi na Tracy hakikuwa na mtu. Akaitazama saa yake akajaribu kufananisha.

*Atoke Marekani afike London tuonane kwenye Metro ndani ya masaa kumi*… alijiwazia huku akiendelea kunywa kinywaji chake taratibu. Akiwa katika mawazo huku akitazama dirishani akajikuta hayuko peke yake tena. Akageuka na kukutana uso kwa uso na mtu asiyemjua, mwanaume mwenye sura ya kitoto. Mtu huyo hakuwa na maongezi marefu.

"Nipe mzigo," akamwambia Laurenti. Kijana huyo akapigwa na butwaa akiwa hajui nini cha kufanya.

*Huyu ndo Tracy?* Akajiuliza. Hakupata jibu.

"Muda unakwenda, nipe mzigo," yule kijana akakazia kauli yake. Laurent akampa bahasha, yule kijana. Akaifungua na kutoa picha tano tofauti za Bwana Touzony, kisha hundi ya Paundi za Kiingereza Laki moja.

"Ok, anapatikana wapi?" akauliza.

"Paris Ufaransa," Laurent akamjibu. Yule kijana akasimama na kuondoka kuelekea behewa la nyuma.

Laurent akaingiwa na wasiwasi, *vipi kama huyu si Tracy?,* akajiuliza. Akainuka kumfuata, akamuona akiishia katika mlango wa behewa la nyuma yake. Akamuwahi, lakini alipofika kwenye lile behewa, hakuomuona yule mtu. Kapotea. Lauretnt akajua kama sio jinni basi shetani, akarudi kitini kwake na kuketi.

Alijaribu kuyatauliza mawazo yake dhidi ya mtu huyo lakini haikuwezekana. Akajiuliza itakuwaje kama atakuwa kampa mtu mwingine pesa na picha ya mlengwa. Ubongo wake ulisawajika kwa mawazo mapya. Aliamua kumsaka mtu huyo kabla treni ile haijasimama. Alizunguka kila behewa kuangalia lakini hakumuona hata wa kufanana naye. Laurent hakujua la kufanya aliinua simu yake na kupiga kwenda namba anayoijua yeye. Simu ikapokelewa, ilikuwa ni

ya mmoja wa watu waliompa kazi na alitakiwa atoe taarifa mara tu akionana na Tracy. Alijua kwa vyovyote atapata shida kueleweka kwa uzembe alioufanya. Lakini alishangaa alipoambiwa *'well done'* na kisha simu kakatwa.

* * *

Akiwa ndani ya suti nyeusi iliyobeba umbo lake la kike lililovutia wanaume waliokuwa wakimwangalia wakati akishuka katika gari lililomleta. Kila mtu alimwangalia mwanamke huyu wa kizungu lakini ngozi yake ilikuwa imepoa kwa rangi, ilikuwa kama aliyekaa juani muda mrefu. Miwani nyeusi iliyaficha macho yake ya bluu, *macho ya paka*. Viatu virefu vyeusi vilimbeba na kumfanya atembee kwa mwendo wa madaha. Alizivuta hatua za wastani kuelekea pale kwenye ule mnara mkubwa kabisa na maarufu duniani. Mnara wa Eiffel uliopo *Champ de Paris*, mnara mkongwe uliojengwa kati ya miaka ya 1887 na 1889. Mnara uliojengwa kwa vyuma tupu, uliosanifiwa kitaalamu na Stephen Suvestre, wenye sakafu tatu na lifti tisa za kukupandisha juu na kukushusha chini.

Tracy, aliingia kwenye moja ya lifti hizo na kunyanyuliwa kuelekea juu kwenye sakafu ya tatu ambako ndiko liliko windo lake. Akafika na kutoka ndani ya lifti hiyo.

Ulikuwa mgahawa mkubwa uliokusanya watu mbalimbali wenye pesa, wakila na kunywa wanachotaka, pesa zilikuwa zikiteketea na kujaza matumbo yao yasiyoridhika. Danford Touzony, pamoja na rafiki zake walikuwa wakiendelea kuburudika pasi na hili wala lile. Walikunywa wakacheka, waliongea na kufurahi. Mwanadada mmoja mhudumu wa mgahawa huo, alikuja mpaka kwenye meza ya watu hao. Meza aliyoketi Danford, akamnong'oneza mmoja wa watu waliokuwa na mtu huyo kwa kuwa haikuwa rahisi kumfikia mlengwa. Ukimya ukachukua nafasi.

"Kuna simu ya mheshimiwa," yule mwanadada alimwambia huyo mtu.

"Ok, nakuja kuisikiliza," akajibu yule mtu.

"Hapana, simu imesisitiza kuongea moja kwa moja na Mr. Danford," yule mwanadada alijibu. Kauli hiyo ilimfanya yule bwana kufungua macho ya akili yake. Jukumu alilopewa ni kuhakikisha usalama wa mtu huyo, mtu aliyeitwa *'muhimu'* na serikali ya Ufaransa. Danford Touzony alisimama na kuelekea kwenye kile chumba cha simu, Kama kawaida, nyuma yake alifuatwa na yule bwana kwa ajili ya ulinzi.

Tracy Tasha, alikuwa katulia katika meza moja iliyojazwa vinywaji akinywa polepole huku jicho lake

lililokuwa nyuma ya miwani yake likimwangalia Danford. Mkononi mwake alikuwa amekamata kidubwasha kidogo kama rimoti yenye ukubwa wa kidole gumba. Alikitumia kidubwasha hicho kutafuta namba ya simu ya moja ya vijichumba vya simu katika mgahawa huo. Akaipata. Kwa kuunganisha na kipini kilichobanwa sawia katika pua yake chenye uwezo wa kunasa sauti na heleni iliyoweza kumfikishia ujumbe, akapiga namba ya simu ile. Ililipopokelewa akatoa ujumbe wa kutaka kuzungumza na bwana huyo yeye mwenyewe na si mpambe wake. Alichanganyikiwa kidogo kuona badala ya mlengwa wake tu kuinuka aliinuka na mtu mwingine.

"Shiit!" aling'aka kwa sauti ya chini, akaibana vyema ile rimoti mkononi mwake kisha akasubiri kidogo. Alimtazama Touzony, aliyeukaribia mlango wa kile chumba. Touzony akampa ishara yule bwana aliyekwenda naye, asubiri hapo nje ya mlango wakati yeye anapokea simu hiyo. Lakini kabla hajaingia, yule bwana alitangulia kwanza akatazama ndani ya chumba kile. Hakuna jipya, akampa ishara bwana Touzony ya kuendelea kuongea na simu yake. Touzony kaingia na kuuchukua mkonga wa simu uliokuwa umeegeshwa juu ya kijimeza kidogo na kuuweka sikioni.

Tracy alimtazama kwa chati kwa mtindo wa kugeuka kiufundi, Alikuwa akisubiri ainue mkono wa simu auweke sikioni, ili afanye yake.

Danford Touzony, aliingia ndani ya kile chumba na kuinua ule mkono wa simu. Akauweka katika sikio na ile sehemu ya kuongea akaiweka kinywani.

"*Oui,*" alianza kwa kuitikia kana kwamba kuna kitu alikuwa ameambiwa. Ghafla akajisikia kama anapaliwa. Akakohoa kusafisha koo. Haikusaidia. Akakohoa na kukohoa. Touzony akajikuta anaishiwa nguvu, akaanguka ndani ya chumba kile. Akajishika shingoni huku akikohoa kwa nguvu. Punde tu, mlango ulisukumwa na yule aliyekuwa nje akaingia na kumkuta bosi wake akigalagala chini. Akaomba msaada, na wengine wakaja. Wakamsaidia kumbeba Danford. Haraka haraka akawekwa kwenye machela iliyofikishwa hapo na watu wa huduma ya kwanza. Huekaheka zilikuwa kubwa, za kumsaidia kwa hili na lile. Kwa ujumla hali ilikuwa tete katika mgahawa huo. Danford alipakiwa kwenye helikopta ya shirika la Msalaba Mwekundu na kuondolewa kutoka hapo kukimbizwa hospitali huku akiendelea na matibabu akiwa angani.

Tracy Tasha, alirudisha rimoti yake katika mfuko wa suruali huku akitikisa kichwa kukubaliana na lililotukia.

Akainuka kutoka pale alipoketi na kumalizia kinywaji chake kisha akateremka chini kwa kutumia lifti. Huko nje waandishi wa habari walijaa wakimbana maswali askari polisi mmoja aliyeonekana kuwa ndiyo msemaji. Tracy alipita taratibu na kutokea nyuma ya kundi lile, huku akiacha askari kadhaa wakipanda kule kwenye ule mgahawa wakiwa na uhakika wa kupata lolote.

Danford Touzony alifikishwa katika hospitali ya A.p.h.p mjini Paris. Harakaharaka, huku akiwa amewekewa vifaa maalum vya kumsaidia kupumua na chupa za maji zikifanya kazi yake ya kumuongezea maji mwilini hata kama hayakupungua. Machela iliyombeba ilikuwa ikisukumwa na vijana nane waliokuwa wakikimbia nayo kupita kwenye korido ya hospitali hiyo kuelekea chumba maalu mcha uchunguzi. Akiwa juu ya ile machela, Danford Touzony alikuwa alilala kimya, na macho yake akiwa ameyafumba. Dakika moja ilitosha kumfikisha katika chumba kilicholusudiwa. Aliteremshwa na kuwekwa kitandani. Wataalam wenye vifaa vya kisasa walimzunguka, kila mmoja akiwa na kazi yake. Mpishano wa humo ndani hakika ulionesha ni jinsi gani hospitali za wenzetu walivyo makini na kazi yao na jinsi walivyojali uhai wa mwanadamu.

Tracy Tasha aliwasili kwenye hospitali ile, akasimama katika mlango wa chumba hicho hicho alicholazwa Danford Touzony. Hakuna aliyeruhusiwa kuingia. Vidirisha viwili, vidogo, vilivyotengenezwa katika mlango na kuwekwa kioo kinene vilimruhusu kuona kile kinachoendelea. Danford aliyekuwa kimya kitandani akizungukwa na mitambo tiba pamoja na wauguzi wachache ambao walikuwa wametingwa na kutafsiri michoro na tarakimu mbalimbali zionekanazo katoka mitambo tiba hiyo. Mwanamke huyu, alitaka kuhakikisha kuwa kazi yake imefanikiwa au la. Kwani sumu mbaya aina ya *Cyanide* ilikuwa imefanya kazi yake.

Mara ghafla, moja ya mtambo tiba ilianza kutoa majibu ya ajabu kidogo, wale wauguzi walionekana kuchanganyikiwa, walishika hiki wakashika kile. Mmoja wao akabofya kitufe fulani kilicho karibu na kichwa cha mgonjwa. Tracy aliona madaktari wengine kama wanne wakikimbia kwenye korido kuja pale kwenye kile chumba. Akawapisha. Wakaingia na kuanza kushika hapa na pale. Mmoja wao alionekana kujishika kichwani ilhali wengine walichukua vifaa vya kutumia umeme na kujaribu kumwamsha Danford. Walijaribu na kujaribu lakini haikuwezekana. Wakakubaliana na kilichotokea. Wakatazamana kwa huzuni, kifaa kimoja baada ya kingine kikaanza kuondolewa mwilini mwa mgonjwa na shuka jeupe

likavutwa mpaka usoni. Hakukuwa na jambo jipya, Danford Touzony alifariki dunia.

*   *   *

Watu watano, vijana wa makamo waliovalia suti nadhifu nyeusi waliingia kwenye kile chumba wakiongozwa na daktari mmojawapo. Walimpita Tracy aliyekuwa ameketi kwenye viti vilivyojipanga kando ya ukuta wa korido hiyo pana. Mwanamke huyo alimtambua mmoja wa wale watu, alikuwa ni ofisa katika maofisa wa juu wa idara ya kijasusi ya Ufaransa. Waliingia ndani ya kile chumba, hawakuwa na la kufanya zaidi ya kuondoa shuka juu ya ule mwili na kuutazama kwa masikitiko huku wote wakiwa wameshika mikono yao kwa mbele. Baada ya dakika kumi hivi walitoka. Pale koridoni, mmoja wao alimuona yule mwanamke akiwa ameketi kakunja nne akisoma gazeti kana kwamba kuna mtu anayemsubiri. Alipohakikisha watu wale wameondoka kabisa na kile chumba hakina mtu isipokuwa mwili wa marehemu tu, aliinuka taratibu na kwa kutumia funguo yake inayoweza kufungua vitasa asilimia kubwa ya milango duniani, alifanikiwa kuingia ndani ya kile chumba. Kwanza akasimama mlangoni pembeni kidogo, akatazama kwa umakini kisha akajivuta na kuuendea ule mwili, akakamata kidani alichovaa marehemu akakata na kukitia mfukoni.

Mara akasikia watu wakiongea nje ya mlango, akainama na kujificha chini ya kile kitanda, walipokuwa wakifungua mlango, akajivuta na kujificha pembezoni mwa kabati, akaiziba kwa mapazia marefu ya dirisha. Wale watu wakafika na kitanda kingine, wakamtoa marehemu na kumweka kwenye kitanda kingine kisha wakatoka nae nje ya chumba hicho. Dakika moja baadae, Tracy akatoka na kuufunga mlango kisha akatokomea anakokujua yeye.

# 1iii

## Dar es salaam - Tanzania

MADAM S aliipokea nukushi iliyoingia ofisini mwake. Ilipomaliza kuandika, aliivuta ile karatasi na kuichana, akaiweka mezani kabla ya kuisoma. Akainuka na kuiendea meza ndogo iliyo pembezoni kabisa mwa ofisi hiyo. Akawesha birika la umeme na kujitengenezea kahawa. Aliporudi akaketi tena mezani kwake na kikombe mkononi, na kunywa taratibu. Alikwishahau kama kuna nukushi iliyoingia muda huo. Umri ulikwishaanza kumtupa mkono.

Akachukua kitenza mbali na kuwasha luninga kubwa ilifungwa ofisini hapo. Taarifa ya habari kutoka kituo cha *Al-Jazeera* ilikuwa ikipepea hewani. Habari iliyokuwa wakati huo ilimvutia sana Madam S. Hakuamini anachokitazama na kukisikia. Habarai ile ilihusu kifo cha Danford Touzony. Mtangazaji aliipamba ikapambika. Lakini kwa kuwa aliikuta katikati, hakuelewa hasa mtu huyo amekufaje.

*Wamemuua au kajifia kwa mapenzi ya Mungu?* Akajiuliza pasi na kupata jib kwani tayari habari ile ilikwisha na kuanza

nyingine. Akaiinua simu yake, akabofya namba fulani na kuweka sikioni.

"TSA 1," akaita.

*"HOT"* akajibu.

"Washenzi wameshafanikiwa…" akamwambia.

"Kitu gani Madam?"

"Touzony amemalizwa,"

"Nini? Touzony Danford! Huyu ambaye Ufaransa walitamba kuwa hatokuja kukamatika?"

"Huyohuyo, nilikuwa naangalia habari hapa sasa hivi…"

"Walimpania, fainali wamefanikiwa! Dah dunia haina urafiki" Amata akamjibu. Wakazungumza machache kasha simu ile ikakatika.

* * *

Kamanda Amata akabaki kimya akitafakari hilo aliloambiwa na bosi wake. Ilikuwa ni taarifa ambayo hakuwahi kufikiri kama ataisikia kwa mtindo huo. Akajaribu kutafuta stesheni ya luninga anayoweza kupata habari ile. CNN ilikuwa bado ikiirusha habari hiyo kama makala.

Aliifuatilia kwa makini, kasha akamwita  Gina, wakaungana kutazama habari hiyo ya tukio lililotokea huko Paris saa chache zilizopita.

“Lazima muuaji ni mtaalam anayeijua kazi yake,” Amata alimwambia Gina.

“Kwa nini?” Gina akauliza.

“Kwa kuwa Touzony alikuwa anapewa ulinzi mkali sana, haikuwa rahisi kumpata, wamejaribu kila mbinu ya kumuua lakini wameshindwa, ila sasa mbinu waliyoitumia inanitia wazimu,” Kamanda Amata alieleza.

“Kwa nini wasema hivyo, unafikiri atakuwa ameuawa?”

“Bila shaka, ameuwa, kwa jinsi wanavyoeleza itakuwa sumu ya *Cynadine* iliyowekwa kitaalamu kwenye mkono wa simu, muuaji lazima awe mtaalamu sana,” Kamanda alimweleza Gina.

“Sasa, kama simu iliwekwa sumu si wangekufa wengi Kamanda!” Gina alionesha kutoelewa katika kifo hicho.

“Usijali Gina, utajua tu wanavyofanya,” akamwambia Gina ambaye alionekana kutokuelewa jinsi gani mtu anaweza kuuawa kwa mtindo huo, “ yaani hapa muuaji anakusoma mwenendo wa maisha yako ili ajue wapi

atakupata kirahisi. Hainiingii akilini kuwa hawajamkamata muuaji au hata kumshuku, lazima alikuwa hapo hapo," akamgeukia Gina aliyekuwa kasimama nyuma kando yake, " tabia ya wauaji kama hawa hupenda kufuatilia kujua kama mtu wao amekufa au la, hivyo huyu kwa vyovyote alikuwa pale pale sema tu kawazidi ujanja kwa namna moja au nyingine," akamweleza.. Gina alisikiliza kwa makini sana na kutikisa kichwa kuonesha ameelewa. Mara simu ya mezani ikaita kwa fujo, Gina aliyekuwa karibu nayo akainyakua na kuiweka sikioni.

*"Namuomba Amata tafadhali,"* sauti ya upande wa pili ikasema. Gina akampa simu ile Amata, naye akaichukua na kuiweka sikioni.

"TSA 1" akaitika.

*"Fika Ofisi Ndogo hapa haraka iwezekanavyo,"* ilikuwa ni sauti ya Madam S.

"Sawa!" akajibu na kukata ile simu.

Dakika kumi baadae alikuwa katika ofisi ya Madam S. "Nimefika!" akamwambia.

"Hata mi nakuona, keti…"

Amata akaketi kitini mkabala na mwanamama huyo, akisubiri ujumbe anaoitiwa.

"Hakuna jipya nililokuitia Amata. Nimepata taarifa kwa njia ya nukushi kutoka Ufaransa," akamwambia na kumpatia ile nakala. Amata akaichukua na kuisoma

Ilikuwa ikieleza juu ya tukio la kifo cha Touzony, taarifa hiyo iliyotoka katika shirika la kijasusi la ndani ya Ufaransa ilikuwa ni kuomba usaidizi wa kupatikana muuaji huyo kutoka katika mashirika mengine makubwa duniani. Kwa mara ya kwanza taarifa hizi zilifika katika shirika la kijasusi la Tanzania, TSA. Kulikuwa na picha kama kumi zilizoambatana na taarifa hiyo zikionesha yule anayesadikiwa ni muuaji. Picha hizo ziligawanywa makundi matatu, na zilikuwa za watu watatu tofauti, ambao kwa maelezo ya taarifa hiyo ni kwamba watu hao waliingia katika chumba hicho na kutumia simu hiyo kwa tofauti ya dakika ishirini kwa wastani. Kati yao mmoja alikuwa mwanamke.

Inaweza kuwa tofauti na wengine waliopata picha na taarifa ile, Amata aliziweka kando zile mbili za wanaume na kuichukua aile ya mwanamke.

"Mbona unazitenga hizi?" Madam S akamuuliza.

“Najua kuwa kama taarifa hii imefika kwenye mashirika mengi, basi akili zao wataelekeza kwa hawa wanaume. Mimi, hapana, naweza nikakwambia kuwa hakuna muuaji mbaya na mwenye mbinu hatari kama mwanamke,” akasema.

“Kwa hiyo…”

“Nina uhakika huyu mwanamke anaweza kuwa muaaji…” kimya kidogo kikapita kati yao, “ina maana wao wameshindwa kumkata ndani ya wigo wao?”

“Unajifanya hujui mambo haya? Jasusi kama wewe lazima ajue mbinu zote mbili, yaani kuua na kutoroka na kumsaka muuaji. Hawa wanaamini kabisa kuwa muuaji ambaye anaweza kuwepo kati ya wale watatu kuna mawili, ama yupo nchini pale au tayari anaelea angani akitoroka nchi, ndiyo maana wameomba msaada huu,” Madam alitoa jibu.

“Ok, kazi yetu ni nini?” akauliza tena.

“Kuweka ulinzi na kubaini kama mtu huyu au mmoja wa hawa ataonekana hapa nchini tuwape taarifa,”  Madam S akamwambia Amata huku akimwangaliza usoni.

“Kwa hiyo tukiwapa taarifa watakuja kumkamata?”

“Ndiyo maana yake,”

“Kama walishindwa kumkamata pale pale wataweza huku? Ok, basi mi nafikiri hii kazi iko chini yetu, sio kiwango chetu, watawanyie hiyo taarifa idara ya usalama wa Taifa wa ndani ili waweke mitego yao uwanja wa ndege, bandarini na sehemu zozote zinazotumika kuingia au kutokea watu nje ya nchi,” Kamanda akatoa maoni.

“Niliwaza hivyo,” Madam akaunga mkono. Mazungumzo mengine ya muda mfupi yakaendelea kati yaw at hawa wawili. Wakaweka baadhi ya mikakati myepesi kwa kazi hiyo.

* * *

**Mwaka Mmoja Baadae**

Ndani ya chumba maalumu ambacho hakuna aliyekuwa akikijua zaidi ya watu hawa watatu, kulikuwa na kikao kizito kikiendelea. Kikao cha siri kwa mambo ya siri. Walikuwa wakijadiliana swala zito kidogo lililoonesha kuwachanganya akili watu hawa. Walikuwa watatu tu walioketi kwa kutazamana lakini ukiwaangalia hawakuwa kutoka sehemu moja; mmoja alionekana Mzungu kabisa, mwingine alikuwa mweusi na wa mwisho alikuwa yupo yupo tu; Mwarabu si Mwarabu, Mchina si Mchina ilimradi alizaliwa na anaishi, ilitosha.

Yule Mzungu aliyeonekana kuchanganyikiwa, aliwatazama wenzi wake hao wawili waliongia hapo muda si mrefu japo kwa tofauti ya dakika kadhaa.

"Tusipoangalia tutapoteza kila kitu," akawaambia wenzake hata bila ya salamu.

"Na mi nilijua tu, nilijua huyu jamaa si wa kumwamini sana, ni ndumilakuwili," akadakia yule asiye na uraia .

"Amekiuka, utaratibu. Kama mnavyojua tulikubaliana kugawana migodi, Mwadui, Buzwagi na Bulyanhulu ili tumfanikishie yeye mambo yake. Sasa tumemuwezesha, mabillioni ya dola tumetumia, leo hii anataka kuwapa mali watu wengine, huyu ana akili kweli huyu?" yule Mzungu aliyeonekana kama mwenyekiti wa kikao aliongea kwa hasira zilizochanganyika na uchungu. Mara kwa mara alikuwa akifuta kamasi jembamba lililokuwa likitoka katika tundu za pua yake.

Walikuwa, wafadhili. Wafadhili waliomfadhili wanayemjadili, aliyonekana kukiuka masharti ya ufadhili huo. Mkataba. Mkataba wa mafanikio, unaotoa udenda wa wenye uchu wa madaraka.

"Haina haja ya kupoteza muda, tuonane nae haraka atueleze kama inawezekana au la, baada ya hapo tutajua la

kufanya. Sisi sio watoto, tunajua tufanyalo," alisema yule Mwafrika. Baada ya mazungumzo marefu kati yao waliamua kumtumia nukushi maalumu mtu huyo ili wajue nini kinaendelea kati ya mikataba yao.

"Tukutane tena hapa hapa baada ya masaa sita, najua, tayari tutakuwa na jibu kamili. Kazi hii nakupa Namba Tatu uonane na ndugu yetu, utuletee mustakabali, ili leo hii tuiache ardhi hii tukiwa na jibu," yule Mzungu aliyeonekana kuwa kinara kutokana na cheo chake katika jopo hilo alimaliza na kufunga kikao hicho kifupi. Kila mmoja alipita kwenye mlango wake alioutumia kuingilia, hakuna aliyejua mwenzake kaenda wapi na anafanya nini.

* * *

Kilikuwa chumba kilekile, kama walivyokubaliana, walikutana tena, sasa wakiwa na shauku ya kusikia habari za huyo waliyemtuma, Namba Tatu.

"Tuambie!" Kinara alifungua kikao kwa neno hilo.

"Nimeonana naye mwenyewe," yule aliyetumwa akaeleza.

"Amesemaje, maana muda unazidi kwenda," akadakia yule asiye na uraia wa maana.

"Nimeongea naye kwa muda wa dakika ishirini na tano, ana kwa ana, anasema yeye kwa kuwa tumemsaidia hana budi kulipa fadhila. Na katika kulipa fadhila ana mlolongo wa watu ambao wote wanahitaji malipo hayo tukiwamo sisi, hivyo amepanga mambo haya kwa awamu…"

"Kwa awamu!" alishtuka yule Kinara.

"Ndiyo kwa awamu, na sisi ametuweka kundi la mwisho," akamalizia kusema.

"Anatuchezea! Anatutania! Hajui tulilokubaliana au amesahau yale aliyotuahidi tulipokutana pale Madrid? Sina muda wa kusubiri, kilichobaki ni kutekeleza kurasa ya mwisho ya makubaliano yetu, basi," alimaliza yule Kinara.

"Samahani Kinara, kabla ya kurasa ya mwisho kuna kurasa ya mkakati tuliyoifunga kwa pini za dhahabu," yule mwenye uraia bubu alidakia pia. 'Kinara' au kwa jina lake kamili Robinson Quebec, raia wa Canada, mlaghai, anayenunua viongozi wa Afrika na kuunyonya utajiri wao, alijikuta anatulia kimya kwanza.

"Oooh Shiit! Nilipitiwa, sasa tutamkumbusha baadae kadiri ya makubaliano na kisha tutaona la kufanya kama ni

kutekeleza kurasa ya mwisho au tufungue kurasa za siri,” Kinara akaongeza.

“Ok, nafikiri tutekeleze mkataba, tumkumbushe, lakini kurasa yetu ya mwisho iwe ya mwisho, nikiwa na maana kuwa tufungue kurasa ya siri kisha tumalizie kurasa ya mwisho kwa kuwa hii ya siri ipo katikati ya mkataba wetu,” akamalizia yule Namba tatu, mwafrika ambaye alikwa kama wakala wa siri wa Robinson ‘Kinara’ aliyesimamia mikataba hiyo kwa upande wa Afrika ya Mashariki.

Kikao kikafungwa na utekelezaji wa hayo ambao ni wa siri zaidi ukasubiriwa. Walichotakiwa wao kufanya ni kutoa taarifa wasipopajua juu ya kile kinachoendelea. Wakatawanyika.

# 1iv

## Miezi Mitatu Baadae

MSAFARA wa mkuu wa nchi ulikuwa ukipita katika barabara itokayo Bagamoyo kuja Dar es salaam. Msafara huo ulijumuisha magari sita yaliyongozwa na pikipiki ya polisi. Ndani ya Toyota Land Cruiser V8 alikuwamo Mkuu wa nchi, ametuna katika kiti cha nyuma huku pembeni yake ameketi '*First Lady*'. Siku hii slikuwa akitoka mapumziko ya mwisho wa juma na kurejea Ikulu kuendelea na kazi zake.

Kila mmoja alikuwa ametulia kwenye gari akifikiri hili na lile, mwendo kasi wa magari hayo ulifanya barabara yote kuachwa wazi na kuruhusu hizo tu kupita kwa mwendo wautakao. Walipokaribia dara kubwa katika eneo la Bunju. Jambo lisilotegemewa likatokea. Walinzi waliokuwa katika gari la nyuma walilishuhudia ile gari la Rais likiyumba na kuacha barabara. Likagonga mwamba wa daraja. Dereva alijitahidi kuliweka tena barabarani lakini ilikuwa ngumu. Lilijipiga tena na kunyanyuliwa juu kabla halijajibwaga chini nje ya barabara. Kitendo cha haraka, wale askari walikwisharuka chini na wale wa usalama wa taifa

walikwishateremka na kukimbilia eneo la tukio. Ulinzi mkali ukawekwa ili wananchi wasivamie eneo. Haraka sana makachero waliokuwa katika magari ya nyuma walishuka hai-hai na kuvunja mlango wa lile V8. Wakamtoa Rais salama japokuwa alikuwa na majeraha hapa na pale. First Lady alipoteza fahamu palepale.

Lilikuwa tukio lililovuta hisia za walio wengi, haikuwahi kutokea.

"Mkuu upo salama usijali, sasa hivi tunaelekea hospitali," kiongozi wa kitengo cha usalama mwenye jukumu la mwisho la kumwambia Mkuu *'Twende'* au *'Tusiende'* alimwakikishia usalama.

"Mke wangu yuko wapi?" akauliza.

"Yuko salama usijali," akajibiwa.

Kila kitu kilifanyika kwa uharaka sana, haikuchukua muda mrefu, helikopta ya jeshi iliwasili tayari kumwondosha Mkuu wa nchi na kumpeleka hospitali kwa matibabu.

* * *

Bunju Darajani, eneo lenye wakazi wengi na shughuli mbalimbali za kujitafutia maisha, maduka, magenge, baa, vilabu vya pombe za kienyeji, vyote hapo palikuwa ni mahali

pake. Siku hiyo ya tukio kila mmoja alikuwa kachanganyikiwa kwa namna yake. Hawakuwahi kuona tukio kama lile katika maisha yao seuze kulisikia tu katika historia ya taifa lao lililojawa na wingi wa amani, likisifiwa kuwa na weledi wa hali ya juu wa usalama na upelelezi. Baada ya hali kuwa shwari kabisa na kila kitu kuondolewa mahala pale ikiwamo gari iliyombeba Rais, watu walirudi katika shughuli zao lakini mazungumzo katika vikundi yaliendelea kubaki, vilabuni na hata katika magenge ya bangi.

"Ile mi niliiona tangu inavyoanza kutokea, lakini yule dereva mi namsifu aisee, unajua angekuwa kama madereva wetu hawa, sasa hivi tunashusha bendera nusu mlingoti. Lakini jamaa alicheza nayo mpaka ikagonga ukuta wa daraja, loh," kijana mmoja alisikika akipiga soga huku wenzake wakimsikiliza kwa shauku. Wote waliomzunguka walionekana kushabikia yale anayowasimulia.

"Yaani ilikuwa kama muvi, kaka zile gari zinakimbia ni balaa, dakika moja tu hapa walitanda *njagu* wa kutosha, wote hatukusogea pale tulikodoa macho kwa mbali tu," mwingine alidakiza mazungumzo, hakutaka apitwe.

Wakati mazungumzo hayo marefu yakiendelea, kijana mmoja aliyekuwa kwenye kazi maalum alikuwa ameketi

jirani na eneo hilo lakini aliweza kusikia yote kwa umakini kabisa huku akiyameza ili kuyakumbuka baadae. Alivaa kikawaida kabisa; jezi ya Taifa Stars na suruali ya jinzi. Hakuna ambaye angemzania kuwa ni mtu mwenye jukumu zito hapo alipo. Waliendelea kupeana stori.

Upande mwingine wa eneo hilo kulikuwa na wazee waliokuwa wameketi wakinywa kahawa na wengine wakicheza bao, mchezo uliopendwa na Mwl. Nyerere, huku wakitaniana na kuongea hili na lile. Wakiwa katika hali ile, alipita mzee mwingine wa makamo aliyevalia kanzu ya kawaida kabisa na baraghashia kichwani. Mzee huyo alipofika mahali pale akasimama na kuomba kujiunga katika mchezo huo. Kwa kuwa naye alijinasibu kuwa ni muumini wa mchezo huo, akakaribishwa. Watanzania hawana hiana siku zote, walimpa nafasi naye akawapa kikombe cha kahawa kila mmoja, wakafurahi na maisha yakaendelea. Mazungumzo ya wazee yakaendelea na kubwa lilikuwa lile lile la ajali ya msafara wa rais, yule mzee mgeni alikuwa akisikiliza na kuwapa maneno ya hamasa ili waongee zaidi.

"Ile ajali bwana! Hivi wewe kwa jinsi nchi hii ilivyokuwa na wana usalama machachari kabisa unafikiri mtu anaweza kuhujumu msafara ule! Hata siku moja! Abadan nakwambiaa, kabla hawajapita hapa panakaguliwa

pote… mnavyokaa kuwakodolea macho wengine mko nao hapo ni Usalama wa Taifa," mzee mmoja alikuwa akiongea kwa sauti ya juu huku akiendelea kucheza bao.

"Wewe mzee umesema, hii nchi kwa upelelezi hata F.B.I wanaiogopa, Gadafi mwenyewe alisalimu amri wakati wa vita ya Kagera..!" mzee mwingine akadakia.

"Lakini watu nao wajanja siku hizi wameendelea, unaweza kukuta mtu kaja hapahapa ili kuhujumu msafara! Siku hizi kuna maboko Haram, Al-Qaeda, na wengine kibao tu sijui na nani hawa wa Somalia… eee Ali- Shababu," aliongeza kusema yule mzee mgeni akiwa na haja ya kuwachokonoa wabwabwaje zaidi.

"Yaani mzee mwenzangu umesema, na hawa wageni wageni wanaokuja kujifana watalii sijui vidudu gani wengine wana mambo yao hawa. Sasa we' mzee Shomari yule mgeni aliyekuja juzi hapa yule mwanamke akapanga chumba pale Kibilisa Gesti hausi, hivi kweli we mzungu unaweza kupanga pale chumba, Gesti chafu, inanuka maana ni uzinzi kila kukicha," akadakia mzee mwingine.

Kwa habari hiyo yule mzee akatega masikio akijifanya ametingwa na bao lile kumbe alishtuka kidogo, kisha akadakia kusema, "Sasa we unashangaa yeye kukaa gesti

kama hiyo wale hata juu ya miti wanakaa, wenzetu sio kama sisi wanajichanganya popote," alisema.

"Wenzetu sio kama sisi mzee mwenzangu, yule mdada sijui mzungu alivyo pale au chotara, amekaa siku tatu hapa, yuko pale gesti ya Kibilisa," mazungumzo yakapamba moto.

Baada ya muda yule mzee mpita njia akaaga, akaahidi kurudi baadae kwa maadai kuwa kapenda kile *kijiwe*, akawanunulia kahawa.

*   *   *

Vijana wawili wa idara ya usalama walifika eneo la nyumba ya wageni ya Kibilisa majira ya saa nne usiku baada ya kuipeleleza na kuhakikisha hakuna mtu aliyetoka wala kuingia mwenye muonekano tofauti na Watanzania wa kawaida. Walipojiridhisha ndipo wakaijongelea na kulifikia dirisha la mapokezi. Mwanadada mwenye kila chembe ya ukarimu wa mwili na roho akawapokea.

*Mh! Hii kweli gesti!* Mmoja akawaza baada ya kumtazama msichana yule aliyekuwa akifumua nywele kwa chanuo la mti.

"Habari dada!" wakamsabahi.

“Salama, niwasaidie nini? Kama vyumba vimejaa,” akawajibu huku akiendelea na kazi yake.

“Asante, hatuhitaji chumba, sida yetu ni leja yako yaa wageni,” mmoja wao akamwambia yule mwanadada. Yule mhudumu akachomoa chanuo lake kutoka kwenye nywele zake na kuliweka juu ya kochi. Akatumbua macho kuwatazama vijana hao.

“Ya nini? Kwani ninyi ni nani?” akauliza huku akisimama kutoka pale alipoketi kwenye kochi kuukuu. Wakamwonesha vitambulisho vya idara ya uhamiaji. Yule mhudumu akawa mpole. Ni mara nyingi anawapokea watu wa idara hiyo, tofauti tu huwa hawaji kama hawa walivyokuja. Hakujiuliza, akavuta droo la meza yake na kutoa kile kitabu.

“Unaitwa nani?” mmoja wao akamuuliza yule mhudumu huku akiipokea ile leja isiyo na jalada upande wa juu na kujawa na karatasi zilizochakaa.

“Tano,” akajibu. Wakachukua lile daftari na kuanza kulikagua, kila chumba kilichokuwa na shaka kikatiliwa alama.

“Mgeni wa chumba namba ishirini na tatu yupo?” akauliza.

“Hapana ametoka tangu asubuhi hajarudi mpaka sasa,” akajibu.

“Ni Mtanzania?” wakauliza.

“Hapana, kwa maana hajui hata Kiswahili vizuri zaidi ya kile cha kuombea maji,” akajibu yule mfanyakazi huku akionekana kujawa na woga.

“Kwa nini hapa hukujaza namba ya pasipoti yake?” wakatupa swali lingiine. Yule mhudumu akabaki amebung’aa macho, hakuwahi kufikiri swali kama lile lingemjia siku moja. “Tueleze kwa kina, alikuwa peke yake? Na anajishughulisha na nini?” maswali yale yakamchanganya kwa kiasi fulani yule mhudumu. Akainama chini kwa jozi la sekunde kisha akarudisha macho yake kwa wale vijana.

“Yuko peke yake, ni mwanamke msichana tu, mwanafunzi wa chuo huko kwao…”

“Kwao wapi?”

“ Jamaica… kwa jinsi alivyoniambia. Kila siku huwa anatoka na kurudi usiku, ila leo bado hajarudi,” yule dada akaeleza kwa marefu na mapana. Wale vijana wakatazamana, hisia za jambo la hatari zikaawajaa.

“Tunaomba kukagua chumba chake,” wakasema. Hatua zikachukuliwa, mjumbe akafika na mlango wa chumba hicho ukafunguliwa kwa funguo ya akiba. Wakaingia ndani. Mlango ulipokuwa wazi mbele yao, wakabaki wametumbua macho. Chumba kitupu. Hakukuwa na kitu wala mtu. wakapekua hapa na pale mpaka juu ya dari lakini hakuna kilichoonekana. Wakakubaliana na kukifunga, tena kwa kuongeza kufuli jingine ili kisiguswe na mtu kisha wakamchukua yule mhudumu kwa mahojiano zaidi, wakaondoka naye.

* * *

Mtaalamu wa kuchora picha aliketi mbele ya yule dada katika kituo cha polisi cha Tegeta, akijaribu kueleza jinsi alivyokua akimuona yule mgeni katika sura tofauti. Mara akivaa kofia, mara akitoka na kilemba na kadhalika. Mtaalamu yule wa uchoraji, aliendelea kuchora na baada ya maelezo hayo, alizinakshi kwa muonekano mzuri. Akapata picha zipatazo kumi na tano tofauti tofauti, akamwonesha yule mwanadada. Haikumchukua hata sekunde mbili kuitazama, akaropoka, “Ni yeye, yaani kama umempiga picha vile,” akasema. Baada ya zoezi lile, zile picha zikawekwa katika bahasha na kukabidhiwa kwa maafisa wale kwa muendelezo wa msako dhidi ya mtu huyo.

Picha za mtu huyo zilisambazwa kila kona ambayo ina uwezekano wa mtu kupita na kutoka nje ya nchi; viwanja vikubwa vya ndege nchini, bandari, vituo vikuu vya mabasi na vituo vya reli. Zaidi ya hapo mahoteli makubwa ya Dar es salaam nayo yalikuwa kwenye taabu siku hizo, kukaguliwa na kupekuliwa kila dakika. Kila aliyeingia na kutoka alichunguzwa kikamilifu. Picha zilisambaa na siku chache baadae zilitoka magazetini. Kila mmoja aliziona, kila mwananchi alizitia machoni.

# 1v

MADAM S alishusha gazeti alilokuwa akisoma, *'Uhuru'*. Akaliweka mezani kabla ya kushusha pumzi ndefu. Juu ya gazeti hilo kulipambwa na picha ya huyo anayetafutwa ikiongozwa na maneno yenye wino mzito *'ANATAFUTWA'* na maelezo mafupi yaliyoeleza hasa juu ya wajihi wake yalifuatia.

*Watampata tu waongeze juhudi!* Akajiwazia huku akiendelea kutazama luninga yake ya ofisini. Akiwa ametekwa mawazo na akili katika kile kilichokuwa kikiendelea katika luninga ile, ghafla mlango ukafunguliwa, Kamanda Amata akaingia katika ofisi hiyo bila hodi, akaketi katika kiti akitazamana na Madam S huku akihema kwa nguvu kama aliyekuwa akikimbizwa.

"Vipi, mbona unakuja kwa shari?" Madam akamtupia swali.

"Hapana, ila kuna kitu kimenifurahisha leo," akajibu huku akimtazama bosi wake.

"Kitu gani?" Madam akapenda kujua.

“Mdunguaji, anayefikiriwa… ninayo picha ya mchoro wa jana, na nikiitazama inafanana sana na ile tuliyoletewa miezi ya nyuma kutoka Ufaransa” akajibu.

“*Come on* Kamanda, sikuwahi kufikiri hilo, hebu ilete hapa,” akasema huku akionesha ishara ya mkono kuwa apewe picha zile. Madam S alipokabidhiwa, akaitazama moja baada ya nyingine. Picha zile zilizochorwa Tanzania na zile zilizopigwa kwa CCTV kule Ufaransa, zilishahabiana kwa kiango kikubwa. Kweli alikuwa ni yuleyule jinsi alivyoonekana kwa sura yake. Madam S alijihisi kweli kuzeeka kwa kuwa hakuweza hata kugusika moyo wake alipoitazama ile picha gazetini.

“Kamanda,” akaita kwa utulivu huku akijiegemeza mezani, “unataka kuniambia yupo hapa?” akauliza kwa shauku japo alinong’ona.

“Sijui, labda ni pacha wake,” Amata akajibu huku akijiweka sawa kitini mwake. Madam S, akamtazama kijana huyu shababi, mjanja mwenye akili za haraka, kisha akatikisa kichwa.

“Hivi unajua idara ya usalama hasa kwenye maswala ya ulinzi wa viongozi itapanguliwa punde tu!” akamwambia Kamanda ambaye kwa hilo alikuwa hajui lolote.

"Uzembe?" Kamanda akauliza.

"Sikia Kamanda," Madam S akajiweka sawa kitini, "sio uzembe, bali tulizidiwa kete, unajua hii hali ya kujiamini kuwa nchi yetu ina amani inatubwetesha sana," alieleza kwa kukata tamaa, "kuna wageni wengi sana nchi hii, hata hawajulikani kazi zao, wengine wanajifanya watalii, sijui misaada ya kibinadamu, wanaitana tu wanajazana, ndivyo tunavyokaribisha Magaidi na wauaji wa kimataifa kama hawa Kamanda. Lazima vyombo vyetu vya usalama vibadilike sasa, hali ya kuaminiana imekwisha, huu ulimwengu mwingine huu, watu wako kazini, ooh! shauri yenu," akavua miwani yake na kuiweka mezani.

"Madam, usemayo ni kweli kabisa, tunafanya mambo kwa mazoea lakini madhara yake ndiyo haya sasa, tusemeje, alitaka kumuua Rais akashindwa akapasua mpira wa gari?" Kamanda akauliza.

"Hapana," akajibu Madam S.

"Kwa hiyo alidhamiria kufanya hivyo, hakukusudia kuua, unajua maana yake ni nini? Tunaamshwa usingizini Madam," Kamanda akaongeza huku mara hii akiwa kaiegemea meza ya Madam S. Baada ya nukta chache za kutazamana, akaendelea, "wao ndio walioshindwa, lakini maadam kafanya haya ndani ya ardhi ya Tanganyika

nakuapia, atapatikana tu awe hai au mfu," Amata alijibu kwa kujigamba.

* * *

Msako ulifanyika kila kona ya mkoa wa Dar es salaam, lakini ilikuwa ngumu kupatikana mtu anayefanana na picha ile. Siku tano zilipita hakuna jibu la matumaini zaidi ya kukamatwa tu wanawake wanaofanana kidogo na huyo lakini walipowahoji waliwaacha tu baada ya kugundua hata kushika manati hawawezi.

Lilipokamilika juma moja baadae, kama alivyosema Madam S, safu ya wanausala na wakuu wa idara za ndani ikapanguliwa na kufumwa upya. Wengine wakiwajibishwa kwa kutokuwa makini na kazi yao. Rais alibadilisha walinzi wake wa karibu na kuteua wengine. Hapa na pale, paligeuzwa hivi na vile, ilimradi tu kujaribu kuweka mambo sawa. Wale waliokuwa Ikulu walibadilishwa na kupewa idara nyingine ikiwemo kuwapeleka mikoani na wapya kabisa walipewa kazi ya ulinzi wa kuratibu ratiba zote za Mkuu wa nchi.

## Miaka Mitatu Iliyopita

## Copenhagen

Kikao cha siri kiliendelea katika moja ya hoteli kubwa ya nyota tano ndani ya Jiji hilo. Kikao hicho kilihudhuriwa na watu wasiozidi wataano, wazungu wane wenye pesa kwa mwonekano wao tu na Mwafrikaa mmoja aliyeonekana kuwepo kwake hapo ni kuomba msaada wa jambo fulani.

"Sisi tutamiza ombi lako. Kukufanya wewe ukae madarakani ndio kazi yetu, ukitazama kila kona ya Afrika tumeweka watu. Jukumu letu ni kuwawezesha ninyi wanasiasa weusi kuingia madarakani. Mkataba wetu kama ulivyousoma, ni *fifty fifty*. Yaani tutakufanikishia, utakaa madarakani. Msimu ni miaka mitano… uwe huru na ujipange kwa miaka miwili na nusu ya kwanza na miaka miwili na nusu ya mwisho huna budi sasa kutuwezesha na sisi kadiri ya makubaliano yetu yaliyomo humu, je unakubali? Kama unakubali basi we saini, maana kwa kusaini tu tayari umekuwa Rais wa Tanzania na umeingia rasmi kwenye mtandao wetu. Mkataba huu husimamiwa kama ulivyoeleza, haupindishwi. Ukikiuka…" akafungua kurasa ya tano kutoka mwish *'JIUE MWENYEWE'*

Mheshimiwa huyu alishusha pumzi na kusoma tena na tena kurasa hizo thelethini na tano zilizoandikwa kwa wino wa dhahabu, yalikuwa ni makubaliano mepesi sana

kutekeleza, hata ungekuwa wewe ni mepesi tu, hayakuhitaji damu ya mtu wala kiungo chake bali yalihitaji wewe kufanya watakalo wao.

"Na nikishindwa je?" akauliza yule Mmheshimiwa.

"Huwezi kushindwa, sisi ndio tunaweka watu madarakani, uchaguzi wa Rais mwaka kesho ambao wewe unataka kugombea utaigharimu dola ngapi serikali yenu masikini ya Tanzania?" akaulizwa naye akajibu kwa ufasaha kabisa.

"Ok, sisi tutakufadhili wewe na chama chako pesa za kampeni na mambo yote, alikadhalika tutawatengenezea karatasi na kalamu maalumu za kupigia kura na masanduku ya kupigia kura ambayo tunatumia teknolojia mpya inayoendana na karatasi hizo. Karatsi ukiziona ni za kawaida kabisa, lakini tunavyowapa kama ni karatasi milioni thelathini basi ujue kura zako za NDIYO ni milioni ishirini na moja bila kuharibika," akaambiwa, akafarijika.

"Hapo nimekuelewa comrade," akajibu Mheshimiwa.

"Basi ni hayo tu, lakini kumbuka, utatawala miaka miwili na nusu kwa manufaa yako na serikali yako, miaka miwili na nusu inayobaki ni kwa manufaa yetu, na jumuia yetu. Tutakuja kwa njia nzuri tu kama tulivyokwambia,

uwekezaji," yule bwana akamweleza mheshimiwa aliyekuwa akiutaka kwa hali na mali urais wa nchi. Uchu wa madaraka. Kila alipojaribu kumtazama yule bwana aliyekuwa akimwita comrade alishindwa kumuona sawasawa kwani kwa jinsi alivyoketi hakuonekana sura yake, hivyo mpaka anamaliza kuongea naye hakumjua ni nani.

* * *

Muda ulipofika, Watanzania wakaingia katika kipindi cha uchaaguzi mkuu. Wagombea wengi wakapitishwa majina yao na kampeni zikaanza. Wagombea walizunguka nchi nzima wakijinadi kwa sera zilizojawa maneno matamu kama asali. Ni Kobelo Mutandala aliyeonekana kung'ara, kampeni zake zilikuwa za kitajiri, alitembea kwa helikopta ya kisasa, aliahidi neema mpya na kumaliza zile za mtangulizi wake. Alikuwa na kila hali ya kushinda uchaguzi huo kwa kuwa chama chake ndicho kilishika dola tangu uhuru.

Muda ulipofika, misululu mirefu ya Watanzania wanyonge ikaonekana juani. Wananchi wakitumia uhuru wao wa kikatiba kupiga kura ya kumchagua wa kuwaongoza.

Kama alivyoahidiwa na mabwana wake, Kobelo aliukwaa uongozi wa nchi bila tabu tena kwa asilimia za kutosha, kura zilihesabiwa mara kadhaa kwa kushuku kuwa wamefanya utapeli lakini jibu lilikuwa ni lilelile. Kobelo

Mutandala akaapishwa kuwa Rais na kushika hatamu za uongozi.

Ilikuwa miaka miwili na nusu ya neema kama ndoto aliyoiota Yusuph, alijitahidi kutimiza ahadi zake kwa wananchi kwa nguvu kubwa. Hakuna aliyegusa wala kumwuliza juu ya kubaliano lile, wafadhili wake walikuwa wakiangalia kutoka mbali kila linaloendela. Waliendelea kusubiri tu wakati wao ufike, nao waneemeke kwa kuitwaa migodi ya madini inayotoa madini kwa fujo bila kuchoka. walijuwa wazi kuwa ndani ya miaka miwili na nusu waliyokubaliana wangeweza kupata faida maradufu ya pesa waliyofadhili kwa kiongozi huyo.

Ulikuwa ni mkataba wa kitoto kwake, kuwapatia mgodi au migodi kwa majina tofauti tofauti na kila mgodi serikali itapata ingepata asilimia nne na wao watabeba zilizobaki. Mkataba wa kitoto, utakaowaumiza wananchi, ilhali wao wakicheka huku wakijikuna matumbo yao.

Walijijenga. Walikuwa na nguvu ya ushawishi. Waliweza kufanya lolote katika dunia hii, walileta migogoro isiyokwisha, na ninyi mkipigana wao wanabeba madini na rasilimali zenu kwa mbadilishano wa bunduki na makombora ya kisasa ili muendelee kuuana. Wakiwapa *condom* na dawa za uzazi wa majira ili msiendelee kuzaana,

wakiwapatia chanjo mbalimbali ambazo ni wao tu wanaojua kazi yake katika miili yenu. Leo hii tunashuhudia dada zetu kati ya kumi wawili watazaa salama na wengine mimba zitaharibika au kunusurika kwa msaada wa madaktari wenye utu ambao ni wachache sana hasa kwa wewe usie na *'njuruku'*. Wanafanya kila wanaloweza kutudunisha watutawale. Mtumbwi wa kibwengo.

**Miezi mitatu baadae**

**Mgodi wa almasi Mwadui**

Ndege ya serikali, *Foker Friendship*, ilitua mgodini hapo, mkoani Shinyanga. Walioshuka hawakuwa wageni sura zao; waziri wa nishati na madini, akifuatana na watu wengine kama wanne hivi. Wote wakaliendea lango kuu la mgodi huo. Hakuna aliyewazuia, walifunguliwa na kuingia, huku wakisindikizwa kwa ulinzi mkali wa mbwa na askari mpaka ndani ya jengo lenye ofisi za utawala. Katika ofisi hii wakapokelewa na mwanadada mrembo, Naomi, aliyekuwa katibu muhtasi wa ofisi hiyo. Akawakaribisha kwa heshima zote na kuwaruhusu kuonana na meneja. Wageni wale wakapita ndani na kumkuta waliyemtarajia. Dr. Justine McLean, alitulia akivuta mtemba wake kwa hesabu kali na kuuruhusu moshi kutoka kwa kupitia tundu zake za pua.

Baada ya kupiga pafu kama mbili hivi ndipo akawakaribisha na kuwaonesha sehemu za kuketi.

"Kama unavyotuona, hatuna muda wa kupoteza, ni dharula na ni lazima itekelezwe, tunahitaji almasi makasha yasiyopungua matano sasa hivi, ni amri ya serikali," yule waziri akamwambia Dr. McLean. Mshtuko dhahiri ukaonekana katika uso wa meneja huyo.

"Kuna utaratibu wa kufuata mheshimiwa, hata kama mgodi ni wa serikali, na wewe unajua hatua kwa hatua," akamjibu.

"Na mimi ndio waziri mwenye dhamana, na nina kibali cha Ikulu," akasema huku akitoa karatasi zake na kumpatia. Ilikuwa barua kutoka Ikulu iliyosainiwa na Rais mwenyewe na kugongwa mhuri wa wa Ikulu. Dr. McLean akarudisha karatasi ile kwa Waziri huyo. McLean akasoma kwa maini ile karatasi aliyokabidhiwa, akahisi mwili ukimtetemeka na ubaridi ukimwingia kutoka utosini mpaka unyayoni. "Hii baki nayo wewe kwa kabrasha lako kama utaletewa shida yoyote," yule waziri akamkabidhi naye akaipokea na kumwita Naomi.

"Naomi, nenda kwa mkuu wa bohari mwambie atoe kasha tano kubwa za almasi ampatie mheshimiwa, serikali inazihitaji kwa shughuli za haraka," Naomi hakuwa na

lingine, alitoka na kuiendea ofisi kama ya tatu kutoka pale alipo. Naye vilevile, katoa maagizo aliyopewa na michakato ikafanyika.

Wale wageni wakaendelea na mazungumzo ya hapa na pale wakati wakiwa ofisini huku vinywaji baridi vikiteketea. Vijana waliokuwa kwenye sare za polisi waliofuatana na waziri walikuwa wakisimamia zoezi la kupakia yale masanduku katika ile ndege. Haikuchukua muda, dakika kumi tu, zilitosha. Naomi akarudi ofisini na kufikisha taarifa ya kuwa zoezi limekamilika kisha yeye akatoka na kuacha wakuu hao wakiagana.

Mara baada ya wageni wale kuondoka zao, kila mmoja aliendelea na kazi kama kawaida. Naomi alikuwa ametingwa kuandaa taarifa mbalimbali za kampuni hiyo. Baada ya dakika kama thelathini hivi aligutushwa na mlio wa saa ya ukutani ukimwashiria kuwa saa saba ya mchana imekwishafika. Akakurupuka pale kitini kwa kuwa alijua wajibu wake kwa mkuu wake wa kazi. Kila ifikapo saa saba kasoro robo angehitaji kikombe cha kahawa. Naomi akafanya haraka kuandaa kinywaji hicho nalipokiweka chanoni akainua kuelekea ofisini kwa bosi wake.

Alaiusukuma mlango kwa bega lake na kuingia ofini humo. Alitegemea kupokelewa na tusi kama ilivyo kawaida

ya Mzungu huyo lakini alishangazwa na ukimya uliotawala. Alipotupa macho mezani, Naomi akajikuta akitokwa na chano ile mikononi na kuanguka chini huku kikombe na kibweta cha sukari vikipasuka. Dr. McLean alikuwa amelalia meza na damu nyeusi ikimtoka na kusambaa taratibu huku akichafua makabrasha kadhaa yaliyokuwa hapo. Naomi alipiga kelele za msaada  hakuna aliyesikia ndipo alipokumbuka nobu ya dharula iliyopo chini ya meza yake. Akaikimbilia huku mwili wake ukiwa umejaa hofu, akaibonyeza bila kuiachia. Haikupita hata dakika na dakika, walinzi waliingia kwa fujo na kumkuta Naomi akiwa bado kaing'angania ile nobu huku akionesha ishara ya mkono kuwa waelekee ofisini kwa Dr. McLean. Wote wakapigwa na bumbuwazi, kumkuta meneja wao katika hali hiyo ya umauti. Ilikuwa ni hali ya kuogofya sana, Naomi hakuweza kuielezea alibaki kimya muda wote huku akitetemeka na kuweweseka.

Nusu saa baadae polisi waliwasili katika eneo la tukio na kufanya utaratibu wao ikiwamo kuchukua maelezo, alama za vidole kila ilipobidi na picha za mwili wa marehemu kisha kuuondoa tayari kuuhifadhi.

"Mnafikiri nani atakuwa kafanya hivi?" wakauliza, lakini wafanyakazi wakabaki kutazamana.

“Mbona mnanitazama… haya nahitaji wafanyakazi wote hapa, haraka,” yule polisi mwenye cheo cha inspekta akatoa amri na baada ya dakika tano wafanyakazi wote wakafika, lakini walipotazamana mmoja hakuwepo.

“Hapa Boharia hayupo,” akasema fomeni wa mgodi.

“Yuko wapi? Na kwa nini hayupo? Naanza kumtilia mashaka, kamwangalieni ofisini mwake, mumlete hapa haraka, tunataka tufanye kazi,” akatoa amri. Lakini mlinzi aliyetumwa alirudi na jibu tata. Boharia naye alikutwa amekufa. Utata juu ya utata.

* * *

Madam S alibaki kinywa wazi, hakuelewa mambo yanavyoenda, likitoka hili linakuja lile na yote yamejawa utata. Akaitua simu taratibu kutoka katika sikio lake na kuipachika katika kikalio chake kwa jinsi hiyohiyo. Akaurejesha mkono wake mezani lakini hakugundua kuwa hata ukope wa jicho lake haukuwa ukifumba, hakutabasamu wala hakukasirika alibaki yupoyupo tu. Simu ilitoka Ikulu, ikimpa taarifa juu ya tukio la Mwadui.

“Haiwezekani, waziri! Waziri kabisa anaweza kufanya hivyo?” alijiuliza kwa sauti ya chini ambayo mtu wa pili hasingeweza kuisikia. Akainuka na kuiacha meza yake, kisha

akakiendea kioo kikubwa kilicho pembeni ya ofisi yake, akajitazama na kujiona jinsi umri unavyomuacha.

*Yanipasa kupumzika na kazi hizi zinazonipa msongo wa mawazo kila kukicha!* Akawaza. Akairudia meza yake, akainua simu na kubonyeza tarakimu kadhaa, akaitega sikioni.

"Uje sasa hivi, acha lolote unalofanya," akakata simu mara tu alipomaliza kusema hilo. Akajibwaga kitini na kupitisha mkono wake kwenye mvi za kichwa chake zinazoongezeka kila kukicha. Mwanamama huyo nguli katika medani za usalama aliendelea kutuliza akili huku akitafakari nini hasa anapaswa kukifanya. Kwa upande wake, kupokea simu kutoka Ikulu maana yake ni aingie kazini katika hicho alichoambiwa.

Alipokuwa katika kutafakari hilo, mlango ulifunguliwa kwa pupa. Mtu aliyemtarajia aliingia, TSA 1, Kamanda Amata. Kijana jamali, shababi, akasimama akimtazama mama huyu aliyeonekana kuchanganyikiwa kiasi fulani.

"Madam!" akaita. Madam S badala ya kujibu salamu ile akamuonesha ishara ya kuketi kitini, naye akafanya hivyo.

"Kuna mambo yanayotokea kila kukicha katika serikali yetu, mi yananipa mashaka, kuanzia lile la msafara wa Rais miezi mitatu iliyopita… kuna vitu sijui tuite vituko au

tuiteje, sijui… vinanitia wasiwasi Kamanda," Madam alieleza huku akionekana wazi kuchoshwa na kazi.

"Ndio Madam, lipi tena limetokea hata uniite kwa haraka na ghafla namna hii?" kamanda akauliza. Mwanamama yule akainuka kitini na kuliendea jokofu lililomo ofisini humo. Aliporudi akaitua mezani chupa ya whisky, Couvosier, pombe ya Kifaransa. Bilauri moja akaijaza pomoni na kumsogezea kijana huyo.

"Kamanda!" akaita huku akiwa kasimama wima na kumatazama kijana huyo usoni. Amata akajua wazi kuwa sasa kuna jambo lisilo la kawaida, maana alikwishazoea Madam S akikwambia jambo huku amesimama mkitazamana basi ujue hilo ni zito kuliko maelezo na ulifanyie kazi kwa nguvu zote. Hiyo ndo ilikuwa aina yake ya kukutuma, hivyo Kamanda akatulia kwa heshima ya kikazi kumsikiliza bosi wake.

"Mheshimiwa waziri wa nishati na madini, wiki hii yupo katika ziara ya kutembelea migodi yote inayoendeshwa na serikali. Lakini jambo la kushangaza na kusikitisha limetokea, amefika katika mgodi wa almasi pale Mwadui asubuhi ya leo na kuchukua makasha matano ya almasi na kuondoka nayo akisema kuwa katumwa kutoka Ikulu. Ameonesha barua ya Ikulu iliyosainiwa na Rais na

kugongwa mhuri wa Ikulu," akatulia kidogo, akameza mate, kisha akaendelea, "Kamanda Amata naomba sasa hivi tunavyoongea uingie kazini, uanze uchunguzi wa kina wa kadhia hii na unipe majibu kila baada ya dakika sitini za uchunguzi wako. Sawa?"

*"Yes, Sir"* Amata akajibu kwa utani kama kawaida akikutana na Madam S.

"Ukihitajiu msaada wowote unajua la kufanya, haya ondoa mkia wako hapa!" TSA 1, akatulia kama sekunde tano hivi, akainua ile bilauri na kuipunga hewani, akapiga mafunda mawili tu na yote ikaishia tumboni, alipoitua, macho yake yakagongana na bosi wake. Akampigia saluti.

*Mtanikumbuka!* Madam S akajisemea moyoni huku akitabasamu.

Kamanda Amata akatoka na kuchukua gari lake, alipokuwa nyuma ya usukani, kwanza aliona afike nyumbani kwake, Kinondoni ili kuchukua zana zake za kazi zitakazomfaa kwa siku hizo. Kichwani mwake aliona wazi kuwa pa kuanzia auchunguzi wa tukio hilo ni Mwadui palepale. Akachukua simu iliyo ndani ya gari hilo na kumpigia Gina aliyemwacha ofisini kwake akiendelea na majukumu mengine ya uongo na kweli.

"TSA 1 kwenye simu…"

*"Nakupata bosi…"* Gina akajibu.

"Nitafutie chata ya kukodi, nina safari ya haraka kuelekea Mwadui mchana huu,"

*"Ok Sir!"* Gina alipojibu tu ile simu ikakatika. Mara tu alipowasili nyumbani kwake aliingia ndani na kuufunga mlango nyuma yake. Moja kwa moja akaelekea chumbani, hakukuwa na jipya zaidi ya kujiandaa. Akachagua silaha za kumfaa, akazipachika katika mkoba wake maalumu ambao hata ukipekuwa vipi huwezi kuziona kirahisi labda nawe uwe mbobevu katika medani hiyo. Akazipanga, zikapangika. Bastola mbili zilizojaa sawasawa zikawekwa kiunoni mwake, suti nadhifu ikafuata juu yake.

Alipomaliza kila kitu, akasimama mbele ya kioo, akajitazama. Waoh! Akaonekana mithili ya mfanyabiashara maarufu duniani.

*Kamwe hawatanijua kama ni jasusi mtata katika historia ya nchi*. Akajiwazia. Kisha akachukua kofia yake aina ya pama na kujitupia kichwani. Akainua mkoba wake na kutoka taratibu mpaka mlango mkubwa, akaminya nobu zake za siri na kuwasha mtambo wa usalama unaoruhusu kamera za siri kunasa picha zote ndani na nje ya nyumba yake. Kamera

hizo ni yeye peke yake anayezijua hata Gina ambaye mara nyingi hulala katika nyumba hiyo bado hakujua juu ya kamera hizo.

"Kamari wapi?" Scoba akamtupia swali wakati akiingia garini tayari kwa safari ya uwanja wa ndege.

"Mwadui *Cassino*, Shinyanga," kwa jibu hilo wote wakacheka na kugonganisha viganja vya mikono yao, kisha lile gari likaondolewa na kushika Barabara ya Kinondoni makaburini kuelekea ile ya Ally Hassan Mwinyi mpaka Bibi Titi na kumalizia ya Nyerere kupitia Mkurumah mpaka Uwanja wa ndege.

Gina alikuwa kasimama kando ya ua kubwa katika Uwanja wa ndege wa *Terminal One*. Alipoona gari la Scoba linaingia, akajitokeza na kuliendea, moja kwa moja alimwendea Kamanda Amata.

"Umependeza *dear!* Utafikiri unaenda harusini," Gina akamwambia Amata huku akimkumbatia na kumbusu.

"Yeah, ukipendeza namna hii kamwe adui zako hawatajua kama ni mtu wa hatari, watalegeza silaha zao na kukukaribisha kahawa," Kamanda akajibu huku akimtoa Gina kifuani mwake, akamtazama usoni, "Gina, nitahitaji msaada wako wa hali na mali."

“Sawa *Boss*! Nipo kwa ajili yako…”

Akatoka na kuiendea ndege ndogo iliyokuwa tayari kwa ajili yake kumfikisha Mwadui, akaingia na kuketi. Safari ikaanza.

* * *

Saa tisa mchana wa siku hiyo, Kamanda Amata aliwasili katika machimbo ya almasi ya Mwadui. Ndege ile ya kukodi iliyombeba, ilitua moja kwa moja kwenye uwanja uliojengwa pembezoni kidogo mwa mgodi huo. Kwa kuwa alikuwa peke yake, haikumchukua muda kuteremka na kuelekea jengo lenye ofisi za utawala. Pale akapokelewa na wafanyakazi na inspekta wa polisi aliyekuwa hapo akimsubiri baada ya kupewa taarifa ya ujio wake.

“Karibu Mwadui mkuu,” akamkaribisha.

“Asante sana afande,” Amata akaitikia karibisho lile na kupeana mikono na yule askari.

“Naitwa Inspekta Maranyingi, nipo hapa kwa ajili yako…” akajitambulisha. Kamanda akatabasamu na kutikisa kichwa chake, “Nilitegemea kukuta…” akamjibu. Wote wawili wakaongozana kuingia ndani ya jengo la utawala pamoja na wafanyakazi wachache wenye nyadhifa za juu

katika mgodi huo. Wakaketi kwenye ofisi ya Naomi ambaye wakati huo hakuwepo.

Mara tu baada ya kuketi, akawasabahi wale wengine na kuuvunja ukimya, “Kwanza poleni sana kwa matatizo,” akawaambia, nao wakaitikia kwa vichwa. Kisha Amata akaendelea, “Nimekuja kwa kazi maalum ya kukusanya taarifa kamili za tukio, naamini mengi mnayajua, kipi mnaweza kunambia, kuhusu kifo cha meneja na kuchukuliwa kwa almasi…” akauliza.

Wale viongozi wa mgodi wakakawa kimya kidogo. “Elezeni mnachokijua ili tupate ufumbuzi wa tukio hili,” Inspekta Maranyingi aliwatoa hofu. Mmoja wa wale viongozi akafungua kinywa chake na kueleza, “Tulipata ugeni wa mheshimiwa waziri wa Nisahati na Madini, pamoja naye alifuatana na vijana wa jeshi la polisi wawili waliovalia sare za jeshi hilo, walikuja kwa ndege ya Serikali…”

“Mnaweza kunambia hiyo ndege ilifika hapa saa ngapi?” Amata akauliza tena kwa kukatisha kile anachokieleza yule mtu.

“Ndege ilitua hapa kati ya saa tano na dakika ishirini na dakika arobaini hivi za asubuhi ya leo,” akaeleza msemaji wa ofisi hiyo.

"Sawa, na ninyi mlikuwa amkimtegemea waziri saa ngapi na kwa lipi?" Kamanda akatupa swali.

"Hatukutegemea ugeni wowote ule wa serikali hapa mgodini, na alipofika akatueleza kuwa ameagizwa na Rais kuchukua hizo kasha za almasi," akajibu. Kamanda Amata akatikisa kichwa na kuuliza tena maswali kadhaa, kisha akaomba kukiona chumba cha Dr. McLean. Akapelekwa. Kamanda Amata, hakuingia ndani, alisimama mlangoni, akakiangalia jinsi kilivyo. Hakikuvurugika, kilipangika vilevile. Chini, sakafuni karibu kabisa na mlango wa kuingilia ndani ya ofisi hiyo palitapakaa kahawa na vipande vya vipande vilivyovunjika. Kilichokosekana ni mhusika tu wa ofisi hiyo ambaye tayari muda huo alikuwa barafuni kwatika hospitali ya mkoa Shinyanga. Hakuvuta hatua nyingi, bali alisogea na kuketi kwenye kiti cha mgeni akikitazama kile cha Dr. McLean. Wakati huo alikuwa yeye na Inspekta Maranyingi pekee. Inspekta yule wa polisi hakuelewa nini anachokifanya kijana yule. Hakumuuliza kwa kuwa alishaambiwa na mchunguzi wa matukio tata aliyebobea. Amata akazungusha macho yake huku na kule, akasimama na kuzunguka upande wa pili, kichwani mwake alikuwa akijaribu kutengeneza mazingira ya jinsi gani mauaji yale yanaweza kuwa yametekelezwa. Akauendea mlango wa

choo, akaufungua na kutupa jicho ndani. Akaona haitoshi, akaingia na kujifungia.

*Inawezekana muuaji alijifungia humu kabla ya kutekeleza azma yake?* Akajiuliza. Hakukuwa na jipya zaidi ya sinki la choo, sehemu ya kuogea, magazeti na majarida yaliyowekwa katika mfuko maalumu uliobanwa nyuma ya mlango. Dakika mbili kama si tatu, akatoka. Ndani ya ofisi ile, akamkuta yule inspekta akimsubiri.

"Ok, sasa naomba nipeleke kwenye ofisi ya boharia," akamwambia. Pamoja na wale wafanyakazi wengine, wakaelekea huko atakako. Nako alifanya ukaguzi wa mtindo uleule. Ukaguzi wa kutazama tu pasi na kugusa kitu. Uwezo wa kufanya ukaguzi wa mtindo huu aliupata katika majiundo yake ya ujasusi. Aliweza kukariri mazingira kwa kuyatazama na kuiweka kumbukumbu kwa muda mrefu. Amata akawageukia wale watu, "Sawa, hakuna la zaidi, naomba niende lakini, ofisi hizo mbili zisiguswe na mtu yeyote mpaka mtakapopata taarifa nyingine". Akavuta hatua chache na kuuliza, "enhe mapokezi nani anahusika? …Nahitaji kuonana naye," akasema.

"Aaa huyu dada anasaidia polisi kwa sasa," akajibu yule nspekta.

"*Ok*, nahitaji kumuona," akasisitiza.

Kamanda Amata akatoka pamoja na yule inspekta wa polisi na vijana wawili kutoka jeshi hilo. Kwa kutumia gari la polisi hao walielekea kituo kikuu cha wilaya ambako huko alihifadhiwa katibu muhtasi wa ofisi ile. Saa kumi na moja ya jioni walifika katika kituo hicho na kukuta makundi ya watu waliokuwa pembeni mwa jengo hilo wakiongea hili na lile kama ilivyo kwa kituo chochote cha polisi. Miongoni mwao walikuwapo waliokuja kuwaona ndugu zao, wapo waliokuja kuwawekea dhamana ndugu zao, wapo waliokuwa kwa hili na lile lakini pia wapo waliokuja kujaribu kuvunja sheria ya nchi, kupenyeza rupia ili kesi za ndugu zao au zao wenyewe ziishe namna hiyo.

Amata akifuatana na yule inspekta, moja kwa moja walielekea katika moja ya ofisi za kituo hicho. Ofisi haikuwa na vitu vingi; meza moja iliyokuwa kati ya viti viwili vya chuma. Amata akakalia kiti kile ambacho kipo upande wa mlango, ambacho kwa vyovyote angetakiwa kukaa mgeni au mtuhumiwa kama inabidi wakati mwenyeji wake angekaa kwenye kile kinachoutazama mlango ili amuone mgeni wake au mtuhumiwa wake anapoingia. Mara mlango ukafunguliwa nyuma yake. akiwa anatazama simu yake ya kisasa, aliweza kuona yanayotukia mlangoni. Mwanadada aliye na nywele timu timu, alikuwa akiingizwa ndani ya chumba hicho akiwa

na pingu mkononi mwake huku akiongozwa na askari mmoja wa kike.

"Samahani mkuu, ungekaa upande ule ili huyu akae huku," yule askari wa kike akamwambia Amata.

"Asante, lakini kwa leo nampa upendeleo wa pekee, muweke aketi kule mimi nitaketi hapa," Kamanda akajibu. Yule askari akampeleka msichana yule katika kiti cha upande wa pili.

"Mfungue pingu, huyu sio mtuhumiwa," akatoa amri, "kisha utupishe kidogo," akaongeza. Baada ya pingu ile kufunguliwa, yule askari akatoka na kuwaacha wawili hao peke yao ofisini. Amata akamtazama yule binti na kumsaili kwa macho. Weupe wake ulikuwa wa kati, nywele ndefu ambazo kabla ya mkasa huo ilionekana zilikuwa katika mtindo mzuri sana. Macho yake yaliyokuwa yamelegea kidogo yalimfanya Amata kujua kuwa mwanadada huyu hutumia miwani kwa kuona na kusoma. Alimtazama kwa makini sana, akashusha macho yake taratibu, akasimama kifuani. Hakuwa na nia hiyo unayoifikiria, alimtazama kifuani kutaka kuona hali aliyonayo kama hofu au la. Kifua chake kilikuwa kikipanda na kushuka kwa hofu, yote hayo kijana huyu aliyang'amua kwa sekunde chache. Kwa jumla

alihisi kuwa msichana huyo hajaolewa kwani alikuwa na kila dalili za kuwa kapela.

"Naitwa Amata," akajitambulisha bila kificho mbele ya mrembo huyo. Ni nadra sana kujiweka jina lake wazi, kwa kuwa alijuwa kuwa wapo wanaomfahamu kwa jina na sifa zake bila kumjua wajihi wa mtu huyo. Aliuona mshtuko wa wazi kutoka kwa huyo binti aliye mbele yake. Naomi aligutuka na kuacha midomo wazi kiasi kama mtu aliyetokewa ghafla na kitu cha ajabu.

"Amata! Kamanda Amata?" akashangaa na kuuliza kwa sauti ndogo. Msichana huyo hakuamini kama mbele yake kakutana na mtu aliyekuwa akimsoma tu kwenye riwaya, hakuwahi kufikiri kama yupo kiumbe hai mwenye jina na sifa hizo. Hakuamini. Akatikisa kichwa na kukumbuka visa kadhaa vya kijasusi vilivyomhusisha kijana huyo kama mpelelezi namba moja katika kitengo cha siri cha serikali. Mtu anayetatua migogoro iliyofichwa kati ya siri nzito. Hakuwahi kujua kama mtu huyo yupo, lakini sasa alikuwa mbele yake. Naomi bado hakuamini.

"Naitwa Naomi," naye akajitambulisha kwa kitetemeshi.

"Usiogope Naomi. Nimekuja kukutoa na kukuacha huru kama mwanzo, lakini nataka kuongea na wewe mambo

kadhaa yaliyojiri pale ofisini kwenu leo asubuhi," akameza mate. Kwa kuanza alimtaka Naomi ajieleze juu ya maisha yake kwa kifupi, hapo Kamanda Amata alipata kujua kuwa Naomi ni binti wa kichaga, aliyezaliwa huko Lushoto mkoni Tanga katika hospitali ya Mlalo miaka kama ishirini na tatu iliyopita na kukulia huko ikiwa na kupata elimu ya msingi na kadhalika. Hakika Kamanda Amata hakuwa mbali na ukweli kwani alipomuona tu, muonekano wake ulijieleza, Mchaga wa Rombo.

"Niambie, juu ya kisa kilichotokea leo ofisini kwako," akamwomba, na Naomi akaeleza kila kitu kuanzia kufika kwa ule ugeni, walikuwa wangapi na yupi na yupi aliwajua. Kisha Kamnda akaanza kuuliza maswali ambayo kwayo labda yangempa mwanga katika kisa hicho tata.

"Mlikuwa mnategemea ugeni huo saa ngapi?"

"Hatukutegemea ugeni wowote siku hiyo,"

"Na ugeni huo wa ghafla ulipofika ulikuwa ukijua umekuja kufanya nini?" Amata akauliza.

"Hapana, mpaka nilipoambiwa na bosi wangu," akajibu na kubaki kimya. Macho yake yalionekana kutona machozi.

“Umesema kuwa ulimgundua McLean akiwa ameuawa ofisini mwake wakati ulipokuwa ukipeleka kahawa, je ulitegemea kukuta watu wangapi ndani ya ofisi hiyo?”

“Nilitegemea kumkuta peke yake,”

“Na ulipomkuta Mc Lean ameuawa, je ulimkuta mtu mwingine ofisini?”

“Hapana, alikuwa peke yake.”

“Na wageni hao walipotoka, uliwahesabu kama idadi yao imekamilika?”

Hapo Naomi akatulia kidogo, sekunde kadhaa zikapita, akashusha pumzi na kumeza mate, akajaribu kukumbuka jambo. “Hapana, sikuwa makini kutazama kama walikuwa idadi ileile.”

“*Ok*, kwa hiyo inawezekana muuaji alijificha nyuma ya mlango au kabatini?”

“Mh!” Naomi akaguna, “labda lakini sina uhakika kwa kuwa milango ile kwa jinsi imetengezwa haiwezi kukaa wazi, hivyo mtu hawezi kujificha nyuma yake...” Naomi akajitahidi kupambana na maswali ya kikachero yalityokuwa yakitafuta kitu.

"Sasa unafikiri alikuwa wapi, au alipita na wewe hukumuona?" lilikuwa ni swali lingine ambalo lilimpa shida Naomi.

"Hapana, hapana, hakutoka kabisa na ofisini hakuwepo," akajibu huku akipumua kwa nguvu.

"Je kuna mlango wowote wa siri kwenye ofisi ya Mc Lean ambao mtu anaweza kuutumia kutoka nje bila kujulikana?"

"Hapana! Sidhani kama kuna kitu kama hicho," akajibu.

"Basi hilo lilikua pepo, au we unasemaje?" kamanda akauliza tena lakini mara hii akitoa cheko la mbali kidogo, "ee maana kama si pepo basi wewe ndiye muuaji," kauli hii ya mwisho ilimchanganya Naomi, akajikuta akibaki na bumbuwazi. Amata hakumtazama usoni.

"Swali la mwisho," akatamka, na Naomi akamtazama kijana huyo usoni kidogo kisha akashusha macho yake chini.

"Unafikiri, waziri mwenye dhamana anaweza kuja na kuua bosi wako kisha vibaraka wake au yeye kuua mtu wa stoo, na kuchukua almasi ambazo ni mali ya serikali?"

"Hapana haiwezekani, ni majambazi tu hufanya hivyo…" Naomi akajibu.

“Kwa hiyo unataka kunambia ni nani aliyeweza kuja na ndege ya serikali na kufanya hujuma hiyo, majambazi? Au magaidi?” Kamanda akahoji. Naomi akatulia kimya, hakuwa na jibu, alibaki kumwemwesa tu.

“Naomi!” Kamanda akaita. Naomi akanyanyua uso wake na kumtazama usoni, machozi yalikuwa huku na huku, mashavu yake yaling’aa kwa chozi hilo lililotiririka juu yake. Uzuri wake uliojificha nyuma ya vipodozi vya kisasa ulidhihirika wazi. Amata akatabasamu, akahisi moyo wake ukipiga harakaharaka, ikawa zamu yake kutazama chini, kisha akamtazama tena msichana huyo.

“Una kesi ya kujibu mbele ya mahakama ya Tanzania…” akamwambia bila kupindisha maneno. Kama kutakuwa na lolote ninalolihitaji nitakutafuta, kwa sasa utaachiliwa huru, lakini, usizungumze na mtu yeyote juu ya hili, hata mpenzi wako usimwambie lolote, ukikiuka ujue ndio mwisho wako,” Amata akamaliza na kuinua simu ya mezani hapo akazungusha namba fulani kisha akaita mtu wa upande wa pili.

Askari yuleyule wa kike aliyemleta ndiye alikuja tena na ile pingu mkononi, nyuma yake akafuata yule inspekta.

“Naomba mfanye utaratibu wenu, huyu aachiwe huru, aendelee na shughuli zake lakini kila baada ya siku mbili aje

hapa kuripoti, na asipoonekana atafutwe mara moja mpaka utata huu ukipatiwa ufumbuzi. Hakikisheni macho yenu yanakuwa karibu na kila alipo ili asije akadhurika na watu watakaotaka kuharibu kesi hii," Amata akatoa maagizo, tayari akiwa wima. Baada ya hapo aliondoka zake kuelekea mjini.

# 1vi

ILIKUWA Saa kumi na mbili na dakika ishirini na tatu, Madam S alipogundua kuwa hajanyanyuka kutoka kitini kwake tangu alipoagana na kijana wake. Zilikuwa zimepita saa zaidi, hata hamu ya chakula hakuwa nayo, mawazo lukuki yalimtawala kichwani.

Simu ya mezani iliyoita kwa fujo ikamgutu kutoka katika lindi la mawazo, akainyakuwa na kuitega sikioni. Alishajua ni nani anayepiga, kwa maana simu ile hutumika kwa nadra sana na kwa kazi maalumu.

"Ndiyo Kamanda," akaitika na kumsikiliza mtu wa upande wa pili.

"Ndivyo tulivyofanya, tumesitisha kila aina ya uchunguzi mpaka tupate jibu kutoka kwako, lakini nakuomba usiku huu usiupitishe huko Shinyanga, akikisha unalala Dar es salaam, name ninakusubiri…" akamjibu na kumpa oda kama ilivyo desturi ya watu wa aina yake.

"Timamu!" Amata akajibu na kukata simu.

* * *

Usiku wa siku hiyo hiyo, majira ya saa nne hivi, Amata aliwasili kwa ndege nyingine ya kukodi. Uwanja wa ndege hapo alipokelewa na bosi wake, Madam S na Chiba. Kikao kifupi kikafanyika ndani ya gari lao.

"Karibu sana kamanda… ni hivi punde tu tumetoka kuonana na mkurugenzi wa idara ya mambo ya anga. Ameteleza mengi sana kuhusiana na ndege hiyo," madam akaeleza.

"Ni kweli kuwa waziri alisafiri leo?" akataka kujua.

"Twende hatua kwa hatua," Madam S akaeleza, "Ndege ya serikali iliondoka hapa saa moja kamili asubuhi, ikaelekea North Mara. Mujibu wa mtoa taarifa ni kuwa, ilifika kule saa mbili asubuhi na wakaondoka tena saa nne kuelekea Mwadui ambako saa tano na nusu walitua pale,"akaeleza. Amata akaoanisha nay ale majibu aliyoyapata pale Mwadui. Yanaendana.

"Sawa, anasemaje kuhusu ndege ile kutoka Mwadui, ikaenda wapi?" Amata akauliza kutaka kujua.

"Enhe hapo sasa kama hadithi ndo inaanza," madam akaeleza na kumpa ishara Chiba, "Ile ndege baada ya kuruka Mwadui, ilionekana kuelekea Kaskazini, na anasema

ikawapotea kwenye rada zikiwa zimebaki kilomita chache kufika mpakani na Uganda," akaeleza.

"Sawa, kwa hiyo na ndege imetekwa?" Amata akauliza.

"Hakuna anayejua. Utata uliopo hapa ni je huyo aliyekwenda ni waziri halisi au gojo?" Madam S akazungumza huku akiendelea kuandika vitu kadhaa katika kijidaftari chake cha kumbukumbu.

"Nina wazo moja" Amata akasema. Wote wawili wakamtazama, "twendeni kwa katibu wa wizara akatujuze kuhusu hiyo safari," akawaambia.

"Nasi tuliwaza hivyohivyo!" Chiba akajibu. Safari ya kuelekea nyumbani kwa katibu wa wizara ya nishati na madini ikaanza.

Masaki, Barabara ya Chole, Scoba alikunja kona na kufuata barabara ndogo ya Salama iingiayo kwenye nyumba za pembezoni. Nyumba ya tatu, akaegesha gari pembeni. Wote wakashuka na kuliendea lango la nyumba hiyo ya bei mbaya, mali ya serikali. Wakakaribishwa na mlinzi wa kimasai aliyekuwa akilinda mlangoni, haikuwa tabu kwao kuruhusiwa kuingia katika kasri hilo.

Waliyemhitaji walimkuta sebuleni akiwa kajipumzisha, huku mtoto wake akiwa pembeni anamsomea kitabu cha

*Paka na Juli*. Alipowaona wageni hao, akamwambia yule mtoto akalale na angemwita baadae.

"Karibuni sana, karibuni ndani, mnanitisha usiku wote huu kutembelewa na watu nisiowafahamu," akawakaribisha huku akiwapa mikono kwa zamu, kisha wote wakaketi. Yule bwana akashusha pumzi, "Ndio labda tufahamiane," aliongea akionekana kuwa na hofu.

"Sisi ni watu wa Idara ya Usalama," Madam S alitambulisha kwa ujumla wao, "samahani kwa kukuvamia usiku huu, lakini kwetu ulikuwa ni muda muafaka sana kuonana nawe. Najua mpaka hapo umefahamu nini tunataka kuzungumza nawe," akaongeza kusema.

"Mmmh! Ndiyo, nawasikiliza wakuu, lakini kabla hatujaendelea na mazungumzo, ningependa kuona vitambulisho vyenu, maana wavamizi ni wengi" akawaomba. Kila mmoja akatoa kitambulisho na kumuonesha, akajiridhisha navyo kwani alivijua vitambulisho vyao vinavyokuwa. Hivyo kungekuwa na kughushi kwa aina yoyote ile angetambua pia, lakini majina yaliooneshwa na vitengo vilivyoainishwa katika  vitambulisho hivyo vilikuwa uongo tupu.

"Tuna jambo moja tu tunalotaka kujua," Madam akaanzisha mazungumzo.

“Enhe…”

“Kama ujuavyo tukio lililotokea leo asubuhi huko Mwadui, tunapenda kujua ni nani na nani walifuatan nae?” Madam S akahoji.

“Ulikuwa ni msafara wa watu kumi na tano; wabunge saba wa kamati ya madini, waziri kivuli wa wizara hiyo. Pamoja nao walikuwapo wageni wanne kutoka mataifa ya Canada na Uingereza zaidi ya hapo ni watendaji wa wizara akiwamo katibu muhtasi wa waziri mwenyewe, na waziri,” akajibu kwa ufasaha.

Kwa jibu hilo akili ya Amata, ikafanya kazi harakaharaka “Unafahamu lolote juu ya mpango wa wizi wa almasi uliofanyika leo?”akamuuliza,

“Mpango kama mpango …kiukweli siujui, labda kama mheshimiwa alikuwa na mpango binafsi katika hilo, lakini mimi hakuna ninachojua kabisa,” akajibu.

“Ok, naomba kupata taarifa kamili za watu wote waliokuwa ndegeni, kuanzia walikozaliwa, wanakoishi na wanafanya nini, napenda kupata usiku huu, nikiwa na maana ama twende ofisini kwako sasa au unipatie kwa njia yoyote lakini usiku huu. Kwa sababu kama ujuavyo, kumetokea wizi wa almasi, upotevu wa ndege ya serikali na watu wote

waliopo ndani yake," Kamanda akamaliza na kujiegemeza kitini, Madam S akatikisa kichwa juu chini kuashiria kuwa karidhika na hilo lililosemwa.

"Taarifa zao zote ninazo kwa sababu pia ni wajibu kuzihifadhi kwa dharula yoyote kwa mfano kama hii, niko tayari kuwapa ushirikiano wowote mtakao," akajibu huku akinyanyuka na kuchukua fulana yake iliyokuwa kitini, akaivaa. akaichukua saa yake na kujiandaa kuipachika mkononi mwake. Lakini kabla hajaiweka mkononi, sauti ya Amata ikamshtua.

"Samahani, saa yako ni nzuri sana naweza kuiona?" akaomba.

"Bila shaka," akampatia.

Kamanda Amata, akaitazama kidadisi sana saa ile kwa kuigeuza geuza huku na huko.

"Umeipenda?" akauliza

"Kwa kweli ni saa ya gharama sana kati ya saa za gharama…" Kamanda akajibu huku macho yake bado yakiitalii.

Wakati bado akiishangaa ile saa, mwenyeji wao akatoka pale sebuleni na kuelekea chumbani akiwataka kumsubiri

kwa dakika kadhaa. Ni nafasi hiyo ambayo Chiba, mtaalamu wa mawasiliano na teknolojia ya kompyuta katika Idara ya Kijasusi ya Tanzania, alipomnyang'anya ile saa Amata. Kwa haraka akaifungua pini yake ya pembeni. Akaichomoa na kuichomeka kwa chini kwenye tundu dogo sana lililo katikati ya mfuniko. Mfuniko wake ukaachia upande mmoja, akabana kitu fulani kwa ncha za kidole chake na kukivuta, kisha akairudishia kama ilivyokuwa na muda huohuo mwenyeji wao alikuwa akifika sebuleni. Akampa saa yake huku akimwuliza, "mzee uko juu, hii saa uliipata duka gani?"

"Aaa nimepewa zawadi na hawa wageni Wacanada walioenda Mwadui, tulipokutana kule Ontario kwenye mkutano wa nchi zinazoongoza kwa uchimbaji wa madini duniani na ya kwetu ilikuwa mojawapo. Ni saa nzuri sana kiukweli," alijibu huku wakiwa wanatoka.

Usiku huo ndani ya ofisi ya katibu huyo, TSA walipata taarifa za wote waliokuwa na waziri. ndegeni. Walipoona zinatosha, wakaondoka na mwenyeji wao na kumsindikiza mpaka nyumbani kwake kisha wao wakageuza gari na kurudi. Wakiwa ndani ya gari lao huku Scoba akiedelea kuwapeleka wanakokutaka, ukimya ulitawala ulijidai kati yao, kila mmoja mawazo yake yalipaa huku na kule.

"Mnajua!" Chiba aliwagutusha. Wote wakamtazama isipokuwa Scoba, ambaye macho yake yalikuwa barabarani. Akajikohoza kidogo. "Ile saa ile, ina kifaa cha kunasa mawasiliano ya watu, hivi tulivyokuwa tunaongea pale, kuna watu wamenasa yote tuliyokuwa tukiyazungumza," Chiba akawaeleza, Madam S akashtuka kidogo na kukodoa macho.

"Unajua Chiba, mi ile saa niliistukia mapema kwa sababu, katika kioo pale juu katikati ya mishale kuna kajitaa kekundu kanawaka na kuzima na wakati tunaongea kakawa kanawaka harakaharaka. Lakini kwa macho tupu huwezi kukaona kirahisi kutokana na rangi yake …ndiyo maana niliposhtukia ile saa nikatoa miwani yangu ambayo wengi hujua ya kusomea na kuivaa ndipo nilipouona ule mwanga kiurahisi zaidi," Amata akawaeleza.

"Ndiyo, ulipoichukua, mimi nilishajua ni saa ya mtindo gani, ndio maana nikakunyang'anya nikijua nini nadhamiria kufanya na nikafanikiwa. Nimeondoa chip ambayo inanasa na kutuma mawasiliano kwa wahusika lakini pia nimeondoa kadi sakima iliyopachikwa ndani yake. Kwa kuwa bila ile kadi kinasa sauti chake hakiwezi kufanya kazi. Sasa tutaujua ukweli ulivyo, tusikilize mazungumzo yote tangu mwanzo tukiwa na muda," Chiba alieleza.

Muda huohuo, simu iliyofungwa ndani ya gari ikakoroma kuashiria kuna taarifa inataka kuingia, Madam akampa ishara Scoba airuhusu. Kutoka katika ile simu ikasikika sauti ya mtu kama anayeongea kutoka mbali, mara moja walitambua ni mtaalamu wa mambo ya anga kutoka JWTZ ambako rada kubwa kabisa Afrika yenye uwezo wa kuona ndege yoyote inayoingia katika mpaka wa Afrika alikuwa akiongea. Madam S akaongeza sauti kidogo ili wote wasikie vyema.

> *(…) kwa vipimo vyetu vya chombo cha kunasa muelekeo wa ndege, ndege aina ya Foker Friendship, iliyoruka Mwadui saa tano na dakika hamsini na moja ilielekea Kaskazini Mashariki, lakini baada ya dakika arobaini, ndege hiyo ilishuka chini sana kitaalamu tunaita 'low attitude' hapo haikuonekana tena, sasa hatujui kama imeanguka au imetua mahali tumeuliza watu wa TAA…*

Ilimalizika taarifa ile.

Kamanda Amata akashusha pumzi, na kuwatazama wenzake, kisha akainua mkono na kuitazama saa yake. Ilikuwa saa sita za usiku.

"HOT," akaita.

"Sema!" Madam akajibu. Wakatzamana.

“Naanza kupata wasiwasi, hapa hatujui nani hasa tunayemchunguza, au nini tunachokitafuta, nafikiri sasa tuanze kufanya chunguzi sambamba maana muda unaisha *madam*. Kama inawezekana, hiyo ndege itafutwe kuanzia usiku huu kwa nguvu zote za angani, ardhini na majini, wakati sisi tunasaka watuhumiwa na usalama wa watu wetu, maana mwizi wetu anazidi kusonga mbele, tutamkosa,” akaongea kwa hisia kali. Chiba akaunga mkono kwa kutikisa kichwa.

“*Ok!* Naungana nanyi nyote, sasa naomba tuonane ofisi ndogo haraka usiku huu, mwite Jasmini na Gina ndani ya dakika kumi,” Madam akatoa uamuzi. Kamanda Amata alimtazama mwanamama huyu ambaye daima aliamini vijana wake. Hakupuuza hata siku moja mpango au hoja inayotolewa na mmoja wa vijana wake hasa katika kazi zao.

Kamanda Amata alimpenda sana mwanamama huyu hasa kwa umakini wake wa kazi, na maamuzi yenye majibu chanya siku zote. Hakuwa mtu wa dharau bali alithamini hata tone la mvua lidondokalo kutoka juu. Alikuwa mwanamke wa chuma, aliyepitia mihangaiko, majanga, na mateso mengi katika kazi yake hiyo. Mtu mzima, taratibu, weusi wa nywele zake ulikuwa ukimezwa na weupe. Lakini ukali na umakini wa macho yake bado uling’aa daima.

Alikuwa na kipaji cha kujua unalotaka kusema kabla hujafungua kinywa chako. Alikuwa na *IQ* ya hali ya juu sana, aliaminiwa sana kwa usiri wa mambo na ndiyo ilikuwa nidhamu ya kazi yao. Kiapo chake kilimfanya awe tayari hata umkate kichwa lakini hawezi kukwambia chochote ambacho hupaswi kukijua.

Idara ya siri ya ujasusi ilipoanzishwa katika utawala wa awamu ya kwanza hasa wakati wa lile sakata la kutaka kuipindua serikali hiyo, ukiachana na mwanausalama namba moja aliyekuwa akifanya kazi kwa siri sana na Mwalimu Nyerere, Mzee Chameleone. Hakuonekana mtu aliyefaa kuiongoza zaidi ya mwanamke huyu, na mpaka sasa ilikuwa vigumu kwake kustahafu kwa jinsi alivyoaminiwa.

Ni idara ya siri sana ambayo kazi zake hufanywa kimya kimya lakini kwa umakini wa hali ya juu sana. Kila aliyefanya kazi katika idara hii alikuwa na utambulisho wake mbele ya jamii, tofauti na kazi yenyewe, hivyo ilikuwa ngumu kutambulika kiurahisi, isipokuwa na watu wachache hasa wale walioko katika nafasi zinazofanya wakutane mara kwa mara. Mwanamke huyu alikwishaachishwa kazi katika ofisi yake ya awali ya usalama wa taifa, na inajulikana hivyo. Lakini kumbe alihamishwa ofisi kwa siri na sasa alijulikana

kama msatahafu isipokuwa tu huitwa kwa shughuli maalum ikibidi kuwa wazi.

Ukiachana na yeye, vijana wake wote walikuwa na shughuli mbalimbali za kufanya zinzowakutanisha na jamii kila siku. Chiba, yeye alikuwa ni mhadhiri msaidizi katika idara ya TEHAMA pale chuo kikuu cha Dar es salaam, wakati Kamanda Amata alikuwa akimiliki ofisi ya kufaulisha mizigo ya *AGI Investiment* akiwa na Gina kama mtu wa mapokezi ofisini hapo. Daktari Jasmini daima alipatikana Muhimbili kama daktari bingwa mpasuaji lakini pia alimiliki kliniki yake binafsi iliyojulikana kama Jabal Al - Hiraa. Scoba, kama anavyojulikana alikuwa ni dereva Taksi na wengi walimjua kwa hilo. Taksi yake aina ya Toyota Carina iliyochoka kidogo, ilikuwa ikiegeshwa karibu kabisa na jengo la wizara ya Elimu ambao ni mitaa miwili tu unafika ofisi ya Madam S. Ofisi maalum ya kusaidia wazee hasa wale wanaofuatilia madai yao ya mafao ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Usiku wa saa sita na dakika arobaini na sita, jopo zima la TSA walikuwa wamewasili katika ofisi ndogo, ofisi ya Madam S. kila mmoja alikuwa katingwa kutupa macho kwenye karatasi iliyo mbele yake. Madam S akavunja

ukimya, “Kiukweli hii ni kali ya mwaka, tangu nimeanza kazi hii sijawahi kupambana na janga kama hili,” akawaambia.

“Ee… maana wengine huwa wanaiba mapesa kiufisadi lakini huyu safari hii kaamua kuchukua almasi kabisa na ndege ya serikali,” akadakia Dr. Jasmin.

“Katumiwa na mabeberu kwa vyovyote vile! Hakuna mtu mwenye ujasiri kama huo endapo hakuna nguvu kubwa nyuma yake… tena Bongo!” Scoba akatia shaka.

“Ok, sasa tupo hapa kwa ajili ya kupanga mpango kazi, lazima hii kesi kesho asubuhi kwenye saa nne hivi tuwe tumepata mwanga fulani maana kutakuwa na kikao kinacholihusu hili saa tano ya asubuhi,” Madam S akawaambia vijana wake. Nao walikuwa kimya kusikiliza. Hawakutakiwa kuandika popote ila walitakiwa kila kinachoongelewa kikae kichwani kwa kuwa ni siri, “Chiba!” akaita.

“Kuna nini kwenye hiyo kadi?” akamwuliza.

“Bado, nilikuwa nahangaika nayo hapa. Inaonekana imefungwa kwa namba ambazo mpaka nijue mchanganyo wake, ni kazi kubwa kidogo mama, lakini kabla ya hiyo saa nne kesho nakuhakikishia nitakuwa nimetegua kitendawili

hata ikibidi niende nje ya dunia kwa kazi hii nitakwenda," akajibu na wote wakacheka hasa kwa sentensi ya mwisho.

"Mpaka muda huo Madam, tutakuwa tumepata ufumbuzi," Kamanda akapigilia msumali.

"Ok, sasa nataka tufanye kazi katika mtindo wa pembetatu, siku zote mfumo wa pembetatu huwa unaleta mafanikio haraka sana, ndiyo maana hata shetani anatumia pembetatu katika utawala wake" Madam akawaambia. Wote wakatingisha vishwa juu-chini kuashiria wako pamoja na mkuu wao, "Mkuu wa nchi kachanganyikiwa, haelewi kipi ni kipi… na hapa ni sisi tu tunaotegemewa. Mkae mkijua, jeshi la polisi na wapelelezi wao, nao wanafanya kazi juu ya hili, ila sisi tupo mbele zaidi, sasa nimefikiria tufanye hivi; Chiba na Amata mtakuwa shamba hakikisheni mnafungua hiyo *chip* na pia mnachambua taarifa zote za hao watu tuliopewa majina yao na katibu. Hakikisheni mnajua mpaka saa ngapi huwa wanaenda haja… Hiyo ni pembe ya kwanza. Gina na Jasmini mtaondoka hapa usiku huu kwenda Shinyanga. Huko mna machache ya kufanya; moja, nataka Dkt. Jasmini ukafanyie uchunguzi maiti ya Mc Lean na boharia wake. Ujue silaha iliyotumika kuwaua ili tufananishe na silaha anayomiliki mheshimiwa ili tuanze kuoanisha mambo. Muda unakimbia, tatu, Gina, kazi yako ni kuhakikisha usalama wa

Jasmin, kunusa kila hatari inayozunguka na kuishughulikia, ukihitaji msaada unanitaarifu mara moja. Sawa?"

"Sawa!" Gina na Jasmin wakajikuta wakijibu pamoja.

"Hiyo ni pembe ya pili… Scoba utakuwa bega kwa bega na marubani wa jeshi ambao wanakusubiri muondoke, mkaitafute hiyo ndege pande hizo za Mwanza mpaka Uganda, wakati huo meli ya jeshi kikosi cha maji pale Mwanza nayo itakuwa kwenye doria, upo kaka?"

"Nipo!"

"Hiyo ni pembe ya tatu. Nafikiri tumeelewana," akawatazama kwa tuo, wote walikuwa kimya. "Kuna swali?"

Ukimya ule ukatawala kati ya wote. Majukumu waliyopewa yalikuwa yanajieleza kabisa, hakuna ambaye hakuelewa kilichosemwa na mwanamama huyo. Kila mtu akajipapasa kiunoni mwake, na kujikuta yupo vizuri, bastola na zagazaga nyingine zilikuwa kamili. Gina alikuwa bado kamtumbulia macho Madam S.

"Gina, mbona unashangaa?" kamanda akauliza.

"Kazi niliyopewa, du! Mi nilijuwa ama Kamanda awe na mimi au awe na Dr. Jasmini, sasa wanawake tupu

tutafanikiwa kweli endapo kutatokea *ambush*?" Gina akauliza kwa shaka.

"Gina, ingekuwa mwanamke hawezi kitu, Ikulu isingenipa hiki kitengo nyeti, na mimi ninsingekuteua wewe kukupa beji ya TSA 5. Kumbuka wewe na Amata mna taaluma moja, na taaluma yenu inatakiwa kila upande. Sijataka ubaki hapa, nimetaka uende Shinyanga nina maana yangu. Huo ni mtihani wako wa kwanza, mi nazeeka, nikistahafu au nikifa hii nafasi haina mtu zaidi ya Kamanda Amata je nani atashika kitengo chake kama si wewe? Nimemaliza, wote mtawanyike." Madam S akamaliza kupanga kazi kwa vijana wake. Hakuwa na mashaka, kwani hawakuwahi kumuangusha katika lolote lile. Kama Ikulu ilivyomwamini yeye na yeye aliwaamini watu wake.

Usiku huo kila mtu aliondoka na kuingia katika jukumu alilopewa, Gina na Jasmini walifuatana mpaka uwanja wa ndege ambapo walikuta ndege ya kukodi ikiwa tayari kuelekea Shinyanga. Scoba, naye aliingia uwanja wa ndege wa Jeshi *'Air wing'* wa kikosi namba 603. Kamanda Amata, Chiba na Madam S walielekea Shamba. Kazi ilipangwa, ikapangika.

* * *

Helkopta ya Jeshi  ilikatisha anga la Jiji la Mwanza usiku wa manane kuelekea ziwani. Safari hiyo ilikuwa maalum ya msako wa kuitafuta ndege iliyopotea mchana wa siku iliyopita baada ya kutumiwa katika wizi wa almasi.

Chopa hilo laa jeshi likiwa angani, chini, katika Ziwa Victoria kulikuwa na meli ya jeshi nayo ikiwa katika operesheni hiyohiyo. Wao katika meli hiyo walikuwa wakitumia vyombo mbalimbali kutazama kama wanaweza kuona chochote kinachohusiana na ndge hiyo. Mawasiliano kati ya wale waliokuwa katika ndege na hawa walioko melini yaliunganishwa moja kwa moja na wale walio katika rada ya jeshi kule Ngelengele mkoani Morogoro.

Wakiwa juu, Scoba na yule kepteni wa jeshi waliweza kuona kitu kisichoeleweka, kilichokuwa kiking'azwa kwa mbwalamwezi. Umbo la kitu hicho ndilo lililowafanya kukisshuku. Wakatoa taarifa haraka na kupewa maelekezo kuwa wateremshe chopa hilo chini Zaidi lakini kwa tahaadhari kubwa. Wakatii na kuteremsha ile chopa kama walivyoelekezwa. Hakika mtu aliyewaelekeza hakukosea hata kidogo.

"Kuna kitu tunachokiona katikati ya msitu, tuna wasiwasi nacho kama ni ndege kutokana na kinavyong'aa kwa mbalamwezi, ova!" Scoba alitoa taarifa.

“TH1…nenda chini zaidi ili uone kwa ufasaha, ova!”

*“Roja! Roja!”*

“TH1 …Kama kuna uwezekano wa kutua basi tueni kabisa, ova!”

Ile chopa ilipita karibu kabisa na kuhakikisha ni ndege iliyotua katika barabara ya vumbi iliyo finyu sana.

“Sierra, Sierra… tulichokiona ni *positive*! Ova!” wakatoa taarifa kuwa walicchoona ni sahihi yaani ni ndege wanayoitafuta. Wakageuza chombo chao na kurudi Mwanza tayari kwa kazi nyingine.

Taarifa zilifika mara moja kwa Madam S, kwani ndani ya jumba lao huko Gezaulole, Shamba, waliweza kunasa mawasiliano yote yaliyokuwa baina ya ile chopa ya jeshi, meli na mtaalam wa anga alikyekuwa huko Ngelengele. Alikurupuka kitandani ambapo aalijilaza akifuatilia mawasiliano hayo kwa chombo maalum, na kuwafata Amata na Chiba waliokuwa katika chumba kingine cha mawasiliano na kuwapa taarifa. Ilikuwa ni furaha kwa wote.

* * *

“Ehne, na ninyi mmefikia wapi katika uchunguzi wenu?” Madam alimwuliza Amata.

“Aaaah, majibu sio mabaya, hawa Watanzania waliofuatana na waziri taarifa zao hazina mashaka sana, ila hawa Wazungu wanne ndio bado ninachimba zaidi,” Kamanda alijibu.

“Mpaka ulipofikia…” Madama alisema

“Mpaka nilipofikia?” Amata akauliza kana kwamba hajasikia vizuri.

“Ndiyo…”

“Kuna huyu Bwana Mark Steuben, tajiri mkubwa sana huko Uingereza, anafanya biashara ya madini na mataifa mbalimbali duniani, ana kampuni kubwa iitwayo *Cunglia Gold Mines*, ambayo ofisi zake zipo katika mji mdogo wa Cunglia, katikati ya Uingereza. Labda anaweza kumshawishi mtu yeyote kufanya wizi kama ule kwa kumpa pesa nyingi sana.” Kamanda akajibu.

“Ok,” Madam S akaitikia huku akitikisa kichwa chake.

“Halafu kuna huyu Bwana Dregen. Amewakilisha kampuni moja ya kuuza madini iliyoko huko Canada katika jiji la Ontario, nimejaribu kuingia kwa undani zaidi wa yeye na kampuni yenyewe, yaani *Robinson Dia-Gold LTD*. Kampuni hii ipo Ontario, na inamilikiwa na tajiri mkubwa

wa huko Canada anaitwa Bwana Robinson Quebec," akamlizia hapo.

"*Very Good* Kamanda, umeona hao wote wana makampuni ya madini kwa hiyo kuna uwezekano wa kushawishi wizi huo au kufanya wizi huo, yote yanawezekana… endelea kuchambua zaidi, anagalia na wigo wa marafiki zao kibiashara duniani kote na Afrika ili tuone kama kuna muungano na popote panapoweza kutupa jibu," Madam alitoa maelekezo. Amata akamuonesha alama ya dole gumba.

"Chiba nipe ripoti," akamgeukia Chiba aliyekuwa ametingwa na kompyuta zake.

"Nimefanikiwa kuivunja nywila waliyotumia, ila kazi ilikuwa ngumu sana. Hakuna cha maana sana isipokuwa *chip* hii ilikuwa inahifadhi kumbukumbu kwa njia ya sauti kutoka upande wa huyu katibu na kuzituma kwa hawa jamaa. Sasa hapa ninachotaka kufanya ili tujue ilikuwa inapeleka wapi hasa, na nani alikuwa anazipokea, inabidi tuiunganishe tena, halafu ndio nijaribu kuona *codes* zake zinavyooana hapo tutajua upande gani na wapi inatuma taarifa, itakuwa rahisi kumpata mtu wetu au watu wetu," Chiba alieleza kinagaubaga.

"*Ok,* kama vipi fanya hivyo asubuhi, sijui utaipataje ile saa ya yule mzee na muda wote iko mkononi," Madam S alionesha mashaka.

"Usijali, mimi ndio Chiba, huwa sishindwi kitu, nitaiunganisha hapahapa kwa kutumia vifaa vyangu na ninauhakika itafanya kazi."

*"All the best,"* madam alimaliza na kutoka.

* * *

Daktari Jasmin alimaliza kazi yake, ile miili ikarudishwa mahala pake. Akavua nguo alizokuwa amevaa na kuziweka vizuri kwenye mfuko wa plastiki, kisha kwenye mkoba wake. Akatoka akifuatana na yule mhudumu wa chumba cha maiti. Nje walimkuta Gina akiwa anazungukazunguka huku na huko, akampaigia mruzi. Gina karudi mara moja.

"Asante sana," akamshukuru yule kijana na kumpa noti ya Shilingi elfu kumi za Kitanzania.

"Vipi, kuna lolote?" akamwuliza Gina.

"Nina wasiwasi, kuna gari limepita hapa kama mara mbili, limezunguko huku, ndio nilikuwa nalitazama nijue lina shughuli gani," Gina akamjibu. "Vipi, nawe umepata lolote?" Gina akamwuliza.

“Yeah, nimepata majibu yenye utata kabisa, lakini hata hivyo…” akasita kidogo, akampa Ishara Gina ya kutazama kwenye ua kubwa lililofanya kichaka cha kuogofya. Gina akageuka kwa chati na kuona kivuli cha mtu aliyetulia kama mti mkavu sambamba na mti wenyewe, akajiweka tayari kiakili na kimwili. “Tutaongea baadae,” Jasmini akamwambia Gina huku wakiharakisha kulifuata lango la hospitali hiyo.

Hakukuwa na mtu kwenye vijia vya hospitali hiyo, isipokuwa wauguzi na madaktari waliokuwa wakipishana usiku huo kwa kazi mbalimbali. Gina alitazama nyuma na kuona watu wawili waliokuwa wakiwafuata taratibu ambao waliachana kama mita mbili katikati yao. Mbele yao kulikuwa na mtu mwingine aliyevalia kidaktari. Akili ya Gina ikafanya kazi kwa haraka zaidi, mwili wake ukasisimka, akaiona hatari hiyo, akamgonga Jasmini kwa kiwiko.

*Kumekucha!* Akawaza. “Una bastola?” akamwuliza Jasmini.

“Ndiyo!”

“Iweke tayari, funga kiwambo kwa siri, pale mbele kuna korido mbili wewe nenda kushoto mimi niende kulia tuone watagawanyika vipi kisha tuwashambulie. Hakuna kubakisha kitu, muda mbaya huu,” Gina alimwambia Jasmini ambaye

aliitikia kwa kichwa. Jasmini akatoa bastola yake kwa chati ndani ya mkoba wake huku mkono ukifunikwa na koti lake la kidaktari. Alipoishika sawia, akaliweka juu koti lake la kidaktari hivyo hakuna aliyeona kama ana bastola mkononi mwake. Wale watu bado walikuwa wakiwafuata kwa nyuma.

Walipoifikia ile pacha ya korido ambapo mbili zilikutana na kufanya alama ya jumlisha. Jasmini akaelekea kushoto na Gina kulia. Kila mmoja akashika njia yake. Wale watu wawili walipofika pale, nao wakagawana njia mmoja kushoto na mwingine kulia. Gina aliona tukio zima, alipofika mbele kidogo akasimama akijifanya anaweka kiatu chake vizuri. Yule mtu aliyekuja upande wa Gina akamkaribia huku mkono wake ukijishika kiunoni. Alikuwa akitoa bastola, amechelewa. Gina alirusha teke moja kali upande wa nyuma na kiatu alichovaa chenye kisigino kirefu kikamtoboa tumboni. Gina akarudi wima. Wakati yule mtu akijishika tumbo, tayari Gina alikuwa hewani akamtandika mateke mawili yaliyompeleka chini. Yule jamaa akajiinua haraka ili akabiliane na mwanamke huyo. Gina aliona upande wa Jasimine, yule aliyevaa kidaktari akigeuka tayari na bastola mkononi tayari kumlipua.

Gina kwa haraka, akamkamata adui yake na kumuweka kati kisha kwa haraka akajirusha upande wa pili na ile risasi

ikamfumua vibaya yule mtu na kumtupa chini kama mzigo. Jasmini, akasimama haraka, na yule kijana akamwekea bastola mgongoni.

"Tembea hivyohivyo… ongoza mpaka garini," akamwamuru. Jasmini hakuonesha upinzani, akatembea. Haukuwa mwendo mrefu, kadiri ya hatua tatu tu ndipo aliposikia mlio hafifu wa bastola inayoondolewa usalama ya yule aliye nyuma yake, akatumia nafasi hiyohiyo. Akageuka ghafla na kuupiga mkono wa yule kijana kwa mkoba wake, bastola ikaanguka chini. Yule jamaa akajitupa chini kuiokota. Ile bastola ikapigwa teke na kwenda upande wa pili. Jasmini alitumia miguu yake kumshambulia yule kijana aliyekuwa bado chini. Mateke yale yaliyokuwa yakimpata usoni na sehemu nyeti za mwili yakamvuruga kabisa. Yule mwingine aliyevaa kidaktari alikuwa na bastola mkononi akimjia Jasmini kwa mwendo wa kukimbia na kutembea. Jasmini alimwona na kupiga hesabu za nini afanye. Bastola iliyo mkononi mwa yule kijana, ikaondolewa usalama. Mara ghafla, yule jamaa akatupwa upande mwingine, kichwa chake kikiwa kimefumuliwa kwa risasi. Gina akawahi pale alipo Jasmini. Akamkanyaga shingoni yule jamaa aliyekuwa akigalagala chini.

"Sema! Nani kawatuma?" Gina akauliza huku bastola yake ikisubiri amri tu.

"Si- si-mjui…" akajibu kwa kigugumizi huku macho yamemtoka, kinywa chake kilijaa damu.

"Sitaki kunipotezea muda… sema, ama nakuua," Gina akang'aka huku midomo ikimtetemeka. Alipoona ukaidi unazidi, akaruhusu risasi moja tu iliyotawanya goti la yule jamaa.

"Aaaaaa, aaaaaa unaniua mimi! Iiiiiii, mama weeee, ona sasa, damu zinatoka," yule mtu alilia kama mtoto.

"Wacha zitoke, utasema au husemi?" Gina aliuliza tena.

"Nasema, nasema, usiniue tena… aaaiiiii,"

"Haya nambie…"

"Tumetumwa na Don Swa…" kabla hajamaliza kusema alitoa macho kama mjusi aliyebanwa na mlango.

"Tunashambuliwaaa!" Jasmini akapiga kelele. Gina akamwachia yule mtu na kuruka kinyumenyume akatua kwenye pipa la taka, akaanguka nalo. Ilikuwa bahati yake tu kwani risasi kadhaa zilitua mahali pale. Kama isingekuwa lile pipa basi tungeongea mengine. Jasmini akachukua bastola yake na kupiga risasi ovyo ili kuwapoteza wale watu huku

akimpa nafasi Gina kuinuka. Alipofanikiwa kuinuka tu, akamkamata mkono Jasmini na kutokomea.

"Wazingile! Wazingile," sauti ilisikika.

"Watatokea huku, we pita kule," mwingine aliamuru.

"Kwani kuna nini jamani?" Muuguzi mmoja aliuliza baada ya kuona watu asiowajua wakiingia wodini mwake na bunduki mikononi mwao.

"Kuna majambazi wawili wa kike tunawasaka, sisi ni polisi, mmewaona wameelekea wapi?" akauliza mmoja wao.

"Wamepita pale kwenye hako kamlango kadogo," mgonjwa mmoja akaropoka na wengine wakashadadia.

* * *

Gina na Jasmini, wakatulia tuli ndani ya chumba cha kubadilishia nguo wauguzi. Yule mtu aliyepewa maelekezo, akatembea kwa hadhari kubwa kuingia katika kile chumba, akasukuma mlango kwa mtutu wa SMG aliyoidhibiti vema mikononi mwake. Ukimya ukamlaki. Zaidi ya ukimya huo ni nguo tu zilizokuwa zikining'inia. Sekunde chache tu akasikia viatu vya mtu anayetembea kuelekea mlangoni pale alipo yule askari aliyeva kiraia. Dkt. Jasmini akatoka akiwa amevaa vazi lake la kidaktari, *stethoscope* yake shingoni, mikono

mfukoni. Alipoukaribia mlango akakutana uso kwa uso na mtutu wa bunduki.

"We vipi huku na libunduki lako?" akamwuuliza.

"Tunatafuta majambazi wawili wa kike," yule bwana akajieleza.

"Sasa majambazi ndio wakimbilie wodini, si watakamatwa tu, hakuna mtu huko," Dkt. Jasmini akajibu, huku akipishana na yule mtu kuelekea ndani ya ile wodi.

"Hawapo, twendeni nje!" yule askari akawaambia wenzake, na wote wakatoka ndani ya ile wodi.

Hali ilipokuwa shwari katika viunga vile vya hospitali, Dkt Jasmini akaenda kumtoa Gina mle chumbani na kuelekea yaliko maegesho. Pale kulikuwa na magari mengi ya serikali na miradi tofauti. Wakaliendea mojawapo, bahati nzuri dereva alikuwa ndani, amesinzia.

"Vipi?" akauliza kwa mgutuko mara baada ya kuguswa shavu. Gina akaachia tabasamu pana lililomfanya yule dereva ajichekeshe kidogo.

"Ndiyo ndiyo akinadada…" akasema huku akijifuta udenda uliyochuruzika shavuni pake.

"Polisi," Gina akamjibu na kumuonesha kitambulisho chake, "Sasa sikia, tutoe hapa na gari yako, kisha we tuache uwanja wa ndege, urudi, mtu yeyote akikuuliza baadae mwambie ni polisi walikuchukua! Haya haraka." Yule dereva alijawa woga, akawasha gari na kufuata maelekezo ya wageni wake. Ilimchukua dakika ishirini na tano kufika Uwanja mdogo wa ndege wa Ibadakuli, Shinyanga. Gina na Jasmini wakateremka bila kumsemesha na kuondoka zao.

# 1vii

SCOBA akiwa na vijana wa Jeshi la Wananchi waliingia kwenye vichaka ambavyo ndege ya serikali ya Tanzania ilionekana kutua. Ilikuwa kilomita chache ndani ya mpaka wa Uganda na Tanzania, kwenye barabara ndogo ambayo hata hawakuijua ilitokea wapi na kwenda wapi. Hakukuwa na tatizo lolote, pori lilikuwa salama kabisa.

Baada ya kuhakikisha usalama huo, walivuta hatua huku wenzao wenye mitutu wakiwa wamelala kimya nyasini tayari kutoa ulinzi kama kuna lolote baya. Scoba na kepteni mwingine wa jeshi waliufungua mlango wa ile ndege ulioonekana haukufungwa sawasawa, akatumia *periscope* kuangalia ndani. Ndani ya ndege ile kulikuwa na watu waliokuwa wamelala vitini, shaghalabaghala. Hakukuwa na hata mmoja wao aliyeonesha uhai sembuse kujitikisa. Scoba akakiondoa kile kifaa na kutoa ishara kuwa ndani ni salama. Wakaingia, pamoja na wale wapiganaji wa jeshi.

Walikagua kila mtu bila kumshika ili wasipoteze ushahidi wa alama za vidole. Kulikuwa na abiria kumi na

moja, abiria wanne hawakuwepo kadiri ya hesabu waliyopewa na Katibu wa Wizara siku iliyotangulia.

Scoba na wale maofisa wa jeshi walikagua vizuri mpaka kwenye chumba cha marubani na kuwakuta wote wakiwa kwenye usingizi mzito. Scoba alianza kujisikia kizunguzungu na kichwa chake kuwa kizito, akawapa ishara wale maofisa kutoka nje ya ndege hiyo haraka. Wakafanya hivyo. "Tumeingia bila tahadhari ya vizuia sumu," akawaambia.

"Kuna dawa kali ya usingizi," mwingine akadakiza kusema.

"Lakini hawa watu ndani ya ndege hii hawajafa ila wapo kwenye usingizi mzito! Mmeona barakoa zote za oksijeni zinaning'inia, ina maana kuna mtu aliwawekea hiyo dawa," Scoba akaeleza.

* * *

Watu wawili walikuwa wameketi katika chumba kilichojengwa chini ya ardhi katika moja ya nyumba za kifahari huko Pasiansi, Mwanza. Muda wote walikuwa kimya hakuna aliyeongea na mwingine, katikati yao kulikuwa na chombo kidogo kama redio, kilichounganishwa na na kompyuta ndogo kabisa. Chombo kile kilikuwa kikitoa sauti ya watu waliokuwa wakiongea kwenye kikao fulani. Watu

hao walikuwa ama wakitabasamu au wakiongea kwa simu zao maalum kutoa taarifa kwa watu wao juu ya mpango unaopangwa na wale walio kikaoni. Mara hii mmoja akamtazama mwenzake na kumsemesha.

"Vipi hapo? Tumefanikiwa au bado?" akamwuliza yule mwingine

"*Fifty Fifty* kaka" akajibu yule mwingine.

"Yaani huyu fala wao anayejifanya anajua sana maswala ya kompyuta, ningemuona ana akili kama angeichoma moto hiyo chip lakini kuendelea kuihifadhi akijua kwamba haifanyi kazi kwa kuitoa kwenye ile saa, imekula kwake. Tena sasa ndio tunapata *data* za kutosha za jinsi wanavyojipanga," yule mwingine akajibu.

"Lakini mi nawaogopa hawa jamaa, mpaka wamegundua juu ya Khumalo, Robinson ina maana wapo hatua chache sana kutufikia. Huyo mtu wao wa kompyuta sio mjinga, lazima kuna kitu anafanya! Hivyo hapa tuwe na tahadari kubwa ikiwezekana tuondoke zetu kwani kuendelea kuwa hapa kunaweza kutuletea tabu," yule wa pili akaongeza na mwenzake akatikisa kichwa kuafiki.

"Ok mpe *Boss* ripoti!" akamwambia mwenzake ambaye alichukua simu yenye antenna ndefu na kuanza kuongea na

mtu wa upande wa pili. Baada ya mazungumzo na huyo bosi wao kwa takribani dakika moja na nusu hivi, akaiminya ndani ile antenna na kuiweka simu ile mezani. Akamtazama mwenzake, “Anasema tuhamishe makazi, maana yake tuondoke sasa, mpaka mambo yakitulia, tuje kufanya awamu ya pili. Lakini kwa hili labda yule mtu wetu atashtuka,” akaongea yule aliyekuwa na simu, kisha wakasubiri kidogo kabla ya kuzima hako kajimtambo kao.

* * *

Wakati wa tukio hilo, kambi ya dharula ya TSA iliwekwa Mwanza. Hapo waliweza kufuatilia kili kitu wanachokitaka, kila mmoja alitumwa huku au kule na usiku walikutana hapo walipopaita ‘Shimoni’, ili kupeana taarifa ya kilichojiri.

Wakati mazungumzo yakiendelea kati ya Madam S na vijana wake, mara kompyuta ndogo ya Chiba ikatoa mlio uliosikika mara tatu harakaharaka. Chiba akaelewa kuwa kuna mawimbi yanakatwa, akaigeukia na kuacha mjadala ule kisha akaanza kubofyabofya lile baobonye la ile kompyuta huku akitabasamu.

“Kamanda!” akaita, naye alipogeuka, akamwambia, “kazi imefika patamu, nilikuwa nasubiri mlio huu tu nikupe jibu…” Chiba akanakili namba fulani zilizoonekana katika

kompyuta yake na kisha akaingiza kwenye *software* nyingine, ramani ya ulimwengu ikajionesha dhahiri, akaendelea kucheza na namba zile kujaribu kuoanisha na vipimo halisi vya ardhini. Wakati huo wote walikuwa wamemzunguka Chiba kuangalia nini anafanya.

Chiba akageuka na kukuta kazungukwa, "Pasiansi kitalu namba 164 au 165 au 166 au 167 moja wapo," akasema.

"Kuna nini?" Madam akauliza.

"Hapo ndipo mawasiliano yetu yanapotua," akaeleza wakati akisimama na kuchukua bastola yake akaiweka sawa na kuipachika kiunoni. Amata akafanya hivyo, Gina nae akaunga. Mambo yameiva. Kazikazi! Wakatoka wote na kuteremka ngazi kisha wakachukua gari dogo lenye vyoo vyeusi wakaingia, Scoba akakamata usukani, wakapotea mtaani.

"Kama wasingezima huo mtambo wao, nisingeweza kuwagundua walipo," Chiba alieleza.

"Ina maana watakuwa wanajipanga kuondoka hao, kwa nini wazime?" kamanda akauliza.

"Unajua, inaonekana walikuwa wakiendelea kunasa mazungumzo yetu, sasa kama wamesikia hatua ambayo

tumefikia, hata ningekuwa mimi ningefunga virago na kuondoka haraka," Chiba akaongeza kusema.

"Madam, hawa watu wasikimbie, zuia ndege zote kuruka pale Mwanza Airport," Kamanda akatoa rai kwa bosi wake.

"Dah! Umenena," Madam S, akainua simu yake na kupiga kwa uongozi wa uwanja wa ndege kuomba ndege hata moja isiruke.

Haikuwachukua muda kufika mtaa wa Pasiansi, wakatafuta vitalu vyenye namba hizo na kuona nyumba nne zenye namba hizo zilizofuatana. Wakateremka kwenye gari lao, Madam S akaelekea dukani kama mteja wa kawaida. Pale dukani alinunua kinywaji baridi na kuvuta kiti, akaketi. Hapo alipo alihakikisha ana uwezo wa kuziona nyumba zote hizo ambazo Chiba aliziainisha. Kisha Chiba, Amata na Gina wakatawanyika huku na kule. Mpango mzima ulikuwa ni kuziweka kati nyumba zile ilhali Scoba akiendesha taratibu gari lake kati ya nyumba hizo kana kwamba anatafuta maegesho.

Nyumba ya kwanza, ilikuwa nyumba ya kawaida tu. Kwa nje ilionekana ni ya kupangisha. Upande wa mbele wa nyumba hiyo kulikuwa na genge la malimbichi na biashara nyinginezo.

Nyumba ya pili kulikuwa na familia moja inayoishi, ilikuwa nyumba ya kawaida tu, iliyozungushiwa wigo wa michongoma iliyoacha nafasi za kuweza kuona ndani. Nyumba ya tatu ilikuwa ni nyumba kubwa ya kisasa yenye kila kinachohitajika kuitwa makazi. Bustani kubwa yenye bembea na maua ya kuvutia ilikuwa mbele ya nyumba hiyo. Nyumba hii ilikuwa kimya, ni mfanyakazi tu aliyeonekana kumwagilia maji bustani hiyo ya kuvutia.

Gina akalijongelea lango na kubonyeza kengele, yule mfanyakazi akasogea. Wakati yeye akifanya hayo, wenzake walikuwa katika kona tofauti na kumwekea ulinzi kwa lolote litalotokea.

"Nikusaidie nini dada?" akauliza kwa lafudhi ya Kisukuma.

"Namuulizia mwenye nyumba, yupo?" akauliza.

"Mwenye nyumba? Mi tangu nianze kazi hapa sijawahi kumuona mwenyenyumba, ni wageni tu wanaokuja na kuondoka," akajibu.

"Fungua mlango," Gina akaamuru.

"Sasa uwende wapi? Hakuna mtu humo ndani," akasema huku akifungua lile lango na Gina akapita ndani.

Kamanda Amata akaiweka bastola yake vizuri, akaipachika miwani yake usoni akitazama pale mlangoni ambako Gina aliingia na kuielekea nyumba hiyo. Scoba akainua bunduki kubwa aina ya AK 47 iliyofungwa lensi yenye nguvu na kupachika katika dirisha la gari lile, akaitazamisha kule kunako lile jumba, huku akichungulia taratibu kutazama kama kuna mtu yeyote ambaye ataleta tabu ili amfumue bila huruma.

"Usiende huko, hakuna mtu dada, utaniletea matatizo kwa mabosi wangu…" yule mfanyakazi akamwambia Gina. Amata akaona hatari inayoweza kumkabiri mwanamke huyo, akawapa ishara wenzake na kuyaacha maficho yake. Akalifikia lile geti na kusimama. Akatazama kwa makini sana kila kinachoendelea. Gina akaukaribia mlango mkubwa wa jumba hilo. Jicho la Kamanda Amata likamtazama yule mfanyakazi ambaye aliuacha ule mpira wa maji na kuliendea bomba ambalo ameliunganisha na ule mpira. Alipoona hilo, akausukuma ule mlango na kuingia kwenye ile bustani. Akaacha kumtazama Gina na kumfuata yule mfanyakazi taratibu.

Yule mfanyakazi akalifikia bomba na kufunga maji. Wakati huo huo Kamanda Amata akasikia mtu akipiga

kelele na mara kimya ghafla, akageuka nyuma hakumuona Gina.

“Gina, Gina, Ginaaaa!” akaita kwa nguvu, na muda huo huo Madam S na Chiba wakajitoma katika uwa huo.

“Vipi?” Chiba akauliza akiwa na bastola mkononi.

“Gina amepotea ghafla,” Kamanda akajibu. Wakati akigeuka kutazama kule bombani alimshuhudia yule mfanyakazi akianguka vibaya kwenye wigo wa jumba hilo. Akamkimbilia, alikuwa anavuja damu, mguu wake umevunjwa kwa risasi mbaya kabisa.

“Ulikuwa unakimbia ee? Haya nieleze, umefanya nini?” Kamanda akauliza huku akiwa kamkanyaga kwenye jeraha lake, “Husemi? We sugu sio? Ujue sicheki na mtu sasa?” Kamanda Amata aliushika mguu wa yule mfanyakazi na kuuzungusha vibaya.

“Aaaaaaa niache, nasema…” akapiga kelele

“Sema, yule mwanamke yuko wapi?”

“Kuzimu, kaingia kuzimu!” akajibu.

“Kuzimu ndio wapi?

“Kuzimu, Kwani we hukujui Kuzimu?” akamwuliza Amata kwa kejeli. Kamanda akaunyonga kwa nguvu ule mguu.

“Aaaaiiiiiiiggggghhh!” mifupa ya mguu ilitawanyika vibaya, ukavunjika.

“Na wenye nyumba wako wapi?” Kamanda akauliza.

“Umenivunja mguu mseng* wewe! Hii nyumba ya wageni, wameondoka,” akajibu.

“Wameenda wapi?”

“Sijui, walikuwa hapa wiki mbili lakini leo wameondoka,” akazidi kutoa maelezo.

“Ok, wametoka saa ngapi na wamesema wanakwenda wapi?” Kamanda akazidi kuhoji

“Mi sijui kaka, niache basi, ushanivunja mguu, inatosha…”

“Nioneshe, Kuzimu ni wapi?” akambana. Yule kijana akiwa na maumivu makali akamwonesha mkono kwenye bomba alilokuwa akitumia kuunganisha mpira wa maji. Kamanda Amata akamwacha na kuliendea lile bomba.

“*Hey, go to hell,*” yule mfanyakazi akampigia kelele Amata. Kamanda alipogeuka nyuma alijikuta akitazamana na

domo la bastola aina ya *Revolver*, iliyokuwa imeshikwa barabara mkononi mwa yule kijana. Ubaridi ukamteremka Kamanda kuanzia utosini mpaka unyanyoni. Paji lake la uso lilitengeneza makunyanzi ya hasira, "Niue kama una shabaha!" akamwambia. Yule kijana akatoa usalama wa ile bastola tayari kumlipua Kamanda. Sura yake iliyobeba taswira ya maumivu makali haikuonesha masihara hata kidogo.

* * *

Gina alijikuta akidondoka katika shimo au chumba kidogo chenye ukubwa wa mita moja na nusu ya mraba. Alianguka juu ya vitu vigumu, alijisikia maumivu makali sana. Akajaribu kunyanyuka akipapasa huku na huko, hakuweza. Giza lilitawala chumba hicho. Harufu ya uvundo na hewa nzito vilikifudikiza. Miguuni pake alikuwa alihisi kama mikono ya watu ikimshika mara kwa mara. Alipouinua mguu na kuushusha mahali pengine alihisi kakanyaga kitu kama nazi lakini hakuweza kuona chochote. Akaingiza mkono mfukoni mwake kutafuta simu, akaitoa, akawasha tochi na kumulika ndani humo. Lo! Gina alishtuka na kubaki katumbua macho. Mifupa ya watu ilijazana ndani ya chumba hicho kidogo.

Gina alijikuta katikati ya wafu, akatetemeka kwa hofu, alihisi amefika kuzimu.

*"Shiit!"* akang'aka, huku akitetemeka sana. Akainua simu yake na kubonya namba za Amata, akaweka sikioni. Hakuna kitu. Simu hiyo haikuita kabisa alipoichunguza akakuta ikimuonesha hakuna mtandao eneo hilo. Gina akachanganyikiwa. Akatazama kwa kumulika kuta za shimo au chumba hicho, zilikuwa kuta laini sana zisizo na hata mkwaruzo. Zilikuwa zimebandikwa marumaru, harufu ya uvundo ilikuwa imetawala ndani yake. Hakujua afanye nini.

*Ntafia humu?* Akajiuliza akikata tamaa.

* * *

Madam S na Chiba walikuwa ndani ya jumba hilo, kila mmoja bastola mkononi wakikagua chumba kimoja baada ya kingine. Kila chumba walichopita kilikuwa tupu, ni vitanda na vitu vingine tu.

"Chiba, nilinde," Madam akamwambia Chiba kisha akaibana bastola yake kwenye kiuno cha suruali aliyovaa, akaanza kufungua kabati moja baada ya jingine. Kila moja lilikuwa tupu, zaidi ya mataulo na mashuka hakuna jipya. Akatoka na kuingia chumba kingine, nako hivyo hivyo, akapita vyumba kama vinne hivi. Akiwa katika ujia mdogo

wa kuelekea maliwato, akauona mlango mwingine pembeni. Chiba akiwa nyuma yake na bastola mkononi iliyokamatwa kwa mikono miwili tayari kutii amri yoyote itakayoamriwa alikua nyuma ya Madam S akitazama kila kona kwa makini.

Katika masikio yao wote walikuwa wamepachika vifaa maalumu vilivyowafanya kuweza kuwasiliana muda wote, hivyo walikuwa wakisikia mahojiano ya Kamanda Amata na yule mtu kule nje. Mlango ulio mbele ya Madam S ulikuwa umefungwa, akautikisa tena na tena lakini ulifungwa kabisa. Akachukua kibanio cha nywele zake, akakifyatua kwa ndani na kutoa funguo malaya. Akacheza na kile kitasa, sekunde chache tu kikafyatuka. Akaingia ndani kwa hadhari kubwa. Chumba hicho kilikuwa kama stoo, makolokolo ya ufundi na vitu mbalimbali vililundikana katika mashubaka yaliyo wazi. Mbele yake kulikuwa na mlango mwingine ulioonekana haukufungwa kwa kuwa uliacha uwazi mkubwa kati yake na muimo wake. Akavuta hatua moja na kuufikia. Hisia zake zikagoma kumruhusu kuingia. Afanyeje? Akapata wazo, akatanguliza mkono aone kama kuna hatari yoyote ambayo ingemshambulia. Ghafla vitu kama misumari vilifyatuka kwenye pande mbili za kile chumba na kutawanyika kila kona.

“Aaaaaaiiigghhh *Shiiit*!” Madam alilalamika maumivu pale msumari mmoja ulipotoboa kiganja cha mkono wake.

“Madam!” Chiba akaita. Mwanamama huyo akamuoneshea ishara ya mkono kuwa abaki pale pale na vilevile. Akachomoa kale kamsumari mkononi mwake, kisha akatoa kitambaa chake cha shingoni na kujifunga kiganjani akidhibiti damu kutotoka kwa wingi. Alipohakikisha yuko sawa, akafanya tena mtindo uleule, akatanguliza mkono ndani ya chumba kile, hakukutokea chochote. Akamtazama Chiba aliyekuwa kasimama imara, mita kama tatu nyuma yake. Chumba kile kilitegwa silaha maalumu ambapo mtu yeyote asiye rafiki na nyumba hicho akiingia angeshambuliwa na bomu la misumari lakini kama ni mwenyeji anajua nini cha kufanya kwanza. Madam S akaingia na kutazama yale makabati yaliyopangwa ndani ya chumba hicho. Hakugusa kitu, alikuwa akitazama tu. Baadae akaanza kugusa na kutikisa hapa na pale. Mahala fulani chini ya moja ya makabati hayo kulikuwa na kipande chamarumaru ambacho kilitofautiana ua moja na vingine. Si rahisi kwa mtu wa kawaida kugundua tofauti hiyo. Alipoikanyaga, mara kabati moja lililo mbele yake likasogea pembeni taratibu na kuacha mlango mmoja uliofungwa mkabala na yeye. Akashika kitasa na kukinyonga, ule mlango badala ya kufunguka ukafyatuka kwa juu na kuwa kama

unaoanguka kwenda ndani taratibu, mbele yake kulibaki na uwazi ambao ni sawa na chumba kidogo. Akasita kuingia.

* * *

Kamanda Amata alitulia palepale akipanga cha kufanya, hakuweza kugeuka kwani alijua wazi kuwa kwa kugeuka kwake basi kijana huyo angefyatua bastola yake.

"Ua!" akatamka. Yule kijana hakuelewa, wakati akishangaa, alijikuta akitupwa nyuma na kujibamiza kwenye nguzo ya umeme, akaanguka chini. Marehemu. Risasi ya Scoba ilitii amri iliyopewa. Amata akaliendea lile bomba na kutazama koki yake, ndipo alipogundua kuwa katikati ya koki kuna swichi ndogo ya rangi ya *bronze*, akajaribu kubonyeza na kuishika bila kuachia.

Mbele ya mlango wa kuingia nyumba ile pakafunguka, na shimo la urefu wa futi nane likawa wazi. Gina aliona mwanga wa nje, hakuamini.

"Kamandaaaa!" akaita. Amata akasikia sauti ya Gina, akamwita Scoba na kumwambia atazame humo ndani. Scoba akatoka garini na bunduki yake mkononi mpaka pale akachungulia ndani akamuona Gina. Scoba akatazama huku na kule, akaenda kutafuta kitu cha kuweza kumsaidia mwanamke huyo kutoka. Pembeni tu palikuwa na kipande

cha bomba la chuma. Akakichukua na kukipachika katikati ya ile milango ya shimo. Akalizuia lisijifunge.

"Achia!" akamwambia Amata ambaye bado alikuwa kaishikilia ile swichi. Ile milango ikarudi lakini ilizuiwa na lile bomba. Scoba akakimbia garini na kutoa kamba ngumu ya kuvutia gari, akarudi. Kwa pamoja na Amata wakatumbukiza huku kipande wakishika wao.

"Gina, haya twende!" Scoba akamwambia Gina. Naye akaishika ile kamba barabara, kisha wakaanza kumvuta juu mpaka walipomtoa.

"Hawa watu ni wakatili sana, ina maana ni watu wangapi wamefia kwenye shimo hili?" akauliza Kamanda.

"Na serikali haijui lolote, mnasikia tu mtu kapotea lakini hamumwoni tena," Scoba akajisemea kwa sauti ya chini, hii lazima ifanyiwe kazi.

"Gina unajisikiaje?" Kamanda akamwuliza.

"Mwili unaniuma maana niliangukia juu ya mifupa, lakini niko poa," akajibu. Akaitazama simu yake sasa ilimuonesha kuwa mtandao unapatikana.

"Vipi? Mbona washangaa?" Kamanda akamwuliza Gina.

“Nashangaa, kule chini simu yangu ilikata mtandao lakini hapa inasoma,” Gina akaeleza.

“Lazima wafanye hivyo kwani bila hivyo hapa pangejulikana kitambo sana,” Kamanda akajibu, “*Ok*, Gina na Scoba wekeni ulinzi nje hakikisha watu wanakaa mbali na eneo hili, mi naenda ndani kuwasaidia Madam na Chiba,” akatoa maelekzo. Tayari watu wa eneo hilo waliikaribia ile nyumba. Kama kawaida ya Watanzania, hatupitwi na kitu.

Timu nzima ya TSA ilikuwa katika eneo la jengo hilo, hii ilikuwa ni mara ya kwanza watu hawa hatari wa serikali ya Tanzania kuwapo katika kazi moja, hii ilimaanisha kazi ilikuwa nzito si kitoto.

Ndani ya jumba lile Madam S alikuwa ameteremka chini kabisa ya jengo na wakati huohuo Amata aliungana nao.

“Amani!” Kamanda akatamka.

“Amani!” Chiba akajibu, bila hivyo ilikuwa ni rahisi kwa Chiba kufyatua risasi yake.

“Nje kwema vipi humu?”

“Utata mwingi Kamanda,” Chiba akajibu.

“Ok, shuka kwa Madam mi naweka ulinzi wenu,” kamanda akamwambia Chiba, na wakati huo Chiba akashusha bastola yake na kuiweka kiunoni, akateremka ngazi kwenye ule mlango na kuungana na Madam kule chini.

* * *

Hali ya hewa ilikuwa imetulia kabisa katika Uwanja wa ndege wa Mwanza, abiria walioahirishiwa safari kwa muda walikuwa wamechoka kusubiri wakimlalamikia uongozi wa uwanja kuwa kwa nini hawawapi sababu ya kucheleweshewa safari zao. Wenye viherehere walikuwa washafika ofisini kwa mkurugenzi huyo.

“Kwa nini mnatufanyia hivyo jamani, nusu saa sasa imepita,” mmoja alilalama.

“Kama mmeshindwa kazi semeni bwana sio mnakuwa wababaishaji tu,” mwingine akadakia huku akirusha mikono yake juu huku na huko.

“Yaani nchi hii bwana, kila kitu wanachukulia kawaida tu,” sauti upande wa pili wa abiria ikasikika.

Yule mkurugenzi, kijana mtanashati, kwa kutumia kipaza sauti cha matangazo akawatangazia watu ili kuwashusha presha.

"Mtusamehe ndugu abiria, kusimamaishwa kwa safari hatujaamua sisi wenyewe, hii ni amri ya serikali haina swali wala jibu ni matekelezo tu."

Muda huo huo gari moja dogo, jeusi likasimama maegeshoni mwa uwanja huo. Madam S akifuatana na Kamanda Amata wakateremka na kutembea harakaharaka kuelekea katika ofisi ya mkurugenzi huyo, wakamkuta ofisini huku askari polisi wakiwa mlangoni kwa ulinzi.

"Mnaenda wapi?" wale polisi wakawauliza.

"Tuna shida na mkurugenzi," Madam akajibu.

"Hamuwezi kumuona kwa sasa, ana kazi nyingi," yule polisi akajibu.

"We! Usinipotezee muda, hujui unaongea na nani sawa?" Madam akaongea kwa hasira wakati huohuo Kamanda Amata alikwishafungua mlango na kuingia ndani, walimkuta yule kijana akiwa kajiinamia kimya.

"Oh, karibuni sana," akawakaribisha mara baada ya kujitambulisha kwake, "Sasa tangu mliposema kuwa tuzuie ndege yoyote isiondoke tumefanya hivyo na mpaka sasa ndege zote nne zilizokuwa ziruke ndani ya saa mbili hizi bado zipo na abiria wake kama unavyowaona almanusura

waning'oe macho ndio maana nimeweka polisi hapo mlangoni," akaeleza.

"Ok, sasa ni hivi, kuna watu tunaowatafuta, lakini hatujui hata sura zao wala majina yao, kwa hiyo tutafanya gwaride la utambuzi sasa kwa abiria wote, Madam akaeleza.

Dakika tano baadae, abiria wote 130 waliokuwa uwanjani hapo walipangwa na kutakiwa kuingia katika ofisi ya Meneja mmoja baada ya mwingine kisha kuelekea kwenye ndege zao. Zoezi lilichukua saa nzima, mahojiano makali ya kujua wapi unatoka, unakwenda na unafanya nini yalichukua nafasi lakini hayakuzaa matunda.

"Hapa hakuna mhalifu, wote wanaonekana raia wema tu," Kamanda akasema, "Je; kuna ndege nyingine yoyote iliyoondoka kabla ya hizi?" akauliza.

"Ndiyo ipo ndege ya kukodi ya shirika la *Darair*, imeruka dakika ishirini kabla hamjapiga simu," meneja akajibu.

"Ilikuwa na abiria wangapi?"

"Imeondoka na abiria watatu tu, wawili wanaume na mmoja mwanamke, wote ni raia wa kigeni," akaeleza.

“Ok, kama inawezekana nahitaji kujua taarifa zao kutoka kwa wakala wa kampuni hiyo zaidi ya hapo naomba uruhusu watu waondoke maana wamenuna wasije kupasuka,” Kamanda akaongea na kuchomekea utani kidogo ili kumfanya Meneja huyo asiogope sana.

*   *   *

Mikononi mwa Kamanda Amata na Madam S kulikuwa na picha sita za watu watatu, kila mmoja alitolewa nakala mbili za picha yake.

*Stephen Peterson, raia wa Norway*

*Mfanyabiashara za madini, umri miaka 32*

*anaishi Texas Marekani, yupo nchini kwa wiki moja.*

Kamanda Amata akaiweka pembeni taarifa hiyo. Akachukua nyingine.

*Richard Clouch,*

*Mwandishi wa habari za kibiashara wa gazeti la Mirror la Uingereza*

*alikuwa nchini kwa wiki moja anishi*

*Manchester ana miaka 30.*

Amata akaiweka pembeni na kuchukua ya yule mwanamke. Akaitazama mara mbili mbili. Akili yake ikafanya kazi haraka kumchambua mwanamke huyo kwa muonekano wake.

*Jennifer Spencer*

*Umri miaka 29, raia wa Honolulu, Mtalii,*

*Alikuwa nchini kwa wiki moja.*

Hii kidogo ilimvutia Kamanda Amata hasa ukizingatia jinsi watu hawa wenye taaluma tofauti kuwa pamoja. Alivutiwa zaidi na Jennifer, akaitazama ile picha ya yule mwanamke kwa umakini wa hali ya juu.

"Umesema wanaondoka na ndege gani?" akamwuliza mhudumu wa ofisi hiyo.

"Kwa taarifa za tiketi zao, wanaondoka na KLM leo saa sita usiku. Sasa wameelekea Dar es salaam," akajibu.

Kamanda Amata akamtazama Madam S, akamwona jinsi sura yake sasa ilivyoanza kuupoteza usichana na kuingiwa na uzee wa ghafla, "Mama, ni sawa?" akamwuliza.

“Si sawa hata kidogo,” akamgeukia yule mhudumu, “Ndege yenu iliyowasafirisha hawa watu imeshatua Dar es salaam?” akatupa swali.

“Ndiyo imetua robo saa ilopita,” akajibu.

“Ok, asante sana, usihofu, tatizo ni kuwa hawa watu walikuwa nchini na kufanya kazi tofauti na vibari vyao ndio maana tunawafuatilia,” Kamanda akamweleza yule binti kisha wakaagana.

* * *

Siku hiyohiyo, Madam S na vijana wake waliwasili Dar es salaam. Breki ya kwanza ilikuwa Shamba kama kawaida yao wanapokuwa na hoja nzito za kutafuatia ufumbuzi. Safari hii walikuwa na mheshimiwa waziri waliyemleta hapo kwa siri. Taarifa za kupatikana kwake zilibanwa, hakuna chombo cha habari wala taasisi yoyote iliyoruhusiwa kutoa habari hiyo. Waziri yule alikuwa akipata kahawa huku akiendelea na matibabu chini ya Daktari Jasmini. Baada ya kuwa kapata nafuu na anaweza kuongea vizuri, akawekwa kwenye chumba maalum cha mazungumzo kilichokuwa na meza moja na viti vitatu tu. Lakini upande wa pili Chiba na wengine walikuwa kwenye mitambo wakisikiliza kila kitu ambacho waziri huyo alitakiwa kuzungumza kuhusu tuhuma

hizo. Ulikuwa ukisubiriwa ugeni wa watu watatu tu kwenye ngome hiyo ya siri, *safe house* au *shamba*.

Dakika tano baadae, gari maalumu la idara ya TSA lililokuwa likiendeshwa na Scoba liliingia kupitia mlango wa nyuma wa jengo hilo kongwe maeneo ya Gezaulole. Likaegeshwa ndani kabisa mwa egesho la siri. Rais, makamu wake na waziri mkuu waliteremka, wakapokelewa na Madam S na Gina, wakakribishwa ndani na kupitishwa moja kwa moja mpaka kwenye chumba maalum walichoandaliwa. Mpaka wanafika hapo waheshimiwa hao hawakujua wako wapi kwani gari waliotumia kufika nalo hapo halikuwa likionesha chochote kutoka ndani hivyo abiria hakujua ni wapi anapelekwa.

"Sasa hapa ni wapi?" Waziri mkuu akamuuliza Gina.

"Mheshimiwa, hapa nimahali pasipojulikana na mtu, hata mimi mwenyewe sipajui, na wanaoshi humu ni watu wasiojulikana…" kisha wote wakacheka.

Kila mtu alipokuwa tayari katika mahala pake, Madam S na Kamanda Amata wakaanzisha mazungumzo na mheshimiwa yule waziri. Waziri hakujua kama kuna ugeni mzito ndani ya jengo hilo na unamsikiliza hatua kwa hatua.

"Tulitua na ndege katika uwanja mdogo wa North Mara majira ya saa tatu asubuhi, nikiwa na wageni wangu wote na ujumbe niliofuatana nao. Tukiwa pale tulifanya kila tulichotakiwa kufanya, tulikagua mgodi katika vitengo muhimu, tukaongea na meneja na wafanyakazi baadhi kuwasikiliza kero zao na pia kujua ufanisi wa kazi zao…"

Kamanda Amata akamkatisha, "…Nikukatishe mheshimiwa, hebu niambie juu ya wageni wako waliofuatana nawe, unawajua kiasi gani hasa hawa wa kutoka nje," akahoji.

"*Yeah*, wale jamaa mwanzoni niliwaona ni watu wenye nia nzuri ya uwekezaji kwa sababu mmoja alikuwa ni muwakilishi wa kampuni ya *Robinson Dia-Gold Mines* ya Canada, na mwingine ni kutoka *Cunglia Cold Mines* ya Uingereza kila upande walikuja wawili, na watu hawa nilikutana nao miezi sita iliyopita katika mkutano maalumu wa uwekezaji huko Geneva ambako nilikwenda nikifuatana na katibu wangu." Yule waziri alielezea mengi sana juu ya safari hiyo.

"*Ok*, Sasa unajua una kesi gani ya kujibu?" Kamanda akamwuliza.

"Hapana na ndio maana nashangaa, sijui kesi yoyote ninayotuhumiwa kama ipo," akajibu. Madam S na kamanda

Amata wakatazamana. Kisha wakawasha luninga ndogo na kumuonesha habari iliyorekodiwa kutoka Televisheni ya Taifa ikielezea wizi wa almasi na vifo vya watu wawili huku yeye waziri akituhumiwa. Hali ya mshangao na mshtuko ilionekana ghafla usoni mwake, akaanza kupumua kwa nguvu.

"Tulia Mheshimiwa, usihofu, hii ni habari iliyotokea ndani ya masaa sabini na mbili yaliyopita, na wewe ni mhusika. Kabla ya kupandishwa kizimbani tukakuleta hapa kwanza ili tujue ukweli," Madam akaeleza.

"Haya tuambie uko vipi na tuhuma hizi, kwa nini umefanya wizi huu wa mali ya wavuja jasho wa Taifa hili?" Kamanda akapiga swali la moja kwa moja.

"Hapana! Hapana! Sihusiki, nashangaa imekuwaje, unajua kilichotokea, mnajua mimi sikuwepo duniani kwa muda mpaka nimejikuta pale Mwanza hospitali."

"Haya, tuambie, nini unakumbuka cha mwisho katika safari yako?" Kamanda akauliza.

"Naomba usiwadanganye Watanzania, kwa kuwa wewe umeiba na inafahamika hivyo," Kamanda akamalizia.

"Hapana, unajua nini … mnajua kilichotokea? Sasa naanza kuelewa, sasa naelewa, naelewa, tulipokuwa angani

wakati tukitoka Mara kwenda Mwadui, tulikumbwa na hali mbaya ya hewa, (akatulia kidogo) kisha tukatangaziwa na rubani kutumia barakoa za oxygen, basi! Basi… hapana sikumbuki kingine. Kweli, mi sijaiba, sihusiki…" yule waziri alikuwa kama anaweweseka, hali hiyo ilijionesha wazi, Madam S akatikisa kichwa.

"Mheshimiwa," akaita, "Mheshimiwa!" akaita tena, ukimya ukatawala. Dkt. Jasmini akaingia haraka na mtungi wa Oxygen, akamwekea puani kumsaidia kupumua, kisha kwa msaada na Kamanda Amata wakamtoa kitini na kusaidiana kumbeba mpaka kwenye kitanda. Jasmini akafanya kazi ya ziada ya kumuwekea drip ya maji, kisha akachukua vifaa vya kupimia presha *(sphygmomanometer na stethoscope )*, akaviunganisha na kuchukua vipimo, dakika moja na sekunde kadhaa, akakitoa masikioni kile kifaa na kulegeza ile mashine ya presha pale mkononi mwa yule.

"Presha imeshuka, muacheni apumzike kwanza," Dkt. Jasmini aliwaeleza.

Uande mwingine Rais na makamu wake pamoja na waziri mkuu, walibaki wakitazamana.

"Nini hiki?" Rais akmuuliza Waziri Mkuu.

“Hapa kuna utata, tena utata mkubwa sana hapa mimi ni kama naangalia muvi au nasoma vitabu vya riwaya, sielewi elewi tu,” Waziri Mkuu akajibu. Mara mlango ukafunguliwa, Madam S akaingia katika chumba hicho.

“Ndio Selina!” Rais akadakia.

“Kama hivyo Mkuu, lakini usijali, ukweli wote utaupata na taarifa itakuja Ikulu ndani ya masaa sabini na mbili kwani tuna watu kumi na nne wa kufanya nao mahojiano,” Madam akawatoa hofu.

“Nakuamini sana pamoja na vijana wako, naona jinsi mlivyojipanga, lakini hebu nipe maoni yako maana hapa nakosa cha kuwajibu Watanzania, nakosa cha kuongea na Waandishi wa habari juu ya kadhia hii, Ikulu haikaliki,” Rais akamwambia Madam S.

“Hatuwezi kusema kahusika katika wizi au la, ila tutakapohoji wengine tutaoanisha mambo kisha tutajua kipi ni kipi na hapo sasa ndiyo tutaingia kazini kukamata waliohusika, hata wawe wanaishi Pluto au Juani kote tutaenda, tupe muda Mheshimiwa Rais. Leo jioni tutakuwa na awamu ya pili ya mahojiano na watu wengine, tutajua mbichi na mbivu,” akamaliza.

* * *

Usiku huo tayari Kamanda Amata alikuwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwl. Nyerere akaijaribu kuona kama anaweza kuwakamata watu wake. Alikuwa amezinasa picha zao kichwani. Aliegesha gari na kuteremka kisha akafunga mlango nyuma yake. Akiwa ndani ya suti nadhifu iliyoficha moja ya bastola zake anayoipenda sana, Kamanda Amata akatembea taratibu kuelekea ofisi ndogo ya KLM. Pale alimkuta mwanadada mbeja kwelikweli akiwa ametulia ofisini mbele akitazama kompyuta kubwa aliyokuwa akiitumia kutatulia matatizo yake ya kikazi. Akakaribishwa naye akakaribia, akavuta kiti akaketi.

"Naitwa George Kamasi," akajitambulisha uongo kisha akampa kitambulisho yule mwanadada, akakipokea na kukisoma. Kilimwelezea Kamanda Amata kama George Kamasi, mwajiriwa wa Wizara ya Mambo ya Ndani katika jeshi la Polisi kitengo cha uchunguzi wa makosa ya Jinai. Yule mwanadada akamrudishia, "Ehne bwana Kama… mh! Na hilo jina lako mpaka linatapisha," akasema yule mwanadada.

"Uwe na adabu unapoongea na watu usiowajua," Kamanda akapiga mkwara.

"Nikusaidie nini?" akauliza kwa utulivu baada ya kuona bastola iliyolazwa mezani kwa utulivu.

"Naomba unipe orodha ya wasafiri wako hasa wanaoelekea Uingereza, Canada na Honolulu," Kamanda akaomba. Yule mwanadada akafanya harakaharaka kuitoa orodha hiyo kwenye mashine yake, akaprinti na kumpatia. Amata akaitazama, haikumfurahisaha sana kwani Honolulu hakukuwa na abiria yoyote anayekwenda huko, Uingereza kulikuwa na abiria kumi na tano lakini wote walikuwa wanafunzi wa chuo kimojawapo cha huko ambao walikuja kwa utalii wa kimasomo na Canada kulikuwa na watu wawili, lakini wote wanawake. Akashusha pumzi.

*Ina maana wametucheza shere?* Akajiuliza. Akachukua zile karatasi na kuzikunja kisha akazitia katika mfuko wa ndani wa koti lake.

"Umeridhika?" yule mwanadada akauliza. Amata akamkazia jicho, "Sijaridhika," akamwambia.

"Sasa mimi nifanyeje ili uridhike?"

"Ulale na mimi leo?" Kamanda akamjibu bila kucheka.

"Hahahahaaaaa huwa silali na wanaume wa ovyo ovyo, unanionaje kwanza, nalala na mapedeshee, watu wenye pesa zao," akajibu huku akinyanyuka.

“Hebu tulia hapo unaenda wapi? Unafikiri mi nimekuja kucheza hapa!” Akatoa karatasi nyingine na kumpatia. Hizi zilikuwa tatu, zenye picha za watu watatu tofauti.

“Hawa ni nani?” yule binti akauliza.

“Nataka uwatambue hao watu, kama wamekuja hapa kukata tiketi siku za nyuma, au unao katika ndege yako,” yule mwanamke akazitazama zile picha kwa kuzirudiarudia.

“Ni nani hawa?” akauliza.

“Hao ni wahalifu wa kimataifa na ukiwatetea… jela inakuita,” Kamanda akazungumza kwa sauti kavu. Yule mwanadada akatazama tena zile picha. Akachukua namba za tiketi zao na kuingiza kwenye mfumo wao wa kompyuta.

“Hamna watu kama hawa kwenye ndege yetu, kwanza tiketi zao ni feki, ona,” akamgeuzia kioo cha kompyuta, kisha akaongeza, “Kama waliwaambia kuwa wanasafiri na ndege yetu leo, hatuna hawa abiria kaka, samahani…”

Amata akachukua zile karatasi zake na kurudisha zilikokuwa. Akanyanyuka na kuwa wima.

“Ok, asante! Na lile nililokwambia la kulala na mimi, tumeishia wapi?” Kamanda akachokoza.

“Heee! Hebu nitokee huko, we unafikiri mi wa kulalwa hovyo hovyo tu, nina watu wangu wenye pesa sio kama wewe unayetegemea kamshahara ka wizara mwisho wa mweli, *go fish*,” akamwambia kwa dharau huku midomo yake akiwa kaibetua juu na mwisho akasindikiza kwa sonyo refu..

“Asante kwa maneno yako machafu, ila ujue tu utaishia mikononi mwangu iwe kwa heri au kwa shari,” akamwambia na kuondoka.

* * *

“Yaani bila shaka yoyote tulitekwa, nakumbuka tukiwa tuko angani dakika thelathini baada ya kuruka kutoka Mara, hewa ndani ya ndege ilikuwa nzito sana, mzunguko wake ukawa hafifu. Nilipotazama kwenye vipimo vinavyoonesha mfumo wa oksijeni, vikanionesha kuwa kuna shida katika mfumo huo, hivyo sikuwa na budi ili kuokoa abiria wangu nikawaamuru kuvaa *mask*. Baada ya kuvaa *mask* mimi mwenyewe nikajikuta nashindwa kupumua sawasawa, kifua kinakuwa kizito, mwili unaishiwa nguvu, nikavua na kuitupa kando,” rubani wa serikali aliyekuwa katika ndege ya msafara wa waziri alieleza kinagaubaga.

“Baada ya hapo uliona nini?” Madam akauliza.

"Baada ya hapo niliona kama kivuli cha mtu anayeingia ndani ya chumba cha rubani na kuwatoa wenzangu vitini, hapo sikuona tena kilichoendelea," akajibu.

"Pole sana Kepteni. Kuna wizi mkubwa sana uliofanyika na ndege yako imetumiwa kubeba kasha tano za almasi zenye thamani ya Zaidi ya Tsh Billioni themanini kwa hesabu ya haraka haraka," Madam akamweleza. Yule Rubani akashtuka na kushikwa na hamaniko, "Lo! Itakuwa walewale wazungu, maana hata kabla hatujaondoka walikuwa wadadisi sana, mara waniulize aina ya ndege ninayoirusha, mfumo wake ukoje, mara hiki mara kile, ah! mi nikawa nawapotezea tu," akawaambia.

Baada ya saa moja ndani ya chumba hicho cha mahojiano alikuwamo mwanadada mmoja mrembo tu, aliyesuka nywele zange mtindo wa rasta za Kimasai zilizomkaa vizuri. Madam S alimkaribisha kitini na kuketi katika mtindo wa kutazamana. Madam S alimtazama mwanadada huyo kwa dakika tano bila kumsemesha neno, kisha akafungua kinywa chake.

"Umeolewa?" akamwuliza.

"Hapana," naye akajibu kwa sauti ya unyonge.

"Una bwana au mchumba?"

"Ndio, nina mchumba tutafunga ndoa mwezi ujao," akaeleza.

"Nieleze Historia yako kwa kifupi," Madam alimwomba na yule dada akafanya hivyo.

"Kwani samahani mama, hapa ni wapi na nafanya nini? Ni haki yangu kujua kama Mtanzania," yule mwanadada akauliza.

"Ok, we ni Mtanzania mzuri unayejua unachotakiwa kujua. Hapa ni hospitali ya vichaa, wewe umeletwa hapa baada ya kukamatwa ukitembea bila nguo mitaani," Madam akamwelieza.

"*What?* Mimi?" akashtuka na kusimama.

"Ndiyo wewe, ulikuwa unazunguka mtaani bila nguo kabisaaaaaa, nsdo maana nikakuuliza una mchumba au bwana," Madam akamwelewesha.

Upande wa pili wa chumba, Chiba alipasua cheko alililoshindwa kulizuia, lakini bahati nzuri sauti haiwezi kusikika mahali popote na wala kuingilia ile rekodi anayoifanya ya mahojiano hayo.

Gina naye alikuwa hoi kwa kucheka, "Mwe! Huyu bibi huyu anajijua mwenyewe, sasa ona alivyomvuruga dada wa

watu halafu mwenyewe yuko sirias," Gina alimwambia Chiba.

"Hebu nambie, cha mwisho unachokumbuka katika maisha yako, ulikuwa wapi?" Madam akaanza.

"Nilikuwa Musoma katika mgodi wa North Mara," akajibu.

"Ulienda kufanya nini?"

"Nilifuatana na msafara wa waziri na wawekezaji wake katika kutembelea migodi ya serikali."

"Enhe baada ya hapo," Madam akahoji.

"Sijui kwa kweli na hisi tulipata ajali, maana tukiwa kwenye ndege hali ya hewa ilikuwa mbaya sana, sikumbuki kilichotokea zaidi isipokuwa nikajikuta hospitali," akajibu. Kisha Madam S akamweleza kila kitu juu ya sakata la madini, yule mwanadada aliishiwa nguvu kabisa, macho yakamtoka pima.

"Usiposema ukweli, unafungwa, kwa maana wenzako wote wametoroka we ndio tumekukamata," Madam akamtishia, "Uliwaonaje hao wawekezaji?" akaongeza swali.

"Aaa nimekutana na wawekezaji au wafanyabiashara wengi pale wizarani kwa kuwa mimi ofisi yangu ni mambo

ya mawasiliano, ila hawa walikuwa walikuwa wahuni sana, halafu walikuwa hawatulii kwenye ndege, mara chooni, mara kwa *air hostess,* mara sijui vitu gani, mmoja akawa ananitaka kimapenzi pindi tukirudi Dar," akaeleza. Maneno haya yakamgusa Madam S, tofauti na wengine wote, huyu alijibu zaidi.

"Ulimkubalia?" akauliza.

"Hapana, ila alinipa kadi yake ya biashara kuwa tukirudi nimtafute ikiwezekana nikamtembelee Ulaya au yeye angekuja tena kwa ajili yangu," akaeleza.

"Hongera mwenzetu umejipolea *'Nyanyamkala'* la kizungu, sasa ungewasiliana naye vipi?" akauliza tena. Madam S alikuwa na maswali madogo madogo lakini yaliyoleta tija kwa kazi hiyo. Yule mwanadada akatoa kadi ya kibiashara akampa Madam S.

"Alinipa *card* yake hii hapa," akamwonesha Madam S. akaichukua na kuigeuza geuza, akaitazamisha kwenye kioo kikubwa ambacho kama si mjanja huwezi kujua kama ni kioo, kisha akaigeuza upande wa pili na kuiweka mezani.

Kitendo cha kufanya hivyo, upande wa pili Chiba alielewa, hivyo aliipiga picha ile kadi kutoka upande wa pili na kuingia kumbukumbu zake kwenye kompyuta yake bila

mwenye nayo kujua. Kutoka upande wa pili walipo Chiba na Gina, akaiingiza ile taswira ya kadi katika kompyuta maalum, iliyounganishwa na mtandao wa utambuzi wa kimataifa, akaagiza imletee majibu juu ya namba za simu, picha na maelezo mengine.

Madam S, akamruhusu yule mwanadada akapumzike, Dkt. Jasmini akaingia na kumchukua kisha akampeleka katika chumba chake cha siri.

# 1viii

JOPO lile la watu watatu lilikutana tena mahala palepale, kama kawaida kila mmoja huwa ana njia ya kufika hapo, wakamkuta mkuu ameketi akiwasubiri, lakini alikuwa katika hali tofauti sana.

"Ndio mkuu tumekutana kama ilivyo ada, tupe ripoti yako ulivyotuahidi kisha tujue tunafanya nini," aliuliza mjumbe mweusi.

"Tunahitaji kufanya kazi ya ziada ndugu zangu, kama tetesi zilivyokuwa kwanza lakini sasa nimeanza kuogopa. Vijana wetu wamerudi, mzigo wa Almas umefika tulipoutaka ufike bila tabu, lakini njama imeteguliwa. Wanausalama wao wameweza kugundua kuwa wizi ule haujafanywa na watu wao, na hii inanitisha kwa sababu mpango wetu ulikuwa yule waziri afie mle ndani ili asionekane tena, kwa mtindo huo tungewajengea imani Watanzania kuwa ni waziri aliyefanya hivyo. Sasa wamempata waziri, kambi yetu ya Mwanza imepekuliwa na kila kitu kiko wazi. Hawa jamaa wanataka kupiga hatua ya pili, hatua hii wanataka kuachana na ya nyumbani na

kuwasaka wale makomandoo wetu tuliowatuma. Wakianza kuwachunguza na kufanikiwa kuwagundua, mambo yataharibika," aliwaambia wajumbe walioonekana kupigwa na butwaa la mwaka.

"Yaani kanchi kale kanajifanya kana idara nzuri ya usalama? Tumewashinda CIA kwenye sakata la kuiba *data* pale Langley na mpaka leo wamekili kushindwa, tumewazidi kete KGB na tukapata siri za wanaotafutwa na majasusi hao, nini hao TSA? Ni kuwamaliza tu kabla hatujafanya kazi nyingine. Kama ni kikwazo, lililopo ni kuwapoteza tu, mbona hiyo kazi ni ndogo, kisha Tanzania itajikuta inaamka bila kajasusi hata kamoja," akaongea kwa hasira yule Mwarabu.

"Sawa lakini tunafanyaje?" yule mkuu akawarudishia uamuzi.

"Tupeleke kikosi chetu cha siri, kikawapeleleze kikiwagundua na udhaifu wao basi ni kuutumia na kuwamaliza, wakati wao wanaomboleza, sisi tunamalizana na mtu wetu," yule mweusi akaongea.

*"Good Idea,* maana mpaka sasa hata mtu wetu hajashtuka!*"* mkuu akaitikia. "Sasa naomba kila mmoja kwenye idara yake akahakikishe analifanya hilo, tukutane tena masaa sita yajayo tumalize kazi.

*   *   *

Madam S alishusha kabrasha jembamba mezani kwake, katika ofisi yake ya siri huko 'Shamba'. Alijiridhisha na taarifa zote zilizowekwa na Chiba katika kabrasha hilo juu ya mtu anyeitwa George Mc Field, Komandoo mtoro wa jeshi la Serbia, anayejihusisha na kazi za kukodi kufanya matukio yenye utata kama haya. Alikuja Tanzania mara ya pili akiwa bado ana kumbukumbu juu ya sakata la Mwanamke mwenye Juba Jeusi jinsi alivyoponea chupuchupu dhidi ya mkono wa Kamanda Amata, na mwenyewe alikiri kuwa huyo ni *'Mwanaume wa chuma'*. Kwa jinsi alivyoweza kujibadili kitaalamu akiwa huko kwao, aliamini wazi kuwa hatoweza kugundulika na mahasimu wake ambao walisikitika kuikosa roho yake akiwemo Madam S.

Madam S analikumbuka jina hili, anatabasamu anapogundua kuwa, mtu huyo kajibadilisha sura na muonekano wake lakini kashindwa kujibadilisha mbinu zake. Bomu dogo la misumari lililolipuka kwenye moja ya vyumba vya lile jumba kule Mwanza na kumuumiza mkononi lilimkumbusha bomu lile ambalo lililipuka miaka kadhaa nyuma katika jumba la daktari mmoja huko Keko na kumuumiza Amata. Lilitegwa na Mc Field, hivyo hakuona ajabu kukutana tena na jina hilo.

“Ndege mjanja hunasa katika tundu bovu,” akajisemea huku akilisukuma lile kabrasha pembeni na kulivuta lingine, nalo akalichambua kutazama ndani yake kuna nini. Mauaji tata ya Khumalo mwaka mmoja na nusu uliopita, lakini kabrasha hilo halikukamilika kwani hakukuwa na taarifa za kutosha kutoka Afrika Kusini kama sakata hilo lilipatiwa ufumbuazi au la. Chiba alimaliza kurasa ya mwisho kwa kuweka kiulizo na kishangao, na chini akaweka sentensi moja yenye maneno *‘Khumalo na wizi wa almasi Tanzania,’* Madam S akagonga gonga kidole chake kwenye kabrasha hilo. Hii ilionesha mwanamama huyu anahitaji kujua jambo katika kisa hicho. Alikuwa peke yake ofisini, wakati wengine wote wametawanyika, isipokuwa Dkt. Jasmini ambaye daima alikuwa jirani sana na Madam S mara nyingi. Akainua mkono wake, akacheza na saa yake kisha akaongea maneno fulani, akatulia na kusubiri.

* * *

Simu ya Kamanda Amata ikaita kwa sauti ya chini, akaichomoa mfukoni, akajua tu kuwa ni simu ya kirafiki ambayo haina madhara yoyote. Akaitoa na kutazama, akatabasamu, Naomi.

Kamanda Amata alikwisha msahau mrembo huyu kutokana na kubanwa na majukumu, alipoona jina hilo

likirukaruka kwenye kioo cha simu yake moyo wake ukachanua kwa furaha kama ua la saa sita. Akavuta kumbukumbu za msichana huyo, katibu muhtasi wa ofisi ya mkurugenzi wa mgodi wa Mwadui ambaye sasa ni marehemu, Mc Lean. Akabonyeza kitufe cha kijani na kuiweka jirani naye sio sikioni.

"Za saa hizi *bro*," sauti ya Naomi ikasikika ikiongea kwa chini kidogo kana kwamba anaogopa kufumaniwa.

"Nzuri, unaendeleaje?" Kamanda akamjibu.

"Niko poa! Sasa sikiliza…"

Kamanda kichwa chake kikafunguka mara moja, mrembo huyu anataka kumwambia nini, "Nakusikia, niambie," akamjibu.

"Kuna kitu nimekiokota hapa lakini sijui ni kitu gani, labda wewe unaweza kukitambua, nimekihifadhi," akamwambia Kamanda.

"Kikoje?"

"Sijui nikielezeeje, ni kama kikadi fulani laini kina rangi ya kijani, hiki kitu sijawahi kukiona ofisini, nimekikuta chooni," akaeleza. Kamanda Amata hakuona umaana sana lakini hata hivyo kutokana na kazi yake huwa hatakiwi

kumpuuza hata kipepeo au dondola, kila kitu kwake huwa kina maana na kinahitaji kufanyiwa kazi.

“Ok, usikitupe, kifiche, nitakupigia na kukuelekeza cha kufanya,” Kamanda akajibu na kukata simu. Alijaribu kuvuta taswira kuwa ni kitu gani lakini hakupata jibu la haraka haraka. Akampa Chiba hiyo taarifa, Chiba akamsisitizia Amata kutopuuza hata unyoya wa kuku.

“Kaka fanya juu chini tukipate inawezekana ikawa ni moja ya vitu vitakavyotusaidia,” alimwambia. Kamanda Amata akainua simu na kumpigia Naomi.

“Kesho, hakikisha unafika Mwanza na kuchukua ndege ya mchana kuja Dar, usikiache hicho kikadi maana ninakihitaji kuliko wewe,” akamwambia na kukata simu. Wakati huohuo saa yake ikamfinya kuashiria kuna ujumbe unaingia. Akaruhusu na kuuvuta nje mkanda mdogo wenye ujumbe huo.

…*Wahi kabla pilau halijachacha*…

Akacheka kwa luga hizo za Madam S. Akafunga malngo wa gari na kuuyaacha maegesho ya Uwanja wa ndege, polepole akaondoka zake huku kichwa chake kikichakata hili na lile.

* * *

Dakika arobaini na tano hivi, tayari alikuwa katika ofisi ya siri ya Madam S. mkononi mwake alikuwa na kabrasha alilokuwa akilitupia jicho kuona, nini hicho kisichotakiwa kuchacha. Kamanda Amata akatua kabrasha alilokuwa akilisoma. Akaliweka mezani na kumtazama bosi wake, akatikisa kichwa juu chini.

“Mbona kazi hii inataka kututoa jasho? George Mc Field yupo hapa, tena katika sakata hili? Sasa nimeelewa, nimeelewa nini kinaendelea, tuna kazi nzito sana,” akasema huku akinyanyuka na kulielekea jokofu lililokuwa likibaridisha vinywaji.

“Achana na hilo,” akamwambia, “Nataka uende Afrka kusini nakupa masaa sita tu ya kufanya kazi pale na kurudi, hivyo siku mbili tu uwe hapa kuanzia sasa ninavyoongea,” Madam S akamwambia Amata.

“Madam, hili halijaisha linakuja lingine tena?” akauliza.

“Hapana, ni hilihili, nataka ukafanye uchunguzi juu ya mauaji ya Khumalo, mazingira ya kifo, muuaji ikiwezekana uje na picha ya muuaji kama aliwahi kuonekana au ni shetani, maana hata shetani picha yake ipo, nimemaliza! Hilo ni moja ya kesi hizihizi, na mimi utanikuta hapahapa siondoki mpaka urudi,” akamaliza.

"Sawa Madam, nimekuelewa," akajibu.

Ilikuwa safari ya ghafla lakini ni moja ya kupata majibu ya mambo ambayo yangeweza kutoa mwelekeo wa sakata zima linalosumbua vichwa vya wanausalama hawa. Baada ya saa mbili Kamanda Amata alikuwa angani kuelekea Durban Afrika ya Kusini kama alivyotakiwa kufanya. Akiwa ndegeni kwenye chumba cha V.I.P alikuwa akifikiri wapi pa kuanzia.

*Masaa sita, maana yake sihitaji kulala,* aliwaza bila jibu. Akajiegemeza kitini na kuchukuliwa na kausingizi katamu kalikoambatana na njozi nzurinzuri.

*"Sir ….!"* Usingizi wake ukakatishwa na mwanadada mrembo aliyekuwa na kitoroli kilichosheheni vyakula na vinywaji.

* * *

Mkuu wa nchi, hakuamini kile anachokiona mezani pake. Alikuwa katika ofisi yake ya siri kabisa, ofisi ambayo hata katibu wake hakuwahi kuingia na funguo zake daima alijua yeye anaziweka wapi. Akatikisa kichwa, akauma meno kwa hasira. Kabrasha moja lenye jalada jekundu lilikuwa mkononi mwake likibeba maandishi makubwa ya rangi ya dhahabu *'Rules on How To Be Mr President'*.

Ndani yake mlikuwa na mkataba kati yake na wale waliokubali kumuweka madarakani kwa makubaliano maalumu. Kwa kuwa alishaambiwa kuwa nusu ya mwisho ya utawala wake akabidhi migodi yote mikubwa kwa maswahiba hao au tuwaite wahisani na wafadhili kwa lugha tuliyoizoea. Akajikuta hana la kufanya baada ya kugundua kuwa kipindi cha utawala kinamtupa mkono.

*Kumbe miaka mitano si mingi*! Akawaza huku akikuna kichwa chake pa si na kuwashwa.

Mshtuko mkubwa ulimfika pale alipokutana na sentensi finyu chini ya ukurasa wa mwisho kuwa, 'hatuwezi kufika kurasa ya mwisho bila kutekeleza kurasa inayoitangulia'. Moyo ulimpasuka. Midomo ikamcheza. Akashika pini ya dhahabu na kuifungua kurasa iliyobanwa barabara ambayo hakutakiwa kuifungua kabla. Kurasa yenye pini za dhahabu.

*Umetugeuka kwa kukiuka makubaliano yetu*

*Tutachukua madini na mali nyingine kwa nguvu ili kurudisha gharama ulizotuingiza wakati wa kukupeleka Ikulu.*

*Tutachukua madini kwa jinsi tunayojua sisi, na hata ukijua kuwa ni sisi basi pia ujue kuwa umechelewa, usifanye lolote, bali utulie katika kiti chako, legeza ulinzi ili tufanikishe.*

*Kumbuka mkataba wetu, faida yetu lazima irudi mara tatu ya pesa tuliyowekeza.*

*Mwisho wa mkataba wetu ni huu, ukifungua kurasa hizi tunaondoka na Roho yako*

*Marafiki zako tunaokupenda sana.*

Akashusha pumzi ndefu, mikono ilikuwa ikimtetemeka. *Nimekwisha, kwa nini nilijiingiza huku?* Akawaza na kuwazua, hakuna jibu.

*Tamaa mbaya, tena mbaya sana.* Rais alijikuta katika hali ngumu, mwili ulilowa jasho wakati ofisi hiyo ilijazwa kwa baridi la mashine na kuondoa joto kali la Dar es salaam.

Ndani ya muda mfupi, akajiuliza mengi, akagundua migogoro mingi na vita vya wenyewe kwa wenyewe katika nchi mbalimbali hasa nchi masikini husababishwa na mambo kama haya.

*Matekelezo ya mikataba?* Akajiuliza zaidi. Akaikumbuka Nigeria, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Mali, Afrika ya Kati, Somalia na nchi mbalimbali za Kiafrika zilizoingia kwenye migogoro mizito ya kisiasa, akakumbuka marais waliouawa wakiwa nyadhifani, bado wanakula maisha ya

urais, wali kwa umma na kuku kwa mrija. Akajikuta akili yake ikitengana na ubongo.

Migogoro mingi katika nchi zinazoendelea husababishwa na mabwanyenye kutoka mataifa beberu ya nchi za dunia ya kwanza, ambazo zinataka kuona nani atatawala pale na nani atatawala kule ili wao wapenyeze fikra na tawala zao dhalimu. Bara la Afrika ndilo lililoathirika sana na siasa za mtindo huu. Vita vilitawala kila kona, hakuna aliyejua amani. Kila mtu alijijengea mazingira ya kujilinda yeye na familia yake. Vikundi vya kigaidi viliiibuka kila wakati na kila mahali, jiulize vinapigania nini? Kwa maslahi ya nani, hata wapiganaji wenyewe hawajui na hawana jibu.

Kila kukicha, kule kumelipuliwa, mia wametekwa, hamsini wameuawa. Vyombo vya habari vya mataifa makubwa vinawekeza katika nchi masikini kutengeneza habari mbaya za Afrika. Wanazisababisha wao na wanazitengeneza wao, kisha wanaieleza historia mbaya ya Afrika ilhali wakiiweka mbali ile tukufu. Sisi wenye bara letu hatukumbuki hata kutangaza historia nzuri na ya kupendeza ya Afrika, kwa kuwa tunafanya kila kitu chini yao, basi hata habari za Afrika tunanakili kutoka katika vyombo vyao wenyewe. Hao ndio *King Makers*, ‘nipe madini nikupe bunduki’. Jiue mwenyewe.

*"No! Noooooooooo!"* alipiga kelele bila kujijua akiwa katika ofisi ile, na hakuna aliyesikia kutoka nje, akaanza kuhema kwa nguvu. Ofisi ilikuwa ndogo kama kibiriti, alihisi hatoshi.

*Wataniua*, alijiwazia. A*ibu!* Akajijibu.

*Haiwezekani, nina askari polisi watalinda migodi. Nina wanajeshi watapambana na udhalimu wowote dhidi ya nchi yangu. Nina askari Magereza watawafunga wote watakaoleta shida dhidi ya utawala wangu awe mweusi au mweupe. Nina watu wakakamavu wa Usalama wa Taifa watanilinda kila ninakokwenda hakuna risasi itakayokifikia kichwa changu. Hawaniwezi! Hawaniwezi kabisa! Hapa nitamuweka yule, mgongoni kwangu atakaa yule kule, nitaongeza body guards wangu kutoka wanne wa karibu sasa watakuwa nane wa karibu na kumi na sita watakaotawanyika, nitabadilisha gari la kutembelea, nitaagiza jipya, la kisasa lisilopenya risasi wala kulipuka kwa moto, ah!*

*Lakini wanaotengeneza gari si ni wao wenyewe! Sasa nifanyeje, simwamini mtu, kama waziri wangu katumiwa kuonekana kaiba almasi kumbe ni wao wenyewe waliojigeuza katika maumbo na sura, hawa ni hatari, nifanyeje, nisitoke ndani. Sasa nikialikwa kwenye shughuli za hadhara, itakuwaje, watanidungua.*

*Aaaaaa, ok sasa nakumbuka, walinidungua pale Bunju, lo! Hawakuniua, hawakushindwa kufanya hivyo. kwa nini nimechelewa*

*kujua hili? Nani alitekeleza anayeweza kuupenya usalama wa nchi yangu uliotukuka ndani na nje, atakuwa mtaalam sana huyo. Dereva wangu naye ni mwanajeshi, mpiganaji anayejuwa kuendesha gari katika 'defensive driving', ilikuwaje hakuona kama tunadunguliwa.*

Yote yalikuwa ni mawazo, nafsi ilitapatapa. Akiwa anatazama saa aliyokuwa akiiona mishale yake ikikimbia kuliko kawaida; akiwa ametota kwa jasho, mkuu wa nchi alichanganyikiwa. Yote yalikuja kwa mara moja. Aliona saa ishirini na nne za siku hazitoshi labda mchana uwe na saa sabini na mbili. Hata miezi kumi na mbili ya mwaka aliiona michache sana.

*Aaaaa sasa nakumbuka kitu cha ajabu, hakuwa dereva wangu yule, kweli, nilitaka kumuuliza lakini nilisahau kutokana na ajali. Dereva wangu hana kovu sehemu ya nyuma ya shingo, lakini yule alikuwa na kovu, alipata lini jeraha? Hapana, niliendeshwa na jinni au shetani, aliingiaje, mbona alikuwa na sura na umbo kama dereva wangu? Mh!*

Alihisi kuetetemeka mwili mzima, akafungua tai na kuitupa huko, akalegeza vifungo vya koti na shati lake apate hewa ingawaje mashine ya kufanya hivyo ilikuwa ikiunguruma kwa nguvu zote. Akalifunga lile kabrasha, akalitia kwenye droo, akafunga kwa namba anazojua yeye.

*   *   *

Ndani ya ofisi za wanausalama katika jengo la Ikulu, mlio wa hatari ukasikika. Johnson Cheka, mwanausalama mwenye amri ya mwisho ya kusema Rais afanye hivi au asifanye alikuwa wa kwanza kutoka na kupiga hatua kumi na tano kufika pale kwenye mlango wa kuingia ndani ya makazi ya Rais ambayo yapo katika jengo hili. Akafungua mlango na kuingia haraka, akaufikia mlango wa ofisi hiyo ndogo, akautikisa, umefungwa, akajaribu kuufungua umefungwa, akachomoa funguo zake za ajabu na kufanikiwa kuufungua. Akamkuta Rais amejilaza mezani akivujwa jasho jingi. Mara moja akainua redio yake na kumwita daktari wake, wakafika, na kumchukua mpaka ghorofa ya chini ambako kuna hospitali ndogo yenye kila kitu iliyojengwa maalumu kwa familia ya Rais.

Johnson Cheka alisimama pembeni mwa kitanda akitazama pilikapilika za daktari na muuguzi wake. Dakika tano baadae hali ikatulia. Cheka akamwita mkuu wa Itifaki akamweleza kubadili ratiba zote za Rais. Kwa siku tatu, hakutakiwa kuonana na mtu yeyote, alitakiwa kupumzika. Ilileta mshtuko kwa kila aliyejua, lakini bado ilikuwa ni siri kubwa sana.

Madam S alipata taarifa ya hali ya Rais, hakuweza kuchelewa, siku hiyohiyo alifika Ikulu kumjulia hali Mkuu

wa nchi. Yeye haina tabu kufika anapotaka, alikaribishwa na kuongozwa mpaka aliko Mkuu huyo.

“Nahitaji kufuma upya kikosi cha ulinzi,” ilikuwa ni kauli ambayo ilipenya masikioni mwa Madam S.

“Kwa nini,” Madam akauliza.

“Hali ya kiusalama ni mbaya, kwangu na kwa nchi,” akamweleza.

“Najua, sasa wataka kufanya nini?” Madam akauliza kwa kuwa alijua wazi kuwa kubadilisha au kuimarisha kikosi cha ulinzi au Rais kuwa na wasiwasi na walinzi wake tayari kuna jambo.

“Nitakwambia, maana nikishaweka mambo sawa, wewe utahusika kujua,” Rais akamwambia Madam S.

* * *

Siku mbili baadae, Kamanda Amata aliwasilisha taarifa ya upelelezi wake kwa Madam S na jopo zima la TSA juu ya mauaji na muuaji wa Bwana Gervas Khumalo.

“Sasa tuna nini lingine la kutafuta?,” Madam aliuliza, kisha akaongeza, “ Huyu mwanamke, ndiye huyu tuliletewa picha kutoka Ufaransa. Ndiyo huyu tulichorewa picha na mchoraji wetu baada ya sakata la msafara wa Rais! Hizi hapa

zinafanana kabisa, ni nani mwanamke huyu? Yuko wapi na anataka nini? Hilo ndilo la msingi sasa kuona, siwezi kusema akamatwe au aachwe. Kwanza huyu ni nani?" Madam S akang'aka, alionekana wazi kuwa na hasira siku hiyo. Ukimya ukatawala, hakuna hata aliyekohoa. Kisha Madam akaendelea kuleta utata mwingine, "Sikieni, tena sikieni kwa makini sana, Mkuu wa nchi anataka kufumua kikosi cha usalama na kukipanga upya. Nimemhoji sana kwa nini akanipa siri ifuatayo, siku msafara wake ulipodunguliwa, dereva aliyekuwa akimwendesha Rais hakuwa dereva wake wa kawaida…"

Kamanda akamkatisha, "Unasema! Hakuwa nani…?"

"Hakuwa dereva wake wa kila siku, sasa kama wanausalama wa kumlinda Rais wanashindwa kujua hilo, uko wapi usalama wa nchi? Amenithibitishia hilo," Madam akaeleza na kila mtu akaonekana wazi kuchanganyikiwa kwa jambo hilo.

"Tuna kazi Madam, kazi nzito, hivi sasa inawezekana hata Rais akawa siye tuliyempigia kura au?" Scoba akauliza.

* * *

“Sasa ipo hivi, almasi za Mwadui hazikuibwa na waziri kama ilivyojulikana mwanzo,” Madam S alikuwa akifanya hitimisho la uchunguzi wa taasisi hiyo.

“Sasa ni nani aliyeiba almasi hizo? Mpaka sasa tuna mtu huyu George Mc Field na nina uhakika hajaondoka nchini, na yeye atakuwa ndiye aliyejigeuza kuwa kama waziri, huyu ni Jasusi mwenye uwezo wa kujigeuza hata akawa mjusi,” akaongezea, akawatazama vijana wake, “Sasa tunaingia kazini, asakwe George Mc Field apatikane akiwa anapumua au hapumui, na swahiba zake, wakati huo ufanyike uchunguzi juu ya chanzo cha wizi wa almasi hizi, sote tunaingia kazini, na tutajipanga kama ifuatavyo…”

Kila mtu alibaki kimya, kila mmoja moyoni mwake aliona wazi kuwa haya ni maji mazito mpaka Madam S anahusisha watu wake wote kikazi kwa wakati mmoja, haikuwa kawaida kwa mwanamama huyo. Yeye daima alimpa mtyu mmoja kazi moja labda itokee inahitaji msaada wa karibu ndipo mngekuwa wawili. Lakini hii wote watano na yeye mwenyewe wa sita, kila mmoja aliona kazi ni kubwa na nzito. Baada ya kushusha bilauri yake iliyojaa sharubati murua ya embe akafungua kabrasha lake na kuliacha wazi mezani.

“Hali ya Rais ni mbaya, amepatwa na *pressure* ya kushuka, sasa dawa yake tunayo sisi kuhakikisha utatuzi wa hili umepatikana. Sasa nataka tufanye kazi hii kwa kasi ya ajabu kidogo. Kamanda Amata utakuwa mstari wa mbele kabisa ukisaidiwa karibu na Gina katika mapambano, kila anayenukia harufu ya almasi za wizi, awe mkubwa awe mdogo, toa taarifa tumkamate mara moja, na atakayekataa kutii sheria bila shuruti basi we unajua jinsi ya kumtuliza. Scoba kama kawaida, utakuwa makini katika kuokoa na kukamata anayetakiwa kufanyiwa hivyo. Chiba utahakikisha unawasaidia wote kwa maelekezo ya kielektroniki kama kawaida, nikiwa na maana kuwa ofisi yako sasa itahamia hapa au ndani ya gari lako maalumu kwa kazi hiyo wakati mimi na Jasmini tutakuwa hapa kwa msaada wa haraka…” akiwa hajammializa kusema hayo, mara sauti ya kengele ya simu ya mezani ikawashtua, wakatai anataka kuinyakua akampa ishara Chiba ya kurekodi mwito huo.

*“…Hello…”* akaita

“Hello, kutoka JNIA hapa…”

“Nakusoma,”

“Kuna mzigo hapa umeingia, tuna wasiwasi nao kwa picha mlizotupatia…”

“Ok tuma taarifa zote hapa haraka…” Madam akamwamuru kijana wa Uhamiaji lakini kitengo cha usalama wa Taifa. Kisha akaishusha simu chini na kuirudisha katika kikalio chake, akawageukia vijana.

“Kumekucha…. Kwa umakini wa huyu kijana lazima aliyeingia ana jambo,” Madam akasema.

Wakati wakiendelea na mzungumzo, kompyuta ya Chiba ilikuwa imekwishapokea taarifa kutoka Uwanja wa Ndege, akazifungua na kuprint nakala kadhaa na picha zilizotumwa pamoja nazo. Picha kumi na mbili za mnato zilizomuonesha mwanamke katika mionekano mbalimbali. Kisha kulikuwa na picha ya mjongeo ambayo Chiba aliicheza klwenye kompyuta kubwa ya ofisini kwa Madam S na wote wakaishuhudia. Mwanamke huyo akipita katika ukaguzi, akitoka mlango wa ‘wanaowasili’ akisalimiana na mwenyeji wake, kisha wakiondoka lakini picha hiyo haikuweza kuonesha mtu huyo kaondoka na gari gani.

Kamanda Amata akazitazama zile picha kisha akampatia Chiba. Chiba akaziweka kwenye kifaa chake. Pamoja na zile ambazo Kamanda alizileta kutoka Afrika Kusini, na zile zilizotoka Ufaransa na zilizochorwa katika tukio la Bunju, kisha kwa kutumia kompyuta, softiwea maalumu akazioanisha kama ni mtu mmoja au ni watu

tofauti. Ndani ya dakika kumi walipata jibu alikuwa ni mtu mmoja hata kama alijibadili namna gani. Softiwea hii iliyotengenezwa na Chiba mwenyewe akishirikiana na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam ilikuwa ikifanya kazi kwa ufanisi wa hali ya juu sana, ikikufananisha pua, macho au maziwa kama we ni mwanamke au ndevu kama we ni mwanaume kwa kuwa waliiaminisha kuwa hata mtu ajibadili vipi kuna sehemu hatoweza kujibadili, hivyo ilitafuta sehemu ambayo ilikuwa na unasaba kisha ikaoanisha kutoka hapo.

Baada ya kupata picha kamili ya mwanmke huyo, akaiingiza katika mtandao wa usalama kwanza alianza na ule wa CIA ambao ulimpa jibu lenye utata, akaingiza kwenye mtandao wa MOSSAD kama unamtambua mtu huyo nao ukaleta majibu kama yale yale.

"Shiit!" Kamanda Akang'aka.

Mtandao mwingine wa kijasusi wa KGB, mtandao uliokufa, nao ukaleta majibu yaleyale.

Tracy Tasha, raia wa Marekani, mzaliwa wa Jimbo la Arizona, mwenye miaka thelathini na moja. Maelezo yaliendelea kumwelezea kama muuaji hatari asiyekamatika, anayetafutwa kila kona ya dunia na kila kitengo kiwe cha

kipolisi, kijasusi au mashirika binafsi. Ulimweleza kuwa hakamatiki, mitandao mingine ikampa jina la *The Devil*, wengi walieleza wazi kuwa wamekamata nyayo zake tu lakini mwenyewe hawakumkamata. Mtandao mwingine uliwafanya Madam S na jopo lake kucheka maana ulijitamba kuwa kamera zake za CCTV ndizo zenye uwezo wa kumkamata kila apitapo eneo fulani.

"Tutoe taarifa kwa wadau wanaomtafuta? Maana sisi huyu sio wa kwetu," Madam S akauliza. Kamanda akadakia mara moja, "Hapana, usitoe taarifa kabisa, kwani itakuwa vurugu kubwa hapa, na sisi lazima tumchunguze kwanza kaja kufanya nini, kisha tumuoneshe kuwa sasa kafika mwisho wa maisha yake…" kabla Kamanda hajamaliza kusema hayo Gina akadakia, "Ningemshauri aandike urithi kama ana watoto," wote wakacheka.

* * *

Hoteli ya Land Mark iliupokea ugeni huo. Watu wawili waliopishana miezi miwili hivi kuwasili Tanzania walifikia hapo. Ijapokuwa huyu mwanaume alikuwa anapenda kubadili makazi kila mara. Hawakuwahi kuonana kabla, maelekezo ya bosi wao tu yalitosha kuwatambulisha mmoja kwa mwingine. Ilikuwa ni kama kukabidhiana kijiti kwa wataalamu hawa.

“Kuna shida kidogo, windo letu halijaonekana nje sasa ni siku ya tatu, uchunguzi wetu wa mwisho ulimuonesha akiwa kwenye kasri lake lakini hajaonekana kutoka tena,” Mc Field alimweleza Tracy wakiwa wameketi katika moja ya viti vya sebule kubwa na pana katika hoteli hiyo.

“Kama alitoka usiku je?” Tracy akauliza.

“Hapana watu wetu wako makini sana kumwangalia, kwa sababu unatakiwa umwangamize akiwa anatoka kwenye geti la Ikulu na si pengine popote,” Mc Field alizidi kueleza.

“*No*! Hiyo *point* mbaya sana *Comrade!* Kwenye lango ni pabaya kwa kuwa pana macho mengi,” Tracy akaonesha mashaka, “Siafiki kufanya kazi katika eneo hilo maana kwa vyovyote mtakuwa mmeniweka kwenye domo la mamba au we unaonaje?”

“Mitazamo ni tofauti, mi naona penye macho mengi ndipo penye uzembe wa kuangalia kwani macho hayo hutegeana,” Mc Field akamweleza.

“Ok, lakini mimi kama mimi ningependelea eneo lingiine, eneo ambalo siwezi kufanya makosa kudungua kwani nina shabaha ya ajabu haijawahi kushuhudiwa duniani. Umesahau nilivyomdungua yule muuza dawa za kulevya kule Caracas, jinsi nilivyopenyeza risasi wakati

mlango wa ndege ukifungwa na kumpata barabara; mlango unafunga na yeye huko ndani anakata roho. Huyu mnayenipa leo, hanitoi jasho, hata mngesema palepale ningemuua nilikuwa na shabaha nzuri tu…" akameza mate, "Sasa hapa sio pa kuumiza kichwa kumpata mtu huyo, kwanza nipe muonekano wa eneo lenyewe."

"*Ok*, mwanamke unajiamini sana, lakini ingekuwa mimi ningepatumia hapo, katika geti kuu la kasri hilo la mheshimiwa kuna barabara inayoteremka, kuelekea baharini kukutana na ile ya Ocean, pembeni au mkabala mwa lango hilo ukivuka barabara kuna jengo la wizara kisha chini yake kuna chuo, lakini hilo si eneo salama kwani linaangaliwa kwa kila njia iwe macho mabichi au magumu yote yako hapo. Sasa nyuma ya chuo huku kuna jengo moja refu sana ambalo nilipanda mpaka juu, ni eneo zuri kutekeleza kazi hiyo, kwani ukitumia bunduki kubwa ya kisasa ni sekunde moja tu," Mc Field alimweleza.

"Kutoka huko ghorofani mpaka kufika chini nitaondokaje? Wakizingira chini si nimekwisha," Tracy aliwasiwasika sana kwa hilo.

"Yaani we bado kinda sana, kwani umesahau Yesu aliwatokaje wale jamaa waliotaka kumtupa shimoni kule Nazareti? Alipita katikati yao na wasimwone kisha akaenda

zake, na wewe utapita hapohapo wanapolizingira hilo jengo na hawatakuona." Mc Field alieleza kwa uhakika zaidi.

"Ok, kwa kuwa kazi yako ni kuniokoa naamini litawezekana," Tracy akajibu.

"Sasa sikiliza, kuna jambo moja nataka nikutahadharishe, mimi nilishakuja hapa miaka kumi ilopita kufanya kazi nyingine, nilipata wakati mgumu sana na ile kazi ilishindikana ijapokuwa mimi nilitoroka," akaanza kueleza.

Tracy akajiweka sawa kitini akizitupia nywele zake ndefu mgongoni, akasikiliza kwa makini. Mc Field akatoa picha moja na kumtupia Tracy, akaidaka kwa ustadi na kuitazama. Kijana mmoja jamali katika suti safi nyeusi iliyotanguliwa na shati la buluu, tai safi iliyomkaa vyema shingoni mwake akiwa ameketi kwenye meza moja na kinywaji kikiwa mbele yake.

"Sijajua kama yuko hai au amekufa maana sijaona makeke yake katika hili ila najua kuwa aliachishwa kazi kipindi fulani," Mac Field alieleza.

"Ni nani huyu?" Tracy akasahili.

“Bora ukutane na Israel mtoa roho, huyo mtu ni hatari sana, ni mwiba katika idara ya kijasusi ya Tanzania, hawezekaniki, Ni mkorofi, mpiganaji mwenye weledi uliopita maelezo, mjanja wa maneno na macho ana IQ kubwa ya kucheza na akili yako kisha ni muuaji asiye na huruma anaweza akitoa roho yako na kuifungia kwenye chupa, anaitwa Amata. Wao humwita Kamanda Amata,” akamaliza na kunyanyua kinywaji chake.

Tracy akashusha pumzi ndefu akiigeuza geuza ile picha, “Siwezi kumwogopa huyu! Nikimuona nitapambana naye kwa mikono…”

“Usijaribu ujinga huo!” Mc Field alionya, “Huyo sio binadamu wa kawaida, nahisi ni chuma kilichovalishwa ngozi ya mtu,” kisha wote wakacheka sana.

* * *

Katika kikao cha dharula cha ndani cha usalama, kiliwakutanisha watu wa Usalama wa Taifa tu pamoja na mkuu wa nchi. Lengo kubwa ilikuwa ni kujadili juu ya kuimarisha ulinzi Rais.

“Nahitaji walinzi wa kutosha kwa ajili yangu na hao wote wawe *full* na wawe wapiganaji hodari, ninyi wenyewe mnajua. Hali ya usalama wa Taifa na mimi mwenyewe ni

mbaya sana, nataka mhakikishe kila kwenye mgodi mmeweka macho yenu ili kupeleleza nini kinaendelea maana nahisi wizi huu unaweza ukatokea tena muda wowote…”

Watu wakajiuliza mioyoni juu ya kauli hii aliyoitoa sasa, “Msishngae lakini siko tayari kuona almasi au dhahabu au Tanzanite inaondoka katika njia rahisi kama hii wakati vikosi vya ulinzi na usalama vipo ni aibu, mnakumbuka tukio la Bunju?” wakajibu kwa kutikisa kichwa, “Sasa kila dereva au anayekaa karibu nami mumchunguze kama ni yeye au sanamu, leo nitawaeleza kuwa aliyekuwa ananiendesha siku ile hakuwa dereva wangu, aliyeiba almasi mwadui hakuwa waziri, polisi aliyofuatana nao hawakuwa polisi wetu lakini sura, lugha, muonekano wao ulikuwa ni uleule, sasa mnaweza mkaamka kesho na Rais mwingine hapa, sasa tusiaminine tena,” Mkuu wa Nchi alieleza kwa undani kila kitu kadiri alivyopewa taarifa kutoka TSA na onyo la mwisho juu ya Mwanamke huyo hatari aliyeingia nchini. Waliona baadae kuwa mwanamke huyo na kama kuna wengine wasakwe kimyakimya bila kelele ili kutowagutusha, hali ya tahadhari ikatolewa kwa watu wa idara ya Usalama wa Taifa kuwa makini na kila wanayekuwa na wasiwasi naye. Ulinzi mpya ukaanza kazi mara moja, safu zikapangwa upya, mkuu wa kitengo kile akaondolewa akawekwa huyu. Akatolewa huyu kule akapelekwa kule, huyu na yule

wakapelekwa mikoani, yule wa mkoa ule akaletwa huku ilimradi tu kuiweka safu mpya.

* * *

Saa tatu asubuhi ya siku iliyofuata, Madam S aliingia ofisini kwa kuchelewa kidogo na kumkuta Chiba akiwa anamsubiri.

"Vipi?" ndilo swali lililokuwa jirani kabla ya salamu.

"Nimekuwa nakusubiri sana maana kila simu nikikupigia sikupati, nikaanza kuwa na wasiwasi," Chiba akajibu.

"Ah! Mbona simu zangu zote zilikuwa *on*? Ikawaje hukunipata?" Madam S akatoa simu zake na kuziangalia. Zote zilikuwa sawa, hakuna hata moja ambayo ilionesha hakuna mtandao.

"Shida za mitandao hizi," akamwambia kisha wakaingia ofisini.

"Nipe jipya," Madam S akamwambia huku akivuta kiti chake na kuketi.

"Jipya, ni kuwa sina taarifa yoyote ya Kamanda tangu jana," akamweleza Madam. Taarifa hiyo haikumshtua sana

mwanamama huyo maana alikwishamzoea kijana wake. Alijua atakuwa alikunywa nyingi akabebwa na usingizi mzito.

"Kamanda tuliachana kama saa nne hivi, na tangu hapo hata mimi sikumtafuta," Madam S akajibu, akafikiri jambo kisha akaendelea kusema, "Jana tuliachania pale Motel Agip n ahata gari aliacha pale, mtaa wa pili hivi. Kuna *information* alikuwa anaifanyia kazi, nafikiri atakuwa ameiendea, hebu mtafute kwa simu yake ya kwenye gari". Chiba akajaribu mara kadhaa lakini simu iliishia kuita tu.

"Hayupo garini!" akaeleza.

"Jaribu nyumbani,"

Chiba akajaribu simu za nyumbani, zote hazikupatikana kabisa, "Hakuna *connection* kabisa," akamwambia Madam S.

"Mpigie Gina," akatoa maelekezo. Chiba akampigia Gina akampata, akamwulizia juu ya Kamanda Amata, Gina hakuwa na jibu sawasawa, akamwambia atapita nyumbani kwake Kinondoni akamwone.

# 1ix

KAMANDA AMATA alikuwa kwenye kiti cha chuma, pasi na fahamu. Mikonoye ilifungwa kwa nyuma ilhali miguu yake ilikuwa imefungwa pamoja kwa kuzungushwa nyuma ya miguu ya mbele ya kiti hicho. Hakuwa na jeraha lolote, bali mzima wa afya. Usingizi mzito ndiyo uliomfanya awe mtulivu namna ile huku shingo yake ikiinamia chini. Ndani ya chumba hicho chenye ukubwa wa wastani kulikuwa na vijana watatu. Kwa mwonekano wao tu ungewatambua kuwa ni walinzi wa eneo hilo kuanzia mavazi waliyovaa mpaka silaha walizobeba.

Maagizo waliyopewa ni kutoa taarifa pindi tu mateka huyo atapoamka. Saa nane zilikwishapita tangu Amata alipokutana na masaibu yaliyopelekea kutekwa kirahisi kuliko wakati mwingine wowote.

Akiwa katika kile kiti, Kamanda Amata alihisi baridi kwa mbali sana, fahamu zilizompotea zilianza kumrudi taratibu. Akajitikisa kidogo kupata uhakika kama mwili wake upo sawa. Kitendo kile kikaonwa na mmoja wa wale walinzi.

"Anaamka huyu! Oya… waite jamaa!" yule mlinzi akawapa taarifa wenzake waliokuwa nje. Ijapokuwa alikuwa Amata peke yake katika chumba hicho kama mateka lakini walinzi wa ndani walikuwa watatu waliobeba *Shortgun* za kisasa zilzizoshiba risasi. Nje ya mlango kulikuwa na walinzi wengine wapatao watano nao walikuwa na silaha hizohizo. Kwa jinsi walivyojipanga ilionesha wazi walikuwa na woga. Mara baada ya wale walinzi wan je kupata taarifa hiyo, kila mmoja akajiweka tayari maana walikwishatahadharishwa juu ya mtu huyo aliyeitwa 'hatari'.

* * *

Ilikuwa asubuhi mapema simu ya McField ilipopata uhai. Alipotupa jicho, moja kwa moja alijuwa ni wapi simu ile inatoka na ujumbe gani inaleta. Akajivuta kutoka upande aliolala na kuketi kitandani akiwa ndani ya pajama.

"Nipe habari njema," akamwambia.

*"A-a-ameamka!"* sauti ya upande wa pili ikajibu.

"Mbona unasitasita?" akamuuliza.

*"Amemka huku, fanya haraka uje boss…"*

Mc Field akakata ile simu na kuitazama kana kwamba aliyekuwa anaongea naye alikuwa ndani ya simu hiyo. Kwa

kutumia simu ileile akapiga simu upande mwingine na kuiweka sikioni.

"Tayari, mtu wetu yuko hai twende tukafanye kazi…" akamwambia mtu wa upande wa pili.

*"Ok, tukutane site!"* sauti ya kike kutoka upande ule ikajibu. Akainuka na kuingia maliwato ambako hakuchukua muda mrefu kijiweka sawa.

George McField jasusi bobevu ambaye tangu ameingia nchini alikuwa ameuvaa Uafrika kwa namna yake. Alionekana mzungu lakini mwekundu, aliyepigwa na jua kali la pwani lililomchakaza na kumuaminisha kila amtazamaye kuwa ameishi siku nyingi katika jiji la Dar es salaam. Hiyo ilitokana na kujibadilisha kwa ngozi yake kwa madawa ili kuupoteza uhalisia wa mwonekano wake. McField, Jasusi aliyetafutwa kila kona ya sayari hii alikuwa Tnzania kwa mara nyingine. Alikuwa mahiri katika kutekeleza mikataba mbalimbali; iwe ya kuua, kuiba, kuteka, kutesa na mambo yanayofanana na hayo. Alijishauri mara kadhaa siku alipopewa kazi ya kuja kufanya wizi wa almasi katika mgodi wa Mwadui, lakini kutokana na donge aliloahidiwa alikubali ijapokuwa alijua ugumu wa kazi hiyo.

McField akachagua vijana watatu makini kati ya vijana wake. Akawafundisha Kiswahili, jinsi ya kutembea kama Watanzania. Kwa upande wa mapigano hawaluwa haba, walifuzu vizuri katika Sanaa ya mapigano. Alipojiridhisha nao, akaandaa mkakati makini wa kuiba almasi kwa kujifanya yeye ni waziri wa nishati na madini. Kazi hii kwa Mc Field haikuwa ngumu sana, kwa kuwa yeye alikwishapitia kozi mbalimbali za kijasusi na ukomandoo. Kilichomgharimu sana ni maandalizi ya timu yake ambayo ingemsaidia kufanikisha. Alipojiridhisha, akampa taarifa mteja wake, Sir Robinson Quebec, naye akamwingizia pesa za kutosha na kumtuma Tanzania kichwani mwake akiwa na wazo moja tu 'Makubaliano ni makubaliano, hayatakiwi na hayawezi kugeukwa'.

* * *

Tracy Tasha alisimama mbele ya kioo kikubwa kilichotodha kuijaza taswira yake kikamilifu. Mwili wake ulioshupaa na kulipoteza umbo la uanamke wake ulionekana kwenye kioo hicho. Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa mwanamke huyo kujichukia, misuli iliyojionesha wazi sehemu za mikono na mapaja yake zilimfanya akose hipsi za kumtofautisha na wanaume. Akasonya! Akaviriga nywele zake na kuzifunga kwa nyuma. Suruali ya jinzi ikafuata, kisha

fulana ya buluu iliyombana, juu yake akavalia kikoti cha mpira. Kishapo, akafungua mkebe wake maalumu, wenye vipodozi laghai, akachukua kitu kama kalamu iliyokuwa na rangi inayofanana na ngozi yake. Akakitazama kile kioo na kuanza kujitengeneza uso wake vizuri kwa namna anayoijua yeye. Alipohakikisha yuko tofauti na mwonekano wake halisi, akaongeza stika moja ambayo aliibandika kwenye shavu lake. Stika ile ilitengeneza taswira ya mtu aliyeshonwa jeraha kwa nyuzi saba. Akajiangalia mara nyingine na kuridhika na mwonekano huo. Hakutaka mambo mengi, bastola moja iliyosheheni risasi, akaibana kiunoni, visu vitatu vidogovidgogo akavipachika ndani ya lile koti lake. Akatoka nje ya hoteli na kuingia katika taksi iliyokuwa ikimsubiri,

"Mtaa wa Ally Khan, karibu na Zanaki Sekondari," almwambia dereva kwa Kiswahili cha kutafuta.

"Hongera, kumbe na Kiswahili unajua?" yule dereva akamtania huku akiiacha ile hoteli na kuingiza gari barabarani wakati mteja wake akiwa siti ya nyuma. Tracy hakujibu swali lile, alibaki kimya.

Dakika arobaini na tano ziliwatosha kupambana na foleni na kuingia katika eneo husika. Tracy alimwamuru dereva kusimama karibu kabisa na makaburi ya Ally Khan, nyuma ya Chuo cha ufundi Dar Tech. akamlipa pesa yake na

kuachana na dereva huyo. Taksi ile ilipopotea, akavuka barabara na kufuata uelekeo aliokuwa akienda na taksi. Mwendo kama wa mita mia mbili hivi akapita kwenye geti dogo na kuingia ndani ya wigo ulioizunguka nyumba kubwa ya ghorofa moja. Nyumba ile ya shirika la nyumba la taifa ilikuwa na mabanda upande wa nyuma. Lakini mabanda yale yalikuwa tupu

“Karibu sana,” George Mc Field alimkaribisha Tracy. Wakapeana mikono na kisha wakaingia kwenye moja ya yale mabanda. Ndani ya banda hilo waliloingia, mlikuwa na mlango wa siri. Akaufungua na wote wawili wakaingia na kuzifuata ngazi zilizokuwa zikielekea chini.

* * *

Kamanda Amata alikuwa palepale alipofungwa. Fahamu zilikwishamrudia, lakini bado alijifanya hajaamka sawasawa. Aliweza kusikia kila kitu kilichoendelea. Alimjua anayesubiriwa, naye alitaka kuona kama hao wanaokuja ndio wale anaowahitaji au la. Akajitikisa ili kuona kama kamba zile zimemfunga sawasawa. Naam! Mikononi alishindwa hata kujitikisa, miguuni nako ilikuwa vivyo hivyo. Akatulia na kufumbua jicho moja kwa mbali, akawahesabu wote waliokuwa ndani. Watatu tu. Na wote walikuwa na bunduki mikononi. Punde tu akasikia mlango ukifunguliwa upande

wa juu. Na watu waliokuwa wakiongea kwa lugha ya Kiingereza wakazidi kukaribia sehemu hiyo.

Sekunde chache tu wale watu wakasimama mbele yake. Mara moja akajua kuwa mmoja ni mwanamke na mwingine ni mwanaume si tu kwa sauti zao bali hata harufu zao. McField akatikisa kichwa chake juu chini. Kwa kitendo hicho, kijana mmoja akaweka ksndo bunduki yake. Akakunja mikono ya shati lake. Amata aliyaona yote angali kichwa chini na jicho robo wazi. Kwa alichokifanya kijana yule akajua sasa kumekucha. Yule bwana akasogea mpaka pale kilipo kiti alichofungwa Amata. Akamtazama. Na kisha akamwinua uso wake. Amata akafumbua macho yote mawili, akamwangalia huku akitabasamu. Yule jamaa akasita kidogo, akarudi nyuma kwa theluthi hatua, maana alishaambiwa uhatari wa kiumbe huyo.

"Unamwogopa wakati mtu amefungwa?" McField akauliza. Yule jamaa akajibu kwa kutikisa kicghwa kushoto kulia akimaanisha kukataa. Akaita wenzake wamsaidie. Amata akafunguliwa kamba na kuondolewa kitini. Alipowekwa wima, zile za miguuni zikarudishiwa kisha zile za mikononi zikafungwa kwa nyuma. Wale vijana wakamkamata huku na huku kisha akaanza kushindiliwa makonde mazito tumboni. Amata alikwishajiandaa

kisaikolojia na mwili wake ulikuwa tayari. Yule mpigaji, alipiga na kupiga, jasho likammwagika. Amata aalivumilia kipigo hicho lakini alihisi maumivu makali kwenye misuli ya tumbo lake. Aliguna kila konde lilipotua. Damu zikamtoka kinywani,

“Hahaha haaaaaa, Amata, TSA 1, leo au niseme sasa, umefika mwisho wako… lazima ufe sambamba na yule tunayemtaka au tuliyetumwa kumtoa roho yake,” Mc Field akamwambia huku akimgeuza uso wake uliowiva na kuwa mwekundu. Alihema kwa taabu sana, “U-ta-li-pa, uta-lipa, na-kwa-mbia, ‘Koh! Koh! Koh!’ uta-li-pa,” akaongea kwa tabu. Maumivu makali yalikuwa dhahiri shahiri usoni mwake.

“Nani anayekudanganya hayo?” akamsogelea na kumsukuma kando yule kijana aliyekuwa akimsulubu. “Sikia we fala… kabla hujafa nataka kukupa siri moja nzito ambayo utakufa na hautaweza kuifikisha popote pale,” akatulia kidogo huku akizungukazzunguka, “Na siri hiyo ni kuwa… kesho tunaondoa roho ya mtu mkubwa sana hapa katika taifa lenu,” McField alizidi kutamba wakati Tracy akiwa kasimama kando mikono yake kaifungamanisha kifuani mwake, akitafuna jojo isiyokwisha.

Konde moja zito la McField lilitua katika shavu la Amata. Nguvu ya msukumo wa konde lile ukawapeleka chibi Amata na wale vijana wawili waliomshika. Akiwa pale chini, alihisi taya lake limevunjika. McField aliruka kwa minajiri ya kutua kwenye mbavu za Amata. Amata kwa haraka, akatumia nguvu na kujisukumia upande mwingine. McField akajikuta akiua sakafuni. Akatoa sonyo refu lililojawa gadhabu. "Sikia we Bwege, nimekuja tena nikiwa na hasira mbili, na kazi moja tu!  Nadhani umenielewa… leo hutoona jua la nje. Kibibi chako kinahaha huko duniani kukutafuta na hakitakuona tena," akamweleza..

"U-ta-li-pa, hata uki-ni-ua, yupo nyu-ma mtu atakayekuua kwa kwa niaba yangu, atakutenganisha kichwa na kiwiliwili chako," Amata akaongea kwa uchungu.

"Hahahahahaaaaaa!" McField akaachia cheko la kifedhuli. akacheka sana, "Nani unayemtegemea, huyu hapa au mwingine?" mara mlango mwingine ukafunguliwa. Gina akasukumwa ndani na kuanguka sakafuni. Amata hakuamini anachokiona, alitamanai aruke kumdaka Gina ambaye alianguka vibaya sakafuni lakini hakuweza.

"Tunapotaka kufanya kazi, huwa tumejipanga, wewe na huyu malaya wako wote leo mnaenda kuzimu," McField alijigamba. Amata alikuwa amefura kwa hasira, akimtazama

Gina aliyekuwa chini hajiwezi. Alivyomtazama tu alijua nini kimemkuta mwanamke huyo.

Tracy Tasha akavuta hatua na kumsogelea Gina. Hakusimama mbali, mota moja kutoka pale alipoangukia. Akamtazama Amata na kutabasamu kisha akampiga teke sawia lililotua usoni. Gina akaanguka upande wa pili na pua yake ikaanza kuvuja damu kwa fujo.  Mguu wa Tracy ulienda juu na kubaki hewani kwa sekunde kadhaa kabla hajaushusha chini kwa maringo. Macho yake yalikuwa kwa Amata. Alipoushusha, akatembea kilimbwende na kumwendea Amata.

"Huyu ndiye ulienipa vitisho juu yake?" akamuuliza McField. "Eti Kamanda! Unajiita  Kamanda? Makamanda wametulizwa kwa mkono huu," akaupunga mkono wake hewani huku akimtazama McField. "Hakuna mwanaume wa chuma wala nini, hapa ni utepetevu tu," akamalizia kisha akarudi alipokuwa. McField alitabasamu huku akitikisa kichwa chake juu chini, akimwangalia mwanamke huyu anayetembea kwa madaha; mrembo wa sura na mzuri wa shepu, lakini mwenye roho iliyojaa kutu.

"Amata Ric, TSA 1, una la kusema? Sasa ni saa saba inaenda saa nane, muda wetu unayoyoma. Huyu mwanamke unayemwona anaitwa Tracy Tasha, ndiye atakayekuua wewe

usiku wa leo kwa kukukata kichwa chako," MacField akamwambia Amata.

"Hata kama! La-ki-ni, kwa-nza nitaku-u-ua we-we," akimaanisha McField, "Pili we-we mwana-m-ke utakiona chamtema kuni…," Sauti ya Amata ilitoka kwa tabu lakini ilionesha kujawa na hasira.. Mc Field na Tracy wakatoka ndani ya chumba kile huku wakiacha maagizo ya watu hao kushughulikiwa ipasavyo.

* * *

Ilikuwa vigumu sana kwa Madam S kuamini kuwa Kamanda na Gina wametekwa. *Amempataje kirahisi hivyo?* Alijiuliza bila ya kupata jibu. kila mara alikuwa akimwita Chiba ofisini na kumwambia hili au lile, alionekana wazi amechanganyikiwa. Chiba alijaribu kumtafuta *senior* wake kwa simu zake zote lakini hakupatikana. Kila alipoangalia mtandao wake, ulimwonesha kuwa mara ya mwisho Amata alikuwa Upanga, katika Cassino Las Vegas.

*Wameniweza!* Alijiambia moyoni.

"Scoba!" akaiita. Scoba akageuka kumtazama Chiba. "Harakati lazima ziendelee kaka! Hatujui Gina na Kamanda wako wapi mpaka sasa, na wala wako katika hali gani, hivyo tufanye juu chini kupata jibu," Chiba TSA 2 ilikuwa ni nafasi

yake sasa kutoa majukumu. "Iendee gari ya Amata pale Motel Agip, kuna *information* inayoweza kutusaidia," akamwambia Scoba.

"Sawa! Kuna lingine?"

"Hakuna, nasubiri jibu… jua kabla halijawa la utosi tuwe tumeikamilisha kazi hii,"

"Sawa!" Scoba akaiacha ofisi hiyo ya siri na kuondoka. Kama alivyoelekezwa. Nje ya Motel Agip gari la Amata lilikuwa maegeshoni. Scoba kwa tahadhari ya hali ya juu sana akaliendea. Hakuhitaji kuliendesha, moja kwa moja aliifungua droo iliyokuwa imefungwa kwa kifungo maalum. Akachukua anachotaka. Alipogeuka tu na kuondoka, nyuma yake mlipuko mkubwa ukatokea, lile gari likateketea vibaya. Watu wakakimbia huku na huko, mtaa mzima ulikuwa ni hekaheka kila mtu alitaka kunusuru gari na maisha yake. Scoba, ni kama alilitegemea hilo, maana hakugeuka hata nyuma. Na pindi mtaa ule ulipogubikwa na hekaheka, yeye akatumia nafasi hiyo kutoweka eneo hilo.

* * *

"Pole Scoba!" Daktari Jasmini alikuwa akimwambia Scoba.

“Nililitegemea jambo lile kutokana na mifumo ya magari yetu,” akamjibu Jasmini huku akimpatia kifaa kidogo alichokitoa kwenye gari lile, “Mpe Chiba ashughulike nacho,” akamwambia. Jasmine alikipokea na kumuacha Scoba pale alipoketi na kuingia chumba kingine ambacho Chiba alikuwapo.

Kilikuwa kinasa sauti kidogo kilichofichwa katika gari la Amata. Chiba alikichukua na kukiunganisha na mitambo yake, kisha akafuatilia mazungumzo yaliyokuwa humo kwa makini. Kupitia mazungumzo yaliyonaswa na kifaa hicho, Chiba aligundua kuwa Amata alitekwa kadiri ya mtu aliyekuwa akiongea na simu katika chumba cha moteli hiyo. Aliendelea kufuatilia mazunguzmao hayo lakini hakujua kabisa ni wapi watakuwa wamemficha swahiba wao. Chiba aliwaita wengine na jambo hilo likajadiliwa katika umoja wao. Vichwa viliuma!

“Tutapajuaje? Kumbuka Mc Field anamjua vizuri sana Amata, hawezi kumpa nafasi zaidi ya kumuua tu. Ndiyo! Amata anaweza kujiokoa lakini ni kazi ngumu sana kwa mtu kama Mc Field ambaye anaujua uwezo wa adui yake… mtu kama yule hawezi kurudia kosa,” Madam S aliwaambia vijana wake. Majadiliano yalikuwa mazito, Amata alitafutwa mawazoni mwa TSA waliokuwa katika chumba hicho.

“Sawa! Madam… najua cha kufanya ila kwanza… tuandae Kikosi cha Ukombozi,” Chiba alitoa ushauri.

“Kikosi cha ukombozi?” Madam akarudia kauli ile. “Sawa, wewe mwenyewe na Scoba mtafanya kazi hiyo… hakikisheni inazaa matunda,” akampa maagizo. Kabla hajatoka katika ofisi ile, akamsogelea Chiba na kumwambia, “Ukikutana na Mc Field usijipime kupambana naye, tumia silaha, mmalize”.

Mara tu baada ya mwanamama yule kuiacha ofisi ile. Chiba, Scoba na Jasmine wakatazamana.

“Kazi kwenu vijana!” Jasmine akawaambia huku nay eye akisimama tayari kukiacha kile chumba. “Uwe tayari kwa lolote…” Chiba akamwambia.

“Bila shaka boss!” akajibu. Chiba akairekodi ile sauti kutoka kwenye kile kifaa kwenda kwenye kompyuta yake. Alipohakikisha iko sawa, akainua simu na kuwasiliana na rafiki yake wa karibu sana katika moja mitandao maarufu ya simu. Akampa kazi ya kutafuta watu hao walikuwa wakiongea wapi na wapi.

Dakika tano baadae alipewa taarifa kuwa mmoja alikuwa eneo la katikati ya jiji, maana mnara uliosoma ulikuwa ni ule wa jirani na jengo la Kitega Uchumi la NIC,

na mtu wa pili alionekana kuwa mitaa ya Shule ya Sekondari Zanaki kwani mnara uliomsoma ni ule wa jirani na shule hiyo. Baada ya maswali mawili matatu, Chiba alijiridhisha na maelezo hayo. Kisha akamwomba mtu huyo amwambie namba hizo kwa muda huo zinasoma wapi ili waweze kuwafuatilia watu hao. Jibu alilopata ni kuwa moja ya namba hizo ilikuwa imezimwa lakini nyingine bado ilionekana ipo mitaa hiyo ya Upanga, Mtaa wa Aly Khan karibu na shule ileile.

*Kazi imeisha!* Chiba akawazxa huku akiitazama saa yake

"Scoba, upo? Tunaweza kuingia kazini?" Chiba akamwuliza. Scoba akaitikia kwa kichwa kuashiria kuwa yuko tayari kwa kazi. "Haya twende mgodini," akamwambia akimaanisha kwenda kwenye chumba cha silaha. Wakatoka pamoja na kuelekea kwenye chumba hicho na kuchagua silaha walizoona zitafaa kwa operesheni hiyo.

"Vipi mbona mnapakua?" Madam akauliza mara baada ya kuwaona kupitia kamera za siri na kuwafuata.

"Tunaenda kupambana na jeshi, *so* lazima tujiweke kamili," Chiba akajibu. Scoba akachagua *Short Gun double barell*, akaijaza risasi. Ikashiba. Bastola mbili aina ya PK 380 akazitia kibindoni. Chiba akatazama huku na kule akatwaa

mashine hatari ya *Heckler and Koch UMP*, akaitia begani na nyingine ndogo ndogo kama visu, kamba za plastiki na kadhalika. Walipohakikisha wapo sawa, wakatoka na kuvitia garini. Ladrover Defender likawa tayari kwa safari kuelekea Upanga.

# 1x

KAMANDA AMATA alikuwa mdhoofu sana baada ya kipigo na mateso makali aliyoyapata kutoka kwa Mc Field na yule mwanamke. Majeraha ya hapa na pale yaliyokuwa yakivuda damu yaliupamba mwili wake. Gina alikuwa pembeni, hajiwezi.

“Sasa kinachofuata ni kumbaka huyu malaya wako huku wewe ukiangalia,” mmoja wale jamaa akamwambia Amata. Yule jamaa akamwendea Gina na kuanza kumfungua suruali aliyokuwa amevaa, huku wenzake wakishangilia na kupiga picha za video. Kitendo kile kilimuuzi sana Amata.  Kikampa hasira ambayo ilirudisha nguvu za ziada mwilini mwake. Mmoja wa wale vijana akamsogele Amata na kumwambia kwa dhihaka huku akimshika kidevu na kumgeuza sura kule walikokuwa wakifanya kile kitendo, “Usijifanye huoni, mpumbavu wewe, angalia huku tunachomfanya malaya wako hahahahaaaa… kisha picha zote tunapeleka kwa wakubwa zako,”.

Ni sekunde au nukta hiyo aliyokuwa akiisubiri kwa hamu. Amata aligeuka ghafla na kudaka kidole cha yule

jamaa kwa meno. Akamuuma na kukikata kisha akakitema chini.

“Aiyaaaaa! Ananing’ata!” yule mjinga akapiga unyende wa uchungu. Swahiba zake wakagutuka na kusogea kumsaidia. Kosa! Alichokifanya Amata hakikutegemewa na wote. Alijirusha akiwa na kamba miguuni na mikononi. Akajikunja mithili ya samaki na kisha miguu yake akaipitisha katikati ya mikono yake na kutua tena sakafuni. Mara hii mikono yake ikiwa mbele. Akashindwa kustahimili na kuanguka. Jambo lote hilo lilitukia kwa sekunde mbili tu kama si tatu. Akajibiringisha na kuifikia nguzo iliyosimikwa kushikia jengo hilo. Akaitumia kujiinua na kuketi. Wale jamaa wakatawanyika kwa woga na kurudi nyuma.

Harakaharaka akashika ile kamba ya miguuni na kuifungua haikumpa tabu aliivuta tu ikalegea. Kabla hajamaliza, alipokea teke kali lililotua upande wa nyuma wa shingo yake. Mwingine aliyekuwa upande wa mbele, akasogea kwa kasi na kurusha teke ambalo lingetua usoni au kifuani kama shabaha yake ingekuwa sawa. Lakini Amata akalizuia kwa mikono yake iliyokuwa ingali bado kambani. Akaunasa ule mguu na kuubana vizuri kisha akauzungusha kwa nguvu na kusikia viungo vya mifupa yake vikiachana. Lakini bado yule jamaa alikuwa kasimama wima huku

kakunja sura kwa maumivu. Wakati tayari, kamba iliyofunga miguu ya Amata ikiwa kando, akazungusha mguu mmoja kwa kasi na kumchota mtama yule jamaa na kumbwaga chini kama mzigo. Ukelele aliyoutoa uliwafanya wale wengine kutegeana nani asogee na nani abaki. Amata akajikuta mtu kati. Hakujali kwani hiyo ilikuwa ni taaluma yake, kwa kasi ya umeme, akajiinua haraka na kuruka samasoti. Tayari alikwisha mwona mmoja wao aliyekuwa akitaka kuitumia bastola yake. Zile risasi zikachimba chini na nyingine kwenye nguzo wakati yeye akitua chini na wawili kati yao. Wote pamoja wakaenda chini. Akajiviringa kwa ufundi na kuliacha eneo lile. Akajificha nyuma ya shubaka kubwa la chuma. Nalo likamkinga dhidi ya adui zake.

"Oya, akitoroka huyo, tumekwisha!" Sauti ya mmoja ikasikika.

"Hatoki mtu hapa, mzungukeni," mwingine akatoa amri.

"We Chulubi! Hakikisha huyo mwanamke umemfungia ndani, tushughulike na huyu mbwa koko kwanza," maneno hayo yalimtia hasira Amata maradufu. Akaiondoa kamba mikononi mwake kwa kutumia meno. Akatulia kwa sekunde kadhaa na kisha ghafla akalisukuma lile shubaka tupu na kulifuata nyuma yake huku akizunguka nalo kupoteza

shababa ya risasi zilizokuwa zikipigwa ovyo. Lengo lake lilikuwa sahihi kabisa, alipofika mwisho wa chumba kile alimbamiza mmoja wao na lile shubaka. Yule jamaa akatoa mguno wa uchungu na bunfuki ikimtoka mikononi. Amata akaliacha lile shubaka na kuruka kiufundi mpaka ilipo ile AK 47 na kuinyakua. Akajiviringa na kujiweka sawa huku tayari akiruhusu risasi kadhaa zifanye kazi. Alipotulia, tayari wawili walikuwa chini wakigalagala kupigania roho zao.

"Uwiiiiii! Mi nilisema! Nilisema mimi!" mtu mmoja akapiga kelele huku akikimbia kupanda ngazi za kutokea nje. Hakumaliza hata ngazi ya kwanza, rakarudishwa ndani kwa risasi zilizopigwa mfululizo. Akajibwaga chali katika sakafu ghafi huku macho yamemtoka. Mipigo ile ya risasi ikamfanya awe macho kwani alitambuani nini kimetokea. Alipotazama juu, uelekeo wa ile ngazi akaona vivuli vya watu vikiteremka upande alipo. Tayari ukumbi ule alibaki yeye na marehemu watatu, huku watu wengine wawili wakiwa wametoweka eneo lile. Akajibanza nyuma ya nguzo akiwa anatweta ili kuzihakiki hisia zake kama zi sahihi au la.

"Amata!" sauti ikaita.

"Chiba!" Akajibu huku akishusha bunduki yake na kutoka nyuma ya ile nguzo. Hakumaliza hata hatua mbili,

alihisi kitu cha moto kikipita sehemu ya juu ya katika mkono wake.

"Aaaaiigh!" Amata akapiga yowe la uchungu na kujibwaga chini. Ilikuwa risasi iliyopigwa kutoka nyuma na mtu mmoja ambaye hakuonekana sawasawa pale alipojificha. Amata akageuka pale chini akiwa na maumivu. Akaiweka bunduki yake sawa lakini kabla hajafanya lolote, yule jamaa alipiga yowe moja tu na kuanguka chini kama mzigo. Risasi moja ilifumua kichwa chake na kumbadili jina mtu huyo.

Alipogeuka upande wa mbele alikuta bastola ya Scoba ikiwa bado imekamatwa barabara mkononi mwake.

"Asante Scoba. Gina hali yake ni mbaya, tumsaidie," akawaambia. Chiba akashusha bunduki yake na kuitupia mgongoni huku bastola yake akiichomeka sawia kiunoni. "Scoba tupe ulinzi!" Chiba akasema huku akivuta hatua kumwelekea Amata.

"Tufanye haraka kabla mambo hayajaharibika," Chiba alieleza. Pamoja na jeraha mkononi mwake, Amata alijitahidi kumsaidia Chiba kumbeba Gina mabegani mwake.

"Assss!" Amata akalalama kwa maumivu. "Pole Kamanda jikaze, najua una maumivu makali…" Chiba

akamwambia Amata huku wakiongoza njia kutoka nje. Amata alijitahidi kudhibiti damu zilizokuwa zikimvuja kwenye nyama ya mkono iliyochanwa vibaya na ile risasi.

Scoba alikuwa wa mwisho kutoka katika ile nyumba pale Upanga, alihakikisha usalama kwa watu hao watatu. Wakaliendea gari na kuingia ndani, wakatulia kwanza wakilifunga jeraha la Amata. Chiba akamwacha Scoba akiendelea na kazi hiyo, yeye akachukua kitenza mbali na kubofya hapa na pale. Mlipuko mkubwa ukatokea kwenye ile nyumba, Chiba akatia moto injini na kuliondoa lile gari eneo hilo na kuacha kelele za wafanya biashara zikiita 'Majambazi! Majambaz!'

* * *

Dakika ishirini na tano zilizofuata, tayari waliwasili katika kliniki ndogo ya Jabal Al - Hiraa, Amata na Gina waliwekwa vyumba tofauti kwa ajili ya matibabu. Kliniki hii iliyojengwa eneo la Changanyikeni, jirani kabisa na kambi ya jeshi ilikuwa ikimilikiwa na Daktari Jasmini. Palikuwa na wafanyakazi wachache upande wa uuguzi na matabibu.

"Pole sana TSA1," Jasmini akamwambia huku akisogeza kando chano iliyojaa vifaa tiba na dawa kadhaa.

“Asante dokta…” akajibu, “Vipi Gina anaendeleaje?” akauliza.

“Anaendelea vyema, yupo amepumzika…” akamjibu. Amata akaitika kwa kichwa na kujiinua kuketi kitandani hapo. Mkono wake ulikuwa umeshonwa na kufungwa kwa bandeji nyepesi. Kitanda chake kilizungukwa na Chiba, Scoba na Jasmini. “Utapona, usijali…” Chiba alisema.

“Ndani ya saa ishirini nan ne, lazima watu hawa wawe mikononi mwetu ama marehemu au wazima,” Amata akaongea kwa hasira. “Hawawezi kutawala namna hii na kujifanyia wanachotaka,” akaongeza kusema.

“Kamanda, wewe upumzike, tutafanya kazi ya kuwanasa sisi tuliobaki,” Chiba alimwambia.

“Hapana! Nasema hapana…” akafinya sura yake kwa uchungu na kuifinyua, “Nichome ganzi tafadhali, nataka kuingia katika mapambano, ama zao ama zangu,” akasema. Daktari Jasmini alikuwa akimuelewa vyema TSA 1, alimjua fika kuwa kazi akitaka kuimaliza lazima aimalize. Hakuwa na hiana, “Unajiamini? Unaweza? Kwa nini usikae walau siku mbili Zaidi kisha tuingie sote kazini,” akamwambia.

“No! tukichelewa Zaidi ya saa kumi na mbili nchi hii itakuwa imeshavurugwa na washenzi hawa. Lazima

tuaharakishe!" Amata akamwambia Jasmini. Mlango wa chumba hicho ukafunguliwa na Madam S akajitoma ndani. Wote wakasimama kwa utii kabisa kuonesha heshima na nidhamu kwa bosi wao. Madam S akasimama mbele ya kitanda cha Amata aliyekuwa sasa ameketi, upande wa miguuni. Uso wa mwanamke huyo ulikuwa makini. Ulikuwa umebeba jambo zito kichwani mwake. Hakumtazama Amata kwa kumwonea huruma bali kwa kutoa oda ya kazi. Chiba Jasmin na Scoba wakatoka nje ya chumba kile kufuatia ishara waliyopewa na HOT. Chumbani mule akabaki Amata na *Spy Master* wake tu.

"Kamanda," akaita kwa sauti ya mamlaka.

"*Yes* Madam!" akaitika.

"Unajisikiaje sasa?"

"Najisikia hasira," akajibu huku akigeuka upande huu na huu kuunyoosha mwili wake.

"Upumzike," akamsihi.

"*No!* Hiyo haipo kwenye kamusi yangu. Kumbuka adui ataona kambi yake imefumuliwa je atakaa hapa? Nikipumzika je; mpaka nipate nguvu tayari atakua London, au hata Moscow…" Kamanda akaeleza. Madam S akajifuta

uso wake kwa kiganja cha mkono. Akashusha pumzi na kumtazama TSA 1. Amata akateremka kutoka pale kitandani na kusimama na Madam S kwa mtindo wa kutazamana.

"Sikia Madam… naongea kwa sauti ya chini. Kuna mkakati mzito unaoendelea, hawa jamaa wametumwa kuondoa roho ya Mkuu wa nchi, *that is it!*" akamtazama Madam.

"Ndiyo, lakini hatujajua kwa nini mpaka sasa wanataka kutekeleza hilo," Madam akamjibu. Akatulia kama sekunde kumi na saba hivi, kisha akamwambia Amata, "Keti Kamanda". Amata akafanya hivyo.

"Hii ni kitu nzito Kamanda, ni ya siri na ni nzito sana. Lazima ishughulikiwe kikamilifu. Kwanza tushughulike na hawa waliokuja, tukiwatia mkononi, wao sasa watatuambia nani na nani ndio matajiri wao, hao sasa tutawafanyia kazi baadae na kwa siri vilevile," Madam akamwambia Kamanda.

"Ndio, lazima tukate mpaka shina sio matawi tu," Kamanda akaongeza, "Mkuu wan chi anaendeleaje na afya yake?"

"Alipata mshtuko, sasa yupo sawa, na kesho ataongea na waandishi wa habari asubuhi saa nne palepale Ikulu, kuhusu hali halisi ya yaliyotokea; moja la kudunguliwa

msafara wake na pili la kuibwa kwa almasi," Madam akamjibu.

"Hapana, sio wakati sahihi wa kufanya hivyo… Mheshimiwa hasijitokeze hadharani". Madam S akajaribu kuimumunya kauli hiyo ya Amata akaona ina uzito fulani.

"Kwanini?" akauliza kwa minajiri ya kutaka kuhakiki mawazo yake.

"Kuna uwezekano wa kujisababishia kifo chake,"

"Amata, nimemwambia hayo, lakini inaonekana kuna kitu anaficha, sasa hii ni hatari kwa usalama wa nchi. Sisi tunamlinda, tupo kwa ajili ya usalama wake na taifa kwa ujumla, wakati mwingine inabidi atusikilize," akatulia kidogo kama anayefikiri jambo. Kisha akaendelea, "Ila safari hii amelazimisha kuongea na waandishi".

"Nimekuelewa, wacha iwe!" akarudi na kuketi pale kitandani huku akimwacha bosi wake angali wima.

"So?" Madam akauliza.

"Naondoka, naingia msambweni…"

"Hali yako inaruhusu?"

"Daktari amesema haina shida…"

“Uwe mwangalifu… bado nakuhitaji,” Madam akamwambia. Kamanda akainuka kutoka pale kitandani. Akajiweka sawa na kisha kuuelekea mlango na kutoka nje. Pale nje kulikuwa na gari la Madam S pamoja na lile walilotumia kikosi cha wokovu.

“Utaendaje? Na unaenda wapi?” sauti ikauliza kutoka nyuma yake.

“Nachukua taksi, ninakoenda hustahili kupajua sasa ila baadae…” akamjibu Jasmini aliyekuwa amesimama ngazini. Wakaagana. Amata akatoka nje lango la ile kliniki ya Jabal Hira na kuziendea taksi zilizokuwa ng’ambo ya barabara. Akaingia kwenye mojawapo na kumtaka dereva amfikishe Mwenge. Yule dreva hakuwa na maswali, akatia injini moto na kufanya alivyotakiwa. Pale Mwenge, Amata akachukua taksi nyingine iliyomfikisha Mbuyuni. Hapo akateremka na kuvuka barabara. Akapotelea mitaani.

* * *

Dakika kumi na tano za kutembea zilimfikisha nyumbani kwake, eneo la Kinondoni. Alipofungua mlango mdogo wa chuma na kuufikia ule wa kuingia ndani, akasita kidogo. Akayakagua kwa macho mazingira yale ya barazani. Hisia yake ikamwambia kuwa nyumba yake imepekuliwa au

imevamiwa. Sifa kubwa ya jasusi yoyote yule ni kutii hisia yake, yaani mlango wa sita wa fahamu. Hakuwa na silaha yoyote Zaidi ya mikono na miguu yake. Haikumuumiza kichwa kwani mapambano ya ana kwa ana kwake ilikuwa kama uji na mgonjwa. Akafungua mlango taratibu na kuingia ndani kwa kunyata. Hakutaka kabisa kusikika kama kungekuwa na mtu ndani ya nyumba hiyo. Kila alipopatazama palipekuliwa, na mpekuzi huyo alikuwa rafu kwani alitupa vitu huku na kule.

*Alikuwa akitafuta nini?* Akajiuliza. Pamoja na yote hayo, ndani mule hakukuwa na dalili yoyote ya mtu. Akakiendea chumba chake na kukifungua. Hali ni ileile, kila kitu shaghala baghala. Hapo akapata hisia tofauti si ya kupekuliwa tena ila kulikuwa na aina fulani ya purukushani. Akavuta hatua na kuelekea kwenye hazina yake, anapohifadhi zana za kazi na kabrasha zake muhimu. Haikuwa rahisi kwa mtu yeyote kuigundua hazina hiyo iliyofichwa kwa picha kubwa ya nguva, samaki mtu. Akabofya jicho la kushoto la mwanamke huyo mwenye umbo la juu binadamu na chini samaki. Ile picha ikateremka taratibu na kuacha kitu kama kisanduku cheusi chenye tarakimu kadhaa juu yake. Akabonyeza tarakimu hizo na mahala hapo pakafunguka. Akapiga jicho ndani ya kisanduku hicho, akaridhika, kila kitu kipo sawa. Akapaacha

na kwenda kwenye chumba chake cha siri ambako huficha mtambo wake mdogo unaoongoza kamera zote za siri ndani nan je ya nyumba hiyo zilivyofungwa kwenye kona tofauti. Akafungua mlango na kujifungia ndani, kimya.

Ni chumba kidogo ambacho mlango wake kwa upande wa nje ni kabati lililoja viatu na makorokoro yasiyo na maana, lakini kwa ndani kulikuwa na vitu vya maana sana. Akawasha kompyuta ndogo iliyo mezani. Akarudisha nyuma matukio mpaka alipoona tukio lililotukia, akaanza kutazama.

Kwanza aliona mlango mkubwa wa mbele ukifunguliwa, vijana watatu wanaingia ndani ya sebule hiyo, kisha wanaanza kuipekuwa huku na kule, wanadondosha hiki na kile. Wanapoona hakuna cha maana wanaamua kuondoka zao. Kamera zinaonesha saa moja na nusu baadae Gina anaingia na kusimama mlangoni anaangalia ile vurugu iliyokuwa hapo sebuleni, anamwita Amata mara kadhaa. Anaiacha sebule hiyo na kukiendea chumba cha Amata huku akiendelea kuita.

Hapo Kamanda akajua, bila shaka Gina alikamatiwa hapo nyumbani kwake. Mara anaona kupitia kamera namba moja mlango unafunguliwa na vijana walewale watatu wanaingia na kumvamia Gina kule chumbani. Kupitia kamera namba nne anashuhudia mapigano makali kati ya

Gina na vijana hao. Kwenye picha hiyo anaona mwanamke huyo anapigwa na kitu kizito kichwani baada ya kuwazidi nguvu vijana wale. Anazirai. Kisha wale vijana wanambeba na kuondoka naye.

Kamanda Amata akashusha pumzi ndefu. Akainuka na kutoka ndani ya kile chumba na kuingia chumbani mwake. Akachukua muda kuoga kisha akajilaza kwa dakika kadhaa akisubiri muda mwafaka wa kuanza kazi yake. Wapi aanzie? Ndilo swali lililokuwa likizunguka kichwani mwake.

*Motel Agip! Nilipoishia ndipo nitapoanzia!* Akapata jibu kichwani mwake. Akajianda kwa mavazi ya kazi, akachukua silaha zake muhimu na kuzitia kwenye kona mbalimbali za mavazi hayo, kisha bastola moja akaitupa kitandani na kuilalia kwa mgongo, yeye akiwa chali. Giza liliposhika hatamu, akaingia kazini.

* * *

Saa sita na dakika ishirini na tatu za usiku, Kamanda Amata aliwasili katika jumba la starehe la Bilicanas lililopo katikati ya jiji la Dar es salaam. Watu walijazana kila kona wakila starehe na kuyatumbua maisha. *Bilicanas and Casino*, au kama lilivyojulikana zamani, *Mbowe Club* lilibeba kila aina ya watu ndani yake. Wavulana kwa wasichana wa kileo

walitumbua maisha, pia walikuwemo wazee watu wazima ambao haya yalikuwa maisha yao; waliokuja kufanya biashara zao *nyeusi*, walikuwemo, wanaocheza disco twende, wanaovuta sigara au bangi sawa tu. Wanaouza miili wakiwa nusu uchi kila kona walikuwa wakijivinjari kutega mawindo yao. Achana na wale waliokuwa kwenye michezo mbalimbali ya kamali na kadhalika. Hapa ndio palikuwa mahala pa kila uovu, wapo waliokuwa wakipanga mbinu za kuvunja, kutia na kutoa mimba na kila jambo lilizungumziwa humo.

Akiwa ndani ya suruali yake ya kadeti nyeusi, fulana nyeusi na kizibao cheusi cha jinzi kilichokuwa juu ambacho ndani yake kilisheheni zana za kijasusi za kuua na kutoa pumzi za waja wa Mola. Kwenye miguu yake usawa wa soksi alibana bastola mbili, moja huku na nyingine kule. Hata zake zilimfikisha kwenye moja ya kaunta nyingi zilizo ndani yanjumba hilo. Akapanda juu ya kiti kimoja kirefu, kati ya viti vingi vilivyokuwa hapo mbele ya kaunta hiyo kubwa ya kisasa. Jicho lake likabarizi kushoto na kulia. Kila mmoja alikuwa na kinywaji kizito mkononi mwake, ama akinywa yeye au akimnywesha binti aliyekuwa naye hapo, kisha wangepigana mabusu ya mahaba; mahaba ya pombe. Amata akaichukua miwani yake na kuivaa. Miwani inayoweza kukuonesha kila kitu cha chuma kilichowekwa kwenye mwili

wa binadamu. Akawatazama kwa tuo wote walioketi eneo hilo. Akawaona jinsi walivyo safi, hakuna mwenye mawaa yoyote zaidi ya funguo za magari mifukoni au sarafu za mia mia na mia mbilimbili. Akatabasamu, kisha akaishusha miwani yake na kuiweka kwenye mfuko wa kile kizibao. Akaweka vizuri pama lake lililokunjwa huku na kule kama Marlboro. Ndevu alizozijaza kidevuni mwake zilimfanya aonekane kama jambazi sugu. Kila mtu alimgwaya, hakutaka hata kumkaribia seuze kumgusa.

Kama kawaida ya warembo, huwa hawaogopi kitu. Mmoja akajipitishapitisha ili apate chochote kwa mtu huyo. Laiti kama angejua kuwa mtu mwenyewe kaja kwa kazi zake asingepoteza muda.

"Unataka nini?" akamwuliza yule binti. Yule msichana mwenye kadiri ya miaka ishirini au ishirini na mitano akamtazama usoni mwanaume huyo na kumrembulia macho. Amata , kichwani mwake kulikuwa na jambo moja tu; kazi.

"Sihitaji hiyo biashara, chukua unachokunywa upotee," akamwambia. Yule msichana akageukia kaunta.

"Nipe *Coke* moja na *kisichana*, usisahau vipande vya barafu," akaagiza na kinywaji kikaletwa. Amata

hakujisumbua kabisa na binti huyo kahaba. Aliendelea kusubiri kile anachokihitaji. Aliitaza,a saa yake, muda ulikuwa ukiyoyoma. Akiwa katika kufikiri hili na lile akahisi kutomaswa mgongoni. Mtomaso ule aliuelewa maana yake. Akainua bilauli yake na kujimiminia kinywaji kwa mtindo wa tarumbeta, kisha akateremka na kuacha vinywaji vilivyobaki pale kaunta na noti mbili za elfu tano tano. Akamfuata yule aliyemgusa. Wakatoka pamoja mpaka nje. Wakaingia katika kichochoro kimoja kinachotenganisha jengo hilo na majumba mengine ya Wahindi.

"Kamanda! Hahahaaaaaa… Hata mimi sikukujua," Chiba akamwambia Amata.

"Kawaida tu! Chiba, leo nina kazi kubwa kaka, nataka uwe nami,"

"Usijali nipo jirani nawe," akaingiza mkono katika kimkoba chake, akatoa bastola moja nyeusi safi kabisa, ukiitazama unaweza kusema ni ya plastiki. Kamanda akaitazama, akatikisa kichwa.

"Ya Kirussi," akatamka.

"Ndiyo! Ni nzuri sana , chukua uitumie. Inapiga mbali na ina nguvu sana. Tazama hapa," akamwonesha kitu fulani kama skrubu. "Hapa ukibonyeza na kusukuma mbele,

bastola hii inuwezo wa kupiga burst," akamwonesha, "ilikuwa na uwezo wa kubeba risasi nane, sasa tumbo lake linabeba risasi ishirini nan ne," akashika magazini yake na kuizungusha. Alipoifyatua , akachomoa risasi kumi zenye wembamba kama msumari

"Hizi ndo risasi zake…"

"Zikiisha je?"

"Nakupa mkoba kaka," Chiba akamwambia na kutoa kiboksi kwenye mkoba wake wa mgongoni na kumpatia. "Kazi kwako! Najua sasa hivi wale washenzi wanakuwinda kila kona…"

"Nami nawawinda pia, lazima wajue kuwa muinda huwindwa," Amata akamjibu Chiba wakati akiisunda ile bastola kiunoni mwake. "Safi sana Chiba, tunajivunia kuwa na mtu kama wewe". Akampiga begani huku akimwacha palepale uchochoroni. Amata akapotelea kwenye vivuli vya majumba ya Wahindi huku Chiba akibaki kumsindikiza kwa macho.

"Chui kazini!" Chiba akasema kwa sauti ndogo.

* * *

Majira ya saa saba hivi, Kamanda Amata alikuwa akiambaaambaa na korido za maduka na maofisi yaliyossheeheni katika mtaa huo. Akaufuata mtaa wa Samora na kuipita picha ya Askari akaikuta barabara ya Pamba na kukunja kulia, kisha akaingia kwa ndani kidogo. Akapita kituo cha mafuta na kuibukia katika ukuta wa hoteli aitakayo. Moteli Agip!

Kama mwenyeji, alitumia mlango wa nyuma ambao hutumika na watu wa usafi kuingilia ndani, akatembea kwa hatua za kujiamini mpaka alipoukuta mlango wa pili. Akautikisa. Umefungwa. Akachukua funguo zake na kucheza na kile kitasa kwa sekunde chache tu, mlango ukatii. Alipoufungua ili apite, akasikia sauti za watu zikitokea upande huo. Akaurudishia na kujibana nyuma yake. Walipopita kwenda upande mwingine, naye akafuata. Viatu vyake havikufanya kelele hata kidogo, vilitengenezwa kwa soli imara ya mpira. Akazikwea ngazi mpaka mlango namba 206. Pale akasimama kwa sekunde kadhaa akiruhusu masikio yake yasikilize sauti ndogo kuliko zote. Jozi la sekunde likapita, hakuna mtu. TSA 1 alirudiwa na kumbukumbu iliyomfanya atekwe siku kadhaa nyuma katika eneo hilohilo na hoteli hiyohiyo, na mara hii alirudi tena palepale. Akachukua kitu kama waya kutoka kwenye moja ya mifuko ya kile kijaketi chake, akaukunjua vizuri na kisha

akaupenyeza kwenye tundu la ufunguo mpaka upande wa pili. Waya ule katika mwisho wake mmoja ulifungwa kamera ya siri ya kijasusi, na upande wa pili ungeweza kuona picha hizo kwa kuunganisha na simu janja yako. Alipofanikiwa kuupenyeza, akachukua simu yake na kuiunganisha upande wa pili kisha akaangalia nani aliyeko ndani humo. Akapiga picha huku akingalia katika simu yake. Kweli, hakukuwa na mtu, kitanda klikuwa pweke kabisa. Akaukunja ule waya na kuurudisha mahala pake. Mfuko mingine, akatoa ufunguo aliouamini, Malaya na kuutumbukiza kwenye lile tundu la ufunguo. Akacheza na kile kitasa kwa namna ya pekee, mlango ukafunguka. Naye akajitoma ndani. Alipohakikisha kila kitu na kila upande ni salama, akavuta kiti akaketi nyuma ya mlango akitazama kitandani. Pembeni akajiwekea chupa ndogo ya pombe kali na kuendelea kunywa kama yupo nyumbani kwake.

Mwanga hafifu kutoka nje ulikuwa ukimulika ndani ya chumba hicho. Amata akiwa palepale nyuma ya mlango kwenye kiti kidogo, akachomoa bastola yake aliyoibana mguuni, akaiweka mezani. Kisha kwenye kizibao chake akatoa kiwambo cha sauti, akaichukua ile bastola na kuifunga barabara ili isilete kelele itakapokuwa kazini. Akaitazama saa yake, inakimbilia saa nane za usiku.

*Saa za wanga na wezi zimefika!* Akawaza na kuachia tabasamu pana. Mara akasikia sauti ya viatu ikijongea kutoka kwenye korido upande wa nje. Mwendo wa mtu huyo ulionesha wazi kuwa alikuwa akikimbia kwa hatua ndogondogo. Akajikuta akicheka kwani alijua wazi kuwa kwa mwendo huo basi huyo mtu atakuwa kabanwa na mkojo na si kingine. Akaiinua bastola yake na kuiweka tayari. Si kwamba alikuwa anajua kuwa mtu huyo ataingia chumba hicho, hapana, ila tahadhari kabla ya hatari ni muhimu. Tayari alikwishatambua kuwa mtu huyo ni mwanamke kutokana na jinsi anavyotembea. Akasubiri aone maana alijua wazi kuwa Mc Field ana uwezo wa kujifanya hata mwanamke ili tu atimize lengo lake.

*Ulinitoroka kipindi kile leo huchomoki*, alijisemea huku akijikuta hasira zikimtambaa taratibu. Mara funguo ikapachikwa katika tundu lake. Amata akajiweka tayari. Upachikaji wa funguo ulikuwa wa fujo na baadae mlango ukafunguka. Amata akatulia ili kuona nani anayeingia. Mwanamke. Mwanamke mwenye asili ya kiarabu. Mweupe, mrefu kiasi, mikononi alikuwa na mkoba, vazi jeusi linalometemeta lilikuwa limefunika mwili wake kuanzia juu kabisa ya mapaja na kuishia juu kidogo ya matiti. Moyo wa TSA 1 ukapata tabu kidogo. Akameza mate ya uchu. *Kumbe*

*kuna waarabu wana shepu tamu namna hii?* Akajiuliza. Akajikuta analegeza mkono ulioshika bastola yake.

Yule Mwanamke akaiendea swichi pale ukutani, alipotaka tu kuwasha, akashangaa taa ile inawaka sekunde moja kabla yeye hajafanya hivyo. Akashtuka. Akiwa katika hali ya mshangao, akasikia kitu kikiwekwa mezani. Akageuka na kukutana uso kwa uso na domo la bastola ya Amata, *Beretta Pico*. Mwanamke yule akaanza kutetemeka.

"Usiniue nakusihi!" aliongea kwa sauti ya woga akibembeleza.

"Hata Malaika watanishangaa nikiua kiumbe kama wewe, ninachotaka ni majibu ya maswali yangu mawili tu," Kamanda akamwambia huku akiweka sawa pama lake kichwani, "Wewe ni nani?"

"Aaaa! Aaan! Mi' naitwa Amba," akajibu, lakini lafudhi yake ilionesha kabisa kuwa hakuwa Mtanzania.

"Swali la nyongeza kabla ya la pili… unatokea wapi na unafanya nini hapa?" akamuuliza.

"Mimi natokea Afrika ya Kusini, nipo Tanzania kwa miaka miwili sasa, nafanya kazi Las Vegas Cassino. Huyu ni mteja wangu tangu afike hapa miezi minne ilopita, huwa

nakuja kumstarehesha kwa ujira mnono. Nafikiri umenielewa, niache niende," akajibu haraka haraka huku akirudishia viatu vyake miguuni tayari kuondoka. Amata akamuonesha ishara ya kuwa hawezi kuondoka.

"Ow! Shit!" yule mwanamke akahuzunika, akapeleka macho yake sehemu ya chiini ya mwili wake. Kajikojolea. Amata hakujali na wala hakuutazama mkojo ule kwani hilo alilitegemea.

"Swali la pili, mteja wako yuko wapi?" akamhoji tena.

"Anakuja, amesema kuna kazi anamalizia kufanya lakini anakuja akanambia mimi nitangulie huku anikute," akajibu kwa ufasaha.

"*Good girl*, sasa huwezi kuondoka. Panda kitandani, umsubiri mteja wako… tena tulia kimya!"

"Hah! Hivi nilivyo?"

"Ndiyo…". Yule mwanamke akajitazama tena, loh; hakutamani kuwa katika hali ile.

"Lete mkoba wako hapa!" akamwamuru. Amba akaupeleka mkoba. Amata akaukagua ndani, akakuta vipodozi, simu, pedi, heleni, pete ya dhahabu na mikufu

kadhaa, bangili za kisasa, kitita cha pesa za kigeni na funguo za gari.

"Ok," akauweka ule mkoba chini huku mkononi akiwa kabaki na simu ya yule mwanamke, "Msubiri mteja wako kama ulivyopanga kumsubiri," akamwambia. Lakini yule Mwanamke akabaki haelewi anachoambiwa.

"Huelewi? Vua nguo zako, panda kitandani jifunike umsubiri, mi sina shida na wewe nina shida na mteja wako ambaye hata mimi ni mteja wangu vilevile," akamwambia. Amba akavua kigauni chake, akabaki na sidiria nyeusi na chupi mchinjo ya rangi hiyo hiyo. Akavua sidiria. Astaghafullulah! Amata akahisi moyo ukimwenda mbio maana titi zilizojaa vizuri zilikipendezesha kifua cha mwanamke huyo. Wekundu wake uliweza kumfanya mwanaume yeyote rijali apate shida katika maungo yake. Akaondoa na ile chupi akabaki kama alivyo. Amata alilisanifu umbo mwororo la Amba. Yule Mwanamke akapanda kiandani na kuvuta shuka mpaka kidevuni, Amata akazima taa.

* * *

Majira ya saa tisa usiku, Kamanda Amata alihisi mlango ukitikisika, na mara ukafunguliwa kwa kasi kwa minajiri ya

kumbamiza Amata pale alipo. Mc Field aliingia haraka bastola mkononi na kuwahi kutazama nyuma ya mlango, hamna mtu, isipokuwa chupa ya pombe na bastola.

"Shiit!" akashangaa na kutamka kwa sauti ya chini. Wakati huo Amba nae alikuwa amakurupuka kwa kishindo kile.

"Tulia hivyohivyo, umeingia mikononi mwangu tena," Sauti ya Amata ilisikika nyuma yake.

Kumbe Kamanda Amata baada ya kuhakikisha kuwa Amba amepitiwa na usingizi alitoka pale alipo na kujificha bafuni akiwa amejua wazi hila za adui yake kwani alishajua kwa vyovyote huko aliko anafuatilia mazungumzo yake na mwanamke huyo. Amata aliona kati ya ile mikufu, mmoja ulikuwa na kinasa sauti cha siri, alikitambua. Mc Field alijikuta hana ujanja. Amewahiwa. Akataka kugeuka kumtazama mtu huyo.

"Tulia! Weka bastola yako chini…". McField akajiandaa kuinama kutimiza lile aliloambiwa.

"No! Usiiname, irushe chini," akamwambia, maana alijua kujitikisa kidogo mtu huyo anaweza kuleta madhara makubwa, "safi sana! Umekuwa kijana mpole sana siku hizi na si mtukutu kama zamani," maneno hayo ya dharau

yalimtia hasira McField. Alitamani amrukie Amata lakini alijikuta hana ujanja, alibakiwa na mbinu moja tu na alikuwa akitafuta jinsi ya kuitumia.

"Geuka, mikono yako ikiwa juu," akamwamuru. Mc Field akageuka. "Hahahahaaaa! Leo una sura ya Kihindi… hivi wewe kwa nini umekuwa mwoga namna hiyo siku hizi? Umeanza kuzeeka ee? Basi leo ndiyo mwisho wako… Roho yako nitaitia kwenye mfuko wa suruali yangu. Nani amekutuma kuja huku tena? Kufanya nini?" akamtupia maswali baada ya kumkejeli.

"Hilo hupaswi kujua mbwa mweusi kama wewe! Waume zenu wanaowalisha ndiyo walionituma, nimetumwa kuua, kukuua wewe!" alipojibu tu, akashusha mkono haraka. Kamanda Amata alikwishalijua hilo, akajirusha upande wa pili wa chumba. Risasi ikapiga kwenye kabati la kioo. Amata akajinyanyua haraka. Kabla hajatulia, konde kali ya McField likatua shavuni. Konde la pili, Amata akalikinga kiufundi kabisa.

Amba alikurupuka kutoka pale kitandani akajikunyata kwenye kona ya chumba. George McField akatumia kichwa kumtandika Amata. Kamanda akayumba na kujibamiza ukutani kabla ya kuanguka chini. Alihisi kama kagongwa na garimoshi. Kutoka pale chini akamwona Mc Field akimjia na

kisu mkononi. Akavuta stuli ndogo iliyo karibu na kitanda na kuirusha kwa mikono yake, ikampiga McField usoni, kisu kikamdondoka. Kamanda akanyanyuka kwa kasi. Akapiga *round kick*, miguu yake ikamchapa Mc Field sawia kichwani. Akaangukia mpaka kitandani. Mzungu yule akajirusha upande wa pili wa kile kitanda ambapo palikuwa na ua la plastiki lililowekwa katika bilauri kubwa la chupa. Akasimama na kuliinua. Kwa kutumia mkono wake wa kuume uliojaa vizuri, akalirusha kwa Amata. Hakika kama angekuwa mtu wa kawaida wewe msomaji, bilauri lile lingemuumiza vibaya lakini Amata alilipiga kiustadi kwa mikono yake na likatawanyika vipande vipande. Nyuma ya vipande vile akamwona Mc Field hewani akija kama mbogo aliyejeruhiwa. Amata akamuepa. Jamaa akatua chini peke yake.

Mc Field akatega mikono yake katika mtindo mahili wa *kung fu* kumkabili Amata, miguu yake aliipanga katika namna ya kupendeza na mikono yake ilizunguka taratibu ikionesha jinsi pigo lijalo litakavomaliza kazi. Usoni mwake tayari damu zilikuwa zikitiririka. Chumba kile kiligeuka uwanja wa vita. Vita ya mahasimu wawili waliokuwa wakiwindana kwa miaka na miaka. Mara hii kila mmoja aliifurahia nafasi ya kukutana tena. Amata akajiandaa kumkabili mshenzi yule. Naye akaweka mtindo mwingine wa *Kung fu*. Akasimama

kwa namna yake kumkabili McField. Hakuna aliyetabasamu wala kucheka, kila mtu alijawa na pepo la mauti.

Amba, alijitoa pale kwenye kona na kuiwahi bastola ya McField iliyokuwa chini. Kamanda Amata akaliona hilo, alipogeuka kidogo tu, maana alijua hatari inayokuja. Kwa kitendo hicho akapoteza umakini kwa nukta kadhaa. Alijikuta akipata mapigo matatu ya *Kung fu* ambayo hakuweza kuyakinga hata kidogo. Maumivu makali yakalifikia bega lake akahisi kama limevunjika. McField akaanza kumpelekea mashambulizi ya haraka haraka ambayo yalimpoteza kabisa Amata. Akaanguka chini kama gunia la karanga, akawahi kujigeuza na kulala kifudifudi.

"Mwisho wako umefika, unafikiri kila mtu ni wa kuchezea, sasa leo Tanzania itakuomboleza wewe na Rais wako," McField alimwambia Amata kwa hasira huku akiuma meno, alikuwa akimsogelea taratibu pale alipo. "Inuka, nikumalize, mbwa mweusi we!" Akamkamata ukosi wa kizibao alichovaa na kumburuza, "nitakuuwa kwa kukuchinja, nitatenganisha kichwa na kiwiliwili chako," alimwambia huku akimburuza kumpeleka bafuni. Kwa mapigo yale Amata alikuwa hoi kana kwamba kakutana na *robot*. Mkono wake ulivimba, damu zikimtoka upya kwenye jeraha lake, lakini hakuona nhaja ya kuuawa kikondoo.

Aliukamata mguu wa Mc Fiel kwa mkono uliobaki, Mc Field akashtuka na kuinama kumtazama. Kwa kutumia mkono uleule uliovimba alimdaka shati na kumvuta kwa nguvu mpaka chini. Kabla hajafika chini sawasawa, akamtandika konde zito lililotua moja kwa moja kwenye koromeo. Maumivu makali na kiu cha dharula kikampata, akakohoa mfululizo. Amata akamsukumia kando na kumbwaga. McField akawahi kuinuka, akiwa wima akakutana ngwala nyingine iliyomrudisha sakafuni huku akijigonga kichwa vibaya na kutua kama mzigo. Amata akainuka na kumtazama hasimu wake akiwa chini, damu zikimvuja puani.

* * *

"Vipi?" Madam S aliuliza.

Chiba akamtazama kabla ya kumjibu, "Saa kumi inakaribia," akajibu. Scoba bado alikuwa kwenye usukani akiendesha taratibu. "Gari ya Mc Field hii hapa maegeshoni," Chiba akamwambia Madam.

"Kamanda atakuwa salama kweli?" Madam S akauliza huku akiweka bastola yake vyema, tayari kwa kazi. "Nisubirini hapa," akawaambia.

Utulivu ulitawala katika mitaa ya katikati ya jiji, watu wachache wachache walionekana kupita huku na huko wakiwa na safari zao za usiku. Ndani ya Motel hiyo ya Agip utulivu ulichukua nafasi, vishindo vilivyotokana na mapigano yale havikusikika upande wa chini ambako wahudumu walikuwapo. Kila aliyekuwa macho aliendelea na mambo yake, na aliyesinzia alisinzia. Mchezo uliokuwa ukipigwa ulikuwa wa wajuvi hivyo haukuleta mushker.

Madam S alikuwa na mawazo mengi sana usiku huo, maana alijiuliza maswali yasiyo na majibu. Alikuwa ametulia, tuli, katika kiti cha nyuma cha gari lile.

"Bora hata sikuwahi kuolewa!" akasema. Chiba akamtazama na kucheka, "Kwa nini?" akamwuliza.

"Namna hii si ngeshaachika? Saa tisa hii mwanamke niko nje sihudumii ndoa, hahahaaaa!" akaongea huku akicheka.

"Hivi mama huna hata mtoto wa dawa?" Scoba akauliza.

"Ninao!" akajibu.

"Wangapi?"

"Watano,"

"Watano!" Chiba akashangaa.

"Ndiyo, watano, wa kike wawili na wa kiume watatu ila ni watukutu balaa, ndio wananifanya mi nisilale mpaka sasa," akawajibu. Wote wakacheka *kizungu* bila kutoa sauti.

Chiba akiwa katika kujiandaa kuelekea katika ile motel, mara walisikia sauti ya kioo kinachovunjika na sekunde chache kitu kama jiwe au furushi kilitua juu ya gari moja iliyokuwa limeegesha upande huo.

"Nini ?" Madam akauliza. Haraka, akateremka na bastola yake mkononi, chiba akifuata nyuma, wakaelekea upande ule. Scoba alibaki nje akiangalia usalama.

* * *

Wakati timu hiyo ya TSA ikiwasili eneo lile, mtanange bado ulikuwa mbichi. George McField aliinuka. Kipigo kile kilimnyong'onyeza lakini bado mwili wake ulikuwa kikazi.

"Hujaniweza bado!" McField akamwambi Amata na kumvamia kwa nguvu, akambeba na kumbamiza ukutani. Amata haraka , akamsukuma lakini akakutana na makonde mfululizo. Yapo aliyoyakwepa lakini mengine yalimpata sawia. Mzungu yule alikuwa amesheheni silaha nyingi za kijasusi mwilini mwake. Akachomoa kisu kidogo na

kukimata kwa kono lake la kulia. Dhamira yake ilikuwa ni kukizamisha utosini lakini pigo lile Amata aliliona, akaepa. Mkito wa kisu kile ukachana nyama ya bega kwenda chini. Amata akamtandika konde moja la mbavu. McField akaguna. Kabla hajajiweka sawa, akamtandika lingine, alipoinama kujishika mbavu, Amata akampiga kifuti kilichotua kwenye paji la uso, akainuka wima. Mapigo mfululizo yalimchakaza McField.

Amba alikuwa kimya machozi yakimtoka, hakuwahi kuona mapigano kama yale mbele yake, zaidi ni kwenye sinema. Hali ya McField ilikuwa mbaya. "Sasa nakunyonga, mshenzi wewe!" akamwambia huku akiuchomoa mkanda wa suruali yake. Akiwa katika kufanya hivyo, akasikia kishindo cha kioo kupasuka. McField hakuwepo chumbani.

"Shubamit!" akang'aka kwa hasira na kuliendea lile dirisha, akasimama na kuangaza macho kama atamwona aakikimbia au vipi. Alipoona hakuna lolote, akarudisha macho kwa yule mrembo, Amba.

"Vaa nguo zako!" akamwambia huku akijitazama ule mkono uliovimba, na lile jeraha la kisu. Amba, akavaa harakaharaka. Saa ya Kamanda Amata ikaanza kumfinya mkononi, akaingiza mkono kwenye moja ya mifuko ya

kizibao chake na kutoa kifaa maalum cha mawasiliano. Akakipachika sikioni.

*"Yes!"* akatamka.

"Tupo, tumefika!" ilikuwa sauti ya Madam S.

"*Ok*, kama unaweza panda 406 haraka uone cha kuona. Chiba hifadhi huo mwili kama hauna uhai," akamaliza. Amata akamtazama Amba akitetemeka pale kitandani. Alikuwa tayari amekwishavaa nguo yake ileile.

"We mwanamke, usipende kuwa na wapenzi usiowajua, angekuua huyu! Ni jambazi," Amata akamwambia Amba. Mlango ukagongwa na Madam S akaingia.

"Pole Kamanda, naona mkono wako umepata shida," Madam alisema.

"Ndio, nahisi kama mifupa imepishana na hapa kisu kimenichana vibaya," akajibu.

"Scoba akuwahishe kwa Jasmini ukapate matibabu, hili la hapa niachie mimi na Chiba," Madam akamwambia Amata.

"Sawa!" akajibu na kumtazama yule Amba, "Twende huku," akamwamuru. Madam S ndipo akagundua kuwa

kuna mtu wa tatu mle ndani, akamtazama binti huyo kwa tuo, “Nani huyu?” akauliza.

“Ah, wafanyabiashara hai,” Amata akajibu huku akimswaga nje Amba. Wakafika mahali pa mapokezi wakakutana na hudumu wa hapo. Kamanda Amata akamtazama bila kuongea kitu.

“Unalala sana, unaweza kuvamiwa na kuuawa hivihivi!” akamwambia, “Haya, sasa hakuna kupokea wageni kwenye hotel hii mpaka mpate kibali kingine cha serikali, tunaiweka chini ya uangalizi kwa masaa machache na kufanya ukaguzi wa chumba kwa chumba naomba uhakikishe wageni wote wasitoke kuanzia sasa,” Kamanda akatoa amri huku akimwonesha kitambulisho u-inspekta wa polisi.

“Sawa, lakini ni swala la kumwambia meneja, maana wengine wana ndege alfajiri hii,” yule mhudumu akamwambia Amata.

“Mpigie simu meneja mwambie afike hapa haraka,” alipomalisa kusema hayo akaongoza nje, akamchukua Amba na kumtia kwenye gari.

*   *   *

McField alipojirusha kutoka kwenye kile chumba. Alijikuta akifikia juu ya gari. Mwanguko wake haukua mzuri ukizingatia alijrusha pasi na kujiandaa. Juu ya gari lile alivunjika vibaya na kushindwa kusogea hata sentimita moja. Madam S na Chiba walifika hapo na kukuta mtu huyo akiwa hoi akipigania pumzi zake za mwisho.

"Limepatikana leo!" Madam S akamwambia McField. Cha kwanza ilikuwa ni kumtia pingu hata kama ni nusu mfu, cha pili na kumteremsha na kumbwaga chini. Walinzi wa kituo cha mafuta cha karibu walisogea na kupewa kazi ya kumpakia garini kisha Chiba na Madam S wakaondoka zao huku wakiwataka kuwa kimya. Kamanda Amata aliwasili kwenye gari akiwa na Amba na kumpakia garini. "Umempata yule hayawani?" akamwuliza Scoba.

"Yupo huko nyuma anakata roho!" akamjibu huku akimwonesha upande huo. Amata akamwendea na kumtazama McField aliyekuwa hoi bin taabani.

"Ulifikiri safari hii utatoroka tena? Utafia hapa hapa," alimwambia. Scoba akachukua kisanduku cha huduma ya kwanza na kumganga kidogo *kaka* yake. "Hii lazima tuwahi kwa Jasmini!" akamwambia.

"*Yeah*! Twende Shamba!"

“Na huyu Mwanamke?” akauliza.

“Hapana, huyu tunamtupa shimoni hapo mbele, au unamhitaji tunpeleke *home* kwako?” Amata akajibu na kumtania Scoba.

“Aaaah braza!” Scoba akajibu huku akiondoa gari.

“Shauri yako na ulokole wako!”

Walipokatiza mtaa wa kwanza, wa pili, watatu; Amata akamwambia Scoba asimamishe gari.

“Vipi?” Scoba akauliza. Amata hakujibu, akamtazama Amba, “Teremka, ondoka na usimsimulie mtu chochote ulichokiona,” akamwambia kisha akaketi vizuri. Amba akateremka na kukimbilia mitaani kama mwendawazimu.

Nusu saa baadaye gari la Scoba likaegeshwa vizuri mahala pake. Kamanda Amata akateremka na kufungua buti kwa mkono wake mmoja. Scoba akafika na kumshusha Mc Field aliyekuwa hoi, akamkokota na kumwingiza kwenye chumba kimoja kisicho na madirisha wala chochote isipokuwa sakafu na choo tu.

“Kaa humu, nakuja unijibu maswali yangu kabla sijakuua,” Amata akamwambia McField wakati Scoba

akmtupa chini sakafuni. Mlango ule ukafungwa kwa namba maalum.

* * *

Dkt. Jasmin akampokea Amata na kumwingiza moja kwa moja kwenye chumba maalum cha matibabu. Huko alimganga kwa kumpa tiba zote zinazowezekana, akamfunga bendeji maalum mkononi na kumwekea kamba ya kuvalia shingoni.

“Ulikuwa hujapona vizuri Amata umejiongezea matatizo. Kumbuka we ni binadamu pia, unapopambana na adui yako wakati hauko kamili kwenye viungo vyako unaweza kupoteza na kupotezwa…”

“Sawa Madam Jasmin!” Amata akajibu huku akitoa cheko la kimya kimya.

“We cheka tu,” Jasmin akamwambia wakati akimdunga sindano za kuzuia maumivu.

Dakika arobaini na tano baadae, Madam S na Chiba waliwasili. Pamoja nao walikuwa na begi moja kubwa. Wakaingia kwenye chumba maalum walichokipa jina ‘*Strong Room*’. Wote walipokwishafika ndani ya chumba hicho lile begi lakafunguliwa.

"Mnaona kazi hii?" Madam aliwaeleza vijana wake. Ndani ya begi hilo walikuta vitu vingi tofautitofauti vinavyotumika kujibadili sura, dawa za kunenepesha na kukondesha kwa muda mfupi. Pia kulikuwamo vitambulisho zaidi ya hamsini vya idara mbalimbali kilichowagusa zaidi ni kile cha dereva wa Rais, hati za safari za nchi mbalimbali, pesa maburungutu za Kitanzania na za kigeni, silaha za kila aina kama bastola, viwambo vyake na silaha nyngi ndogondogo za kijasusi. Madam S alikiweka kando kile kitambulisho na kuendelea kupanga mezani kitu kimoja baada ya kingine. Wote walikuwa wamevaa vinyago maalum ili kujizuia endapo kwenye begi hilo kutakuwa na vitu vya kemikali.

"Hii ni hatari sana," Gina aliongea kwa sauti ya chini. Wote walibaki midomo wazi, begi hilo lilikuwa limetengenezwa kwa malighafi ambayo ukiipiga exray itakuonesha tu ndani kuna nguo na vitabu hata kama ndani hamna kitu, nah ii ilimfanya mtu huyu kuweza kupenya kwenye vizuizi vya Uwanja wa Ndege.

"Kamleteni hapa!" Madam akatoa amri. Chiba na Scoba wakaenda kwenye kile chumba kumleta Mc Field, wakamkamata huku na huku na kwenda naye. Hawakujali hali yake wala hawakuwa na huruma naye. Wakamburuza

mpaka kwenye kile chumba na kumtupa sakafuni. Chiba na Scoba wakachomoa bastola zao. McField alitua sakafuni na kujigeuza haraka huku akitoa yowe la uchungu. Uti wake wa mgongo ulikuwa umejeruhiwa kwa kipigo kule hotelini. Macho yake mabaya yakakutana uso kwa uso na ya mwanamke wa chuma, HoT; Head of TSA.

"Ulipofanikiwa kuponyoka mara ya kwanza, hukutakiwa kurudi mara ya pili… bahati huwa haiji mara mbili. Leo umenasa mikononi mwetu pumbavu wewe!" Madam S akamwambia McField aliyeonekana kutokujali maumivu yake.

*"Stubid!"* McField alimtukana Madam S. Amata akavuta hatua tayari kumsulubu mwamba huyo lakini mkono wa Madam S ukawa tayari kifuani pake.

"Acha! Huyu ni motto sana… hawezi kuleta shida!" akamwambi na Amata akatulia. "Shusheni bastola zenu, nataka anijibu maswali yangu kwa Amani kabisa… Tanzania ni nchi ya Amani hatutakiwi kuonesha silaha za moto hadharani, ni kinyume cha sheria," akamwambia Scoba na Chiba. Jasmin na Gina walikuwa kando wakiangali na kusikiliza kila kinachoendelea.

“Sasa utuambie, lengo zaidi la kuja hapa ni lipi, na nani kakutuma?” Madam S akamuuliza. Mc Field aliyekuwa pale chini. Badala ya kujibu akabaki kimya akimtazama mwanamke huyo.

“Subirini msikie, Rais wenu amejiua mwenyewe, na atakufa, tuko wengi sana, hamtatuweza sote, azma yetu itatimia popote pale atakapokuwepo… hahahaaaaa *stupid all of you!*” McField akajibu kijeuri huku akimalizia na tusi.

“Unajua unaongea na nani?” Madam akamuuliza. Vijana wake wote walikuwa kimya wakifuatilia kila hatua na kila nukta.

“Ahahahaaaaa! Hahahaaaaaa… koh! Koh! Khooo!” McField alitoa cheko la kifedhuli na kuanza kukohoa mfululizo. Cheko lile liliwafanya TSA wacheke pi isipokuwa Amata na Madam S waliokuwa bado kweny umakini wao. Wakiwa katika kicheko kile, ghafla McField aliinuka kama umeme kumvamia Madam S. kwa kasi zaidi ya ile, Amata aliachia pigo la dharula akiwa tayari mbele ya bosi wake. Pigo lile lilitua sawia kwenye mifupa inayoulinda moyo na kuivunja vibaya. McField alirudi nyuma kwa kasi ya uszito wa lile pigo. Akajibamiza ukutani na kujibwaga chini huku povu likimjaa kinywani. Uhai ukamwacha. Madam S hakuamini kilichotokea, alijikuta tu yuko nyuma ya mgongo

wa Amata. Hakujua kama ni yeye aliendа kusimama nyuma yake au ni Amata alikwenda kusimama mbele yake.

Amata akashusha mikono yake na kuwaangalia wenzake, tayari Chiba na Scoba bastola zilikuwa juu na vidole vyao kwenye kifyatulio. McField alikuwa chini kimya kabisa.

"Wasalimie babu zako," Amata akasema na kurudi katika hali ya kawaida. Akageuka kumtazama bosi wake, "Ulikuwa unakufa…"

"No! ningekufaje na wewe upo?" akamwambia huku akivuta hatua kutoka ndani ya kile chumba, "mwacheni apoe hapohapo, nyie tuonane chumba cha mkutano. Kazi ndo kwanza inaanza," akawaambia huku akiongoza njia.

# 1xi

NJE YA JENGO la Ikulu, palikuwa na watu wengi. Wengine wakiwa kwenye viti wameketi na wengine wakiwa wamesimama hapa na pale wakiwa na kamera zao pamoja na vifaa vya kunasa sauti. Kwa walivyo tu walijulikana kuwa ni waandishi wa habari. Bado katika lango kuu kulikuwa na wengine wanaongia, wakikaguliwa kila kona na vijana wa usalama waliowekwa hapo kuhakikisha ulinzi unakuwepo.

Watu wa luninga nao walitega kamera zao hapa na pale ili kuhakikisha wanapata picha nzuri kadiri iwekanavyo, wakirekebisha vinasa sauti vyao na huku magari yao makubwa yenye mitambo ndani yake yakiwa tayari kupeleka maangazo hayo moja kwa moja kwa wananchi.

Huko majumbani nako kila mmoja alifanya kazi harakaharaka ili awahi kutazama au kusikiliza nini mkuu wa nchi anataka kuliambia Taifa. Na hali hii ilitokana na utata wa mambo makubwa mawili; kudunguliwa msafara wa Rais kule Bunju na wizi wa almasi uliofanyika Mwadui ukimhusisha waziri wa nishati na madini. Ilikuwa siku ya aina yake. Kila mtu aliisubiri saa nne na nusu ifike. Kwenye

migahawa, mabaa, maofisini wote walikuwa tayari kusikiliza hotuba ile, na kila mmoja akisubiri jibu la maswali yake.

* * *

Saa mbili asubuhi, kabla ya tukio la Rais kulihutubia taifa, katika ofisi ndogo ya TSA kila mtu alikuwa tayari kajipanga kwa tukio hilo. Hawakuwa na amani kabisa ijapokuwa McField alikuwa tayari marehemu lakini bado walitatanishwa na kauli yake 'tuko wengi'. Ijapokuwa walijua wazi kuwa Tracy bado hawajafanikiwa kumpata lakini taarifa ya kuwa wapo wengi ilizidi kuwafanya waongeze umakini katika kazi yao.

"Kama tulivyoongea jana, huyo mwanamke ambaye picha yake nimewapa mumgundue mapema," Madam S akawaambia.

"Nina wasiwasi anaweza akafanya maajabu hapa," Kamanda Amata akaunga mkono hoja kwa kauli hiyo.

"Ndio, daima inabidi tuwe katika tahadhari," Chiba akaongezea.

"Si mnajua Mkuu atahutubia asubuhi hii? Basi muwe makini na mjikamilishe kila idara. Chiba kazi yako unaijua, hakikisha unakamata mawimbi yoyote ya sauti chochote

katika maeneo hayo, hakikisha unakata mawimbi yote ya simu kilomita nne za mraba. Scoba utakuwa tayari kuratibu usafiri kama itahitajika," akageuka kumtazama Gina, "unajisikiaje sasa?" akamuuliza.

"Niko sawa Madam," Gina akajibu.

"*Ok*, Gina na Kamanda nawarudisha katika kazi yenu, mtakuwa kwenye viwanja vya Ikulu kuangalia kila kinachoendelea. Mimi nipo hapa wala sitoki, mawasiliano yasikatike mpaka itakapoamriwa. Chiba kumbuka usikate *frequency* tunayoitumia bila taarifa! Sawa?" Madam akamaliza.

"Timamu Madam!" Chiba akajibu. Baada ya mazungumzo hayo mafupi na maagizo, kila mmoja alitoka kwa wakati na njia yake tayari kuingia kwenye umati ule wa watu. Kila kona kuliimarishwa ulinzi. Vijana wa TNS yaani usalama wa taifa Tanzania waliweka wavu wao wa usalama kila kona. Ukiachana na hao wanaojuana walikuwapo wasiojuana waliojificha kwenye idara na vitengo anuai. Jambo la muhimu lilikuwa ni kumlinda kiongozi wa nchi dhidi ya hujuma yoyote inayokusudia kufanyika, kama ipo ukizingatia ni wiki chache nyuma amekoswakoswa kuuawa.

Katika ofisi ndogo ni Madam S na Jasmini tu waliobaki wakifutailia kila kitu kwenye luninga maalumu ambayo

iliunganisha picha tatu kutoka kwa Amata. Gina na Scoba ambazo zilikuwa zikichukuliwa kupitia miwani walizovaa. Wakati polisi, jeshi na walinzi wengine wakiimarisha ulinzi hawakujua kabisa nini kinaendelea chini ya pazia ambapo TSA walikuwa wakichunguza.

*   *   *

Dakika chache kabla ya tukio lile kuanza, gari moja, Subaru lilisimama karibu kabisa na lango la Ikulu, eneo ambalo liliandaliwa kwa waandishi wote kushuka hapo. Mwanamke mwenye shepu tamu kwa kuiona kwa macho aliteremka akiwa na video kamera kubwa mkononi mwake. Mgongon mwake alikuwa na begi dogo alilohifadhia vitu vyake vichache. Mwanamke yule mweupe mwenye nywele ndefu alikuwa amevalia suruali ya kaki, blauzi nyeupe ambayo juu yake ilifuatiwa na kizibao cha randi ileile kilichokuwa na mifuko mingi, hili lilikuwa ni vazi maalum la wanahabari. Kifuani kwake upande wa kulia paliandika *PRESS* kwa wino mweusi. Akalifikia lango na kusimamishwa kwa ukaguzi. Ndani ya chumba kidogo alikaguliwa na kuonekana yuko sawa hakuwa na silaha wala kitu chochote cha hatari. Kitambulisho chake kilionesha kuwa ni mwanahabari kutoka kituo kikubwa cha luninga duniani NBC. Akapita na kuungana na waandishi wengine

ijapokuwa alichelewa kidogo. Katikati ya kamera nyingi akaweka ile ya kwake na kuhakikisha amekwishafanya mipangilio yote. Aliwasilisha kinasa sauti chake kwa kamati maalum nao wakakiweka jirani kabisa na mimbari ile itakayotumika na Rais kuwasilisha hotuba yake.

Saa nne na nusu kama ilivyopangwa, Rais wa Jamhuri alijitokeza na kukaribishwa kwa makofi baada ya kutoonekana wala kusikika kwa siku kadhaa. Mbele ya jopo la waandishi na wanausalama, Mkuu wa nchi alisimama na kisha kuanza kutoa hotuba yake iliyojawa na maneno mazuri na matamu.

Tracy Tasha aliingiwa na wasiwasi, kila alipojaribu kumtafuta Mc Field hakumpata simuni. Mpango walioupanga ulikuwa ni kukutana hapo, lakini alishangaa hakumuona swahiba wake. Wawili hawa walifanya kazi yao kwa muda maalum na si kila wakati. Walikuwa wakipanga muda wa kukutana mahali fulani kwa jambo fulani baada ya hapo kila mmoja aikuwa na hamsini zake. Hawakupigiana simu wala kutumiana ujumbe mpaka zibaki dakika kumi kukutana ndipo wangeanza kutafutana. Tracy akajua kwa vyovyote atakuwa tayari katika kona aliyomwambia atamkuta mara akikamilisha kazi yake. Laity angejua kuwa mwenzi wake tayari anajibu maswali ya uovu wake duniani

mbele ya kiti cha enzi, labda angejaribu kubadili mpango wa utekelezaji wa kazi hiyo. Kupitia kamera yake alikuwa akiitembeza kuangalia wote waliokuwa mbele, licha ya Rais na walinzi wake walioonekana kuwa makini katika kutazama huku na kule, alimwona mtu ambaye alimfanya moyo wake ulipuke. Tracy hakutegeme kumwona mtu huyo. Alitazama kwa makini na kumwona kwa makini vilevile. *Ni yeye!* Akawaza.

Kamanda Amata alisimama pembeni kabisa mwa jukwaa kuu, akiwa na ile plasta yake kubwa mkononi na mkono huo kuuning'iniza shingoni kwa mkanda maalum. Tracy akatabasamu, akajua hapa hana mkono hivyo mmoja hawezi chochote. Akatazama na wengine wote akaona walivyojipanga na jinsi walivyojiweka bastola zao ndani ya makoti yao. Tracy alitazama tena kwa makini sana hali nzima ya usalama, akaangalia wapi na wakati gani ataweza kuifanya kazi yake, akakumbuka maelekezo ya McField wapi pa kutokea pindi akikamilisha hilo. Alivuta pumzi na kushusha kwa nguvu kisha akarejesha jicho lake kwenye ile kamera.

TSA 1, alitulia kama sanamu. Macho yake yaliyofichwa kwa miwani nyeusi iliyokuwa ikipiga picha na kumpelekea Chiba mpaka ofisi ndogo yalikuwa yakimtalii kila aliyekuwa

mbele. Zaidi ya kuzisafirisha picha hizo, ikivuta na kurudisha na kuhifadhi katika kadi sakima ndogo iliyokuwa imepachikwa katiika kona moja ya miwani hiyo.

*"Point one!"* Chiba akaita

*"Clean!"* sauti ya Kamanda Amata ikajibu na wote wakaisikia vizuri.

*"Ponit two!"*

*"Clean!"* Gina akajibu kutoka juu dirishani ambapo aliweza kuwaona watu wote kwa chini.

Chiba alikuwa akiangalia kila tukio kupitia luninga zake ndogo ndani ya gari alililoliegesha nje ya ukuta wa Ikulu. Gari lile, Volkswagen Transporter lililofungwa kila kona na kuacha madirisha mawili tu kule mbele huku ubavuni mwake likiwa limeandika 'Habari Maelezo' lilikuwa likipokea picha zote kutoka kwenye miwani ya Gina na Amata. Chiba alikuwa ndani yake akikamata mawimbi mbalimbali ya mawasiliano yaliyokuwa yakikatisha eneo hilo. Kama alivyoamriwa na bosi wake, alizima mawasiliano yote ya simu kilomita nne za mraba. Aliweza kuchuja kila *frequency* inayokatiza usawa wake na kuisikiliza kama ina madhara kwa kuwa simu zilikuwa zikisuasua aliweza kuzipata chache zilizokuwa na jeuri ya kuupita mtambo huo.

Tracy aliiangalia saa yake mara kwa mara. Kitendo hicho kilimfanya Kamanda Amata kumuona na kumtilia shaka kabla ya kumtambua. *Kwa nini astazame saa yake mara kwa mara?* Akajiuliza. aliishika miwani yake na kumvuta karibu, picha yake haikuwa ngeni hata kidogo. Akaituliza hapo.

*"Ground zero! Ground Zero!"* akaita. Chiba akaipokea na kutazama kwenye kijiluninga chake, akaona sura ya Tracy Tasha akiwa nyuma ya kamera kubwa ya luninga. Akaivuta ile picha na kuiweka kando kisha akachukua kidijitali picha halisi ya Tracy nan a kuziweka pamoja kisha akauruhusu mfumo wake umtambue mtu huyo. Mfumo ule ulikubaliana na Amata, mwanamke huyo alikuwa Tracy ijapokuwa alijibadili kwa namna ya pekee.

"*Point one* kazini!" Chiba akaita lakini ilikuwa ni kupeleka ujumbe kuwa yuko sahihi na aanze kumtia mkononi mwanamke huyo.

"*Copy*," Kamanda akajibu.

"*Point two, stand by*!" Chiba akatoa ujumbe tena.

"*Copy,"* Gina akajibu, akashusha mkono chini na kuinua bunduki kubwa ya kudungulia aina ya SR 25 iliyotengenezwa huko USA iliyobuniwa na Eugene Stoner yenye urefu wa

inch 44.0. Gina aliipachika dirishani na kuweka jicho lake katika lensi iliyofungwa juu yake na kumwangalia vizuri yule mwanamke.

* * *

Tracy Tasha aligeuza kamera yake na kumtazama tena Kamanda Amata. Hayupo! Hakumuona pale alipomwacha mwanzo. Alihisi akili yake inaganda ghafla. Alitazama kwa chati huku na kule lakini hakumuona Amata mahala aliposimama. *Kaenda wapi mshenzi huyu?* Akajiuliza. Tracy alijikuta anashindwa kuchanganyikiwa. Hakuhitaji kupoteza muda. Hakuona sababu ya hilo. Aliigeuza kamera yake kwa heshimiwa Rais. Akamweka vizuri katika kioo chake cha kuvuta, akakijaza kifua cha Mkuu huyo, kisha kidole chake chembamba kikabonyeza kitufe chekundu cha kuiruhusu kamera hiyo ianze kunasa picha. Kizaazaa.

Ni nukta ileile, Rais alitupwa hewani, na ile mimbari ikienda chini. Walinzi wake walichanganyikiwa. Wale wa nyuma walijitahidi kumdaka lakini wote sita wakarudi chini na kufika naye sakafuni bila kipingamizi. Wale wa mbele wakageuka mara moja, na kumwendea Mkuu. Wakafungua vitu kama miamvuli wala hakuna mtu aliyejua wametoa wapi. Haraka wakalisalimisha eneo lile huku Rais akiondolewa katikati ya taharuki ile. Eneo lote

lilikwishazingirwa na askari polisi pamoja na vijana wa JW wakiwa na bunduki zao mikononi.

Tracy Tasha, alijishika kiuno katikati ya watu waliokuwa wakihaha huku na kule. Alikuwa akiangalia nini cha  ufanya. Hakuonesha woga wowote. Macho yake, kwa sadfa, yalitazama juu ya jengo la ikulu na kujikuta akitazamana na domo la SR 25. Akajaua *pamenuka*. Akabinya kijitufe kingine kwenye ile kamera yake na yote ikalipuka na kutoa moshi mzito uliowafanya watu kukohoa huku wengine wakitokwa na machozi yaliyochanganyikа na kamasi jembamba. Tracy alipoona tayari domo la SR 25 linamwelekea yeye alijuwa wazi kuwa sasa mambo yameharibika, kamera yake ambayo ilikuwa na bunduki ndani yake yenye kubeba risasi tatu tu, pia ilifungwa mabomu mawili ya machozi. Akayafyatua mara moja na ile kamera ikatawanyika vipande vipande. Yeye akajiangusha chini na kujivingirisha kisha akaibukia nyuma ya waandishi wa habari.

Wakati watu wakiendelea kukohoa, na kutokwa machozi, mwanamke yule alivuta hatua ndefu na kuufikia ukuta kisha bila hata kuugusa alijirusha sama soti akatua nje ya ukuta huo pasi na kuonwa na mtu. Lakini alijikuta na wakati mgumu sana pale alipojua kuwa McField alitakiwa kuwa hapo na hakuwepo. Akachanganyikiwa. Tracy

akaamua kujiokoa kwa akili yake mwenyewe. Akavuka barabara ya Magogoni kwa haraka na kuingia katika Chuo cha Utumishi wa Umma. Akiwa jirani na ofisi za chuo hicho, alikutana na mwalimu mmoja wa kike, akamwomba msaada wa kumwonesha msalani kwa kuwa alipatwa na shida ya moshi ule. Watanzania hatuna shida na Mzungu. Akamwongoza mpaka kule msalani.

Sekunde chache tu Tracy alitoka msalani akiwa na mavazi ya yule mwalimu. Wakati wanafunzi na wafanyakazi wakikimbilia mbele ya jengo hilo kujua kulikoni, yeye alipita katikati yao na kutokomea. Ving'ora vya polisi vilimchanganya kiasi fulani, alishindwa upande gani aelekee. Akapita jengo la kwanza na la pili, akaibukia nyuma. Hakuona njia nyingine ya kutoroka, akaivuta hijab aliyoipata kutoka kwa yule Mwalimu, akajiweka vizuri kichwani mwake.

*   *   *

Gina alitoa jicho lake katika lensi ya lile bunduki kwani alishachelewa kupiga, Tracy alipotea katikati ya ule moshi.

"Shiiit! Mwanaharamu wa kike," Gina aling'aka alipojikuta kazidiwa kete na Tracy. Aliendelea kutazama kwa

lenzi mtu mmoja baada ya mwingine huku kinywani mwake akiendelea kutukana matusi anayoyajua yeye mwenyewe.

*"Point two on duty?"* Chiba akauliza kama Gina yupo kazini au vipi.

"Ametoweka," Gina akajibu.

Kamanda Amata alipata wakati mgumu, alikuwa akimfuatilia Tracy kwa utaratibu maalumu kabla hajafanya kile anachotaka kufanya. Mara kizaazaa kilipoanza alijikuta akibabaika, hakujua amuendee Tracy au arudi kumsaidia Namba moja. Alijikuta njia panda kwani yote yalikuwa majukumu yake. Lakini alipokuwa akitafakari hilo, ni nukta hiyohiyo aliposikia kishindo cha pili kilichozua mtafaruku, moshi mzito uliomfanya hata yeye achanganyikiwe ulizagaa.

"*Point one, point one*!" Chiba aliita.

"Hali tete, mheshimiwa kaangushwa!" Amata alijibu haraka.

*"Man down!"* Chiba alipigwa na butwaa.

"Ametoroka! Ametoweka!" Gina alipeleka ujumbe. Amata, bastola mkononi, alihaha kutafuta huku na kule akiwa tayari ameweka miwani yake usoni ili kumtambua mtu huyo. Hakumuona. Tracy alikwishaliacha eneo lile.

* * *

Madam S alikurupuka katika kiti chake, "Jasmin, nifuate haraka chukua silaha!" akatoa amri nia Dkt. Jasmini akafanya hivyo, hawakuwa na haja ya kutumia gari.

"Vipi Madama, kuna nini?" akauliza.

"Mkuu wa nchi amedunguliwa," akajibu huku akimaliza kuchomeka bastola katika kiuno cha suruali yake ya suti. Wakatoka nje na kuvuka barabara. Huko nje hakukutamanika, magari ya polisi yalikuwa yakipiga ving'ora kwa fujo yakizuia njia zote. Kila mtu aliye karibu na ukuta wa Ikulu aliondolewa na aliyetiliwa mashaka alitupiwa kwenye kalandinga. Mitaa iliyozunguka makao ya Rais ilichafuka, kuanzia Hazina ndogo mpaka Magogoni kuzunguka mpaka hospitali ya Ocean Road, kwa ujumla kila upande ulimwagwa askari wakipekuwa mpaka kwenye vichaka huku wakiwa hawajui hata ni nani wanamtafuta.

Madam S aliingia getini na kukuta hali ya sintofahamu. Waandishi wote walikamatwa na kuwekwa mahala pamoja. Ilibidi kwa haraka lifanyike gwaride la utambuzi kwa waandishi hao kwakuwa uchunguzi wa haraka ulionesha ni wapi risasi ile ilitokea.

Kamanda Amata alilifuata gari la polisi lililokuja na mbwa, akamwomba askari mmoja ashuke na mbwa wake. Wakafuatana mpaka pale kwenye mabaki ya kamera ya Tracy. Yule mbwa alinusa hapa na pale huku akitoa kilio chake cha ajabu, kisha akanza kufuata uelekeo fulani. Kamanda na yule polisi walifuatana kumfuata mbwa huyo. Mbwa aliwaongoza mpaka kwenye ukuta, umbel iwa mita kama 200 hivi kutoka eneo la tukio, kisha yule mbwa akasimama mahala na kuendelea kunusa hapa na pale bila kwenda popote.

Amata akiwa na yule mbwa mwenye mafunzo maalumu, walizunguka nje ya ukuta. Huko yule mbwa akaipata tena harufu ya Tracy na kuvuka barabara mpaka kwenye chuo cha utumishi wa umma. Mbwa akawaongoza mpaka msalani, walipoingia wote wakapiga na butwaa. Yule mwalimu alikuwa hana uhai, mwiliwe ukiwa umebaki na nguo za ndani tu. Pembeni yake kukiwa na nguo za Tracy. Amata akauma meno, akachomoa bastola yake, ile aliyopewa na Chiba usiku uliotangulia.

"*Shiit!* Katuweza, mtuhumiwa ameruka kihunzi!" aliongea kwenye kinasa sauti chake.

"Lazima akamatwe!" Gina akajibu.

“*Point one*! Upande wa Mashariki tafadhali, kuna mtu anayejaribu kujipenyeza katika kundi la wachuuzi wa samaki akielekea upande tofauti na wengine wote,” Chiba alitoa hadhari hiyo, akiwa anakamata picha kutoka katika kamera za siri zilizozunguka eneo hilo.

“*Point One kazini*,” Kamanda akajibu.

“*Point two*, ongeza nguvu tafadhali,” Chiba akaomba.

“*Point two* kazini,” Gina akajibu.

“*Ground zero…. Ground zero…*” sauti ya Madam ilifika kwa wote, aliyekusudiwa akajibu.

“Nakusoma,” akajibu Chiba.

“Nipe dira yako!” akamwambia.

“Mashariki, soko la samaki, nyuzi sufuri usawa wa bahari,”

“*Copy!*” Madam S akajibu.

* * *

Tracy, alijitahidi kupenya kwenye kundi la watu kwa minajiri ya kufika baharini, aliamini akifika tu baharini, kamanda na kikosi chake hawatamwona tena kwani mbinu

za kutoroka kwa njia hiyo alikuwa akizijua vyema. Alipogeuka nyuma alimwona Amata akimfuata kwa umakini wa hali ya juu huku mkononi mwake amekamata bastola ndogo.

"Simama!" Amata akatoa amri lakini mwanamke yule hakusimama. Amata akapiga risasi hewani na watu wote wakatawanyika, wengine wakianguka chini na kukanyagana vibaya. Tracy akapata kipingamizi kipya, lakini bado hakuonesha udhaifu. Alichomoa bastola yake iliyopachikwa mguuni, akageuka nyuma na kumfyatulia Amata, ambaye tayari aliliona hilo. Kamanda Amata akajitupa na kubingirika chini ile risasi ikamkosa na kujeruhi mwingine nyuma yake. Miwani yake ikavunjika vibaya, akaiokota na kuitia katika mfuko wa koti. Akanyanyuka haraka na kumtazama Tracy, hakumuona. Akiwa bado na bastola yake mkononi, akatazama huku na huku.

"*Point one*, Chumba cha kuhifadhia Samaki," Chiba akatoa maelekezo kwani alikuwa akiendelea kumfuatilia Tracy kwa mtandao.

"*Point one* kazini," Kamanda akajibu huku akiingia katika chumba kikubwa kilichopangwa majokofu mengi makubwa makubwa. Ndani ya chumba hichi utulivu ulitawala. Harufu ya samaki ilikijaza chumba chote, kelele za pangaboi na

muungurumo wa mafriji ndizo zilisikika. Bastola mkononi, Amata alikuwa makini kupekuwa uchochoro mmoja baada ya mwingine.

Ghafla, Amata alijikuta akipewa dhoruba kali ya pigo la karate lililodhamiria kuua. Pigo lile lilitokea nyuma yake, akayumba lakini hakukubali kuanguka. Akajiweka sawa, kisha akageuka nyuma na kukutana na mapigo makali kama matano hivi ya haraka haraka yaliyomchanganya na kumpeleka chini. Tracy akasimama sakafuni kwa mtindo wa kuvutia, akiwa tayari kwa mapigano na kijana huyo mtanashati.

Wakati wanawake wenzake walikuwa wakitafuta nafasi ya kuwa mapenzini naye ili tu wajisifie yeye alikuwa anatafuta nafasi ya kupigana naye. Amata alijizoazoa pale chini, alihisi mkono wake kutonesheka tena. Tracy alijirusha kwa namna ya ajabu kwa minajiri ya kutua na shingo ya hasimu wake lakini hapo ndipo alipopajutia. Kamanda Amata alijitupa pembeni na Tracy akatua peke yake, alipomtazama Amata tayari alikuwa mbele yake. Pigo moja la maana likapiga katikati ya sura yake nzuri, Tracy alishuhudia nyota nyingi mbele yake, kabla hajatulia pigo zito la pili likatua mbavuni, Tracy akajikuta analegea, hana la kujitetea. TSA 1 aliamua kutumia mapigo ya kifo kumlegeza

mwanamke huyo. Pigo la tatu lililokuwa linalenga kutoboa tumbo la Tracy na kufumua takataka zote za tumboni, lilikingwa kiustadi sana. Tracy akainyonga mikoni ya Amata hasa ule ambao umefungwa bendeji ambao Kamanda aliutumia bila kujali. Akaunyonga kwa nguvu, maumivu makali yakapenya kwenye mishipa ya Amata. Akabana meno kwa maumivu hayo kisha akajifyatua na kumtandika kichwa kimoja maridadi. Yule mwanake alihisi kama jiwe limepiga kwenye mwamba wa pua. Akamwacha Kamanda na kurudi nyuma, akasimama akihisi kama kitu kinatoka ndani ya pua yake, damu.

Tracy akawa kama mbogo aliyejeruhiwa, sasa alimdhamilia Amata. Alikula yamini moyoni mwake, ama zangu ama zake. Aliruka na kutua juu ya moja ya jokofu kubwa akinuwia kushusha kipigo kwa Kamanda kutokea juu. Loh, alicheza pata potea, kwani hilo Kamanda alilitegemea baada ya kusoma macho ya Tracy kabla. Amata aliruka hewani na kumchota ngwala kutoka pale juu huku akienda kutua upande mwingine. Wakati miguu ya Tracy ikitua ilikutana na mguu wa Amata. Tracy alijikuta akirudishwa hewani sasa kwa mtindo wa kuangushwa vibaya lakini kwa ustadi wake na ufundi wa mapigano alijigeuza juu kwa juu na kupoteza lengo la Amata. Akatua chini na kukutana na guu lenye nguvu lililotua kifuani mwake. Tracy

akatupwa nyuma na kupiga mgongo kwenye jokofu. Alipokaza macho yake ambayo yalikuwa yakipoteza nuru, alimwona Amata bado akiwa kaweka mguu juu, hajaushusha chini. Tracy alihema kwa nguvu, damu zikiendelea kumvuja puani. Aliruka sarakasi moja matata na kupeleka pigo la *kung-fu* kwa Amata lakini likakingwa kiufundi. Kamanda Amata alionesha ukamanda wake kwa kumchanganyia mapigo yule mwanamke na kumchakaza vibaya. Tracy alipokea pigo moja zito lililopigwa kwa mikono yote miwili na kutua kifuani mwake, kisha *double kick* zilizompelka chini kama mzigo. Amata alitua sakafuni kwa madaha kabisa.

Watu tayari walikwishajaa eneo lile wakiangalia mpambano huo.

"Umekamatika, Tracy Tasha, muuaji mwenye taaluma, nawe utauawa kitaalamu vile vile…," Amata alimwambia huku akishusha mguu wake chini.

Tracy hakuongea kitu, alibaki kimya akihema huku akitema mabonge ya damu. *"Ne-ver"* alijibu kwa shida sana, sauti yake ilikuwa ikimezwa na maumivu makali.

"Sasa utanyongwa Tanzania, mzungu muuaji wewe, uliona haitoshi kumuua Khumalo, Touzony na sasa ukaamua kuja Afrika Mashariki? Basi aliyekutuma

amekuuza, alijuwa wazi kuwa hapa ndiyo kaburi lako kama mwenzako McField ambaye tangu jana tayari yuko motoni bila shaka na wewe anakusubiri kule ili mkamuue shetani kama mnaweza kuua," Kamanda alimwambia Tracy.

Tracy Tasha alikunja sura baada ya kusikia kuwa Mc Field alikuwa tayari marehemu. Maneno yale yaliuchoma moyo wake. Alimtazama mwanaume huyo aliyesimama mbele yake asiamini anachosema. Kwa jinsi anavyomjua McField atakufaje kirahisi namna hiyo anayosema huyu mtu.

"Tunakufahamu sana, na tulikuwa tunakusubiri. Serikali ya Tanzania haiwezi kuangushwa na nguvu yenu vibaraka na sasa utanambia ni nani aliyekupa kazi ili naye nikamshughulikie hata akiwa na ulinzi wa namna gani," Kamanda alimweleza.

"Maneno mengi hayavunji mfupa, na siwezi kufa kabla sijakuharibu," Tracy alijibu na kujifyatua kutoka pale alipo. Akashusha kipigo kizito kwa Amata. Kasi aliyokuwa anaitumia Tracy kupeleka mapigo kwa mikono na miguu ilimshangaza Amata. Tangu alipoanza kupambana na watu wenye ujuzi mbalimbali huyu alikuwa tofauti. Kamanda Amata valikuwa makini, alikinga mapigo yote kumi na nane na hakuna hata moja lililopata. Tracy hakutulia, pigo la mwisho alijinyoosha na kupiga msamba akiwa anakwepa

teka kali la Amata ambalo lingetua ubavuni mwake basi bila shaka lingevunja mbavu za kutosha. Teke lile lilimkosa Tracy. Akajirusha upande wa pili na Tracy aliyedhamiria kushusha pigo kwenye korodani alikosa shabaha na kujikuta kabaki peke yake.

Akanyanyuka haraka na kukutana na konde zito la Amata, lililotua shavuni, akapepesuka kidogo kabla hajatulia, akapokea la pili, la tatu, la nne, la tano, la sita, la saba, Tracy akajikuta sakafuni, sura yote imechakazwa.

Akajinyanyua tena haraka na kusaimama wima, akamfuata Kamanda kwa kasi. Amata akamkwepa na kumtwisha konde la kilo nyingi lililotua tumboni, Tracy akaganda akiwa kajishika tumbo, damu ikimtoka kinywani. Amata alikuwa katulia palepale, akisubiri mwanamke huyo ajibwage chini maana alijua kwa kilo za ngumi hiyo hawezi kupona tena na akipona hatokufa tena.

* * *

Watu walijazana katika mlango mkubwa wa jengo hilo wakiangalia mapigano yale yaliyokuwa yakiendelea, walishangaa mwanamke huyo alivyokuwa akifanya minyumbuliko ya ajabu katika kupigana.

“Huyu atakuwa Cynthia huyu!” mmoja akamwambia mwenzake na kufanya wengine kucheka. Mara ving’ora vya polisi vilisikika karibu na eneo hilo. Watu wakaanza kusogea nyuma, kuwapa nafasi ya kufanya kazi yao. “Eeeee wanoko haooo!” akasikika kijana mmoja mchuuzi wa samaki.

Ndani ya soko hilo kulikuwa na hali ya sintofahamu, kila mmoja alitaka aone kinachotukia, lakini, gari la kikosi cha kutuliza ghasia lilifika na kuwataka watu wote kusogea mbali na eneo. Hawakupinga, walitii sheria bila shuruti. Gina aliwasili, huku nyuma akifuatiwa na askari wengine. Alimkuta Amata bado kasimama palepale huku Tracy akiwa chini sakafuni.

“Apelekwe Shamba!” Amata akamwambia Gina. Kwa kusema vile tayari TSA wote walipata taarifa. Dakika chache tu, liliwasili gari maalum la kubeba watu kama hao. Scoba akateremka na kuelekea eneo la tukio. Akafika pale na kuuvuka utepe. Wanausalama kadhaa na askari waliimarisha ulinzi katika eneo lile.

Yule mwanamke alichukuliwa kutoka pale sakafuni mzobemzobe, huku miguu yake ikiwa imefungwa mnyororo na mikono yake ikiwa na pingu. Akafikishwa kwenye lile gari, Land Rover Defender, lililofungwa pande zote na

kuruhusu watu wawili tu walio mbele kuweza kuona nje. Umati ulikuwa ukishuhudia tukio hilo.

Kitendo cha dakika zisizozidi mbili, Tracy alipofikishwa kwenye gari hilo, mtu mmoja aliyevalia soksi jeusi kuficha sura yake akajitokeza akiwa na silaha nzito kifuani mwake. Akafungua mlango wa nyuma na wengine wakampakia mwanamke huyo akiwa hoi bin taabani. Milango yake ikafungwa. Lile gari likatiwa moto na kuondoka mahali pale huku likiacha watu bado wakiwa kwenye taharuki. Magari ya polisi yalijazana eneo hilo na kila aina ya askari alionekana akiwa katika sare yake. Soko la samaki liligeuka *Afghanistan* kwa muda mfupi.

Amata akachukuliwa mpaka kwenye gari la wagonjwa na kupakiwa humo. Mwanamke mmoja aliyevalia kidaktari aliingia pamoja naye na kuanza kumpatia huduma ya kwanza kwa majeraha machache aliyoyapata. Hakuwa na shaka na mtu huyo, alimjua. Madam S akawasili, akaongozwa kulifuata gari lile. akafungua mlango na kuingia ndani. Akamtazama kijana wake aliyekuwa akiendelea kupata huduma. "Vipi! Upo sawa?" akamuuliza.

"Nipo sawa mama. Yule mshenzi mmemwifadhi vizuri?"

“Ndiyo!” Madam akajibu na lile gari likawashwa na kuondoka eneo lile huku likipiga ving’ora vya kuomba njia.

Nusu saa iliyofuata, lile gari likawasili Magomeni bila kelele za ving’ora wala kuwasha taa zake za tahadhari. Likaiacha Barabara ya Morogoro na kukunja kushoto. Mwendo wa mita kama mia mbili hivi, likawasili kwenye nyumba moja ya kizamani, iliyochoka. Madam S, Amata, Gina aliyekuwa na dereva wa gari hilo na Jasmini wakateremka na kuliruhusu lile gari kuondoka. Kisha wao wakaingia ndani yaa nyumba ile. Nyumba ile ilitumiwa na watu wa TSA kama maficho yao ya muda pindi wanapotaka kupoteza watu malengo. Kwa nje ilikuwa ya udongo na iliyochoka lakini kwa ndani ilijengwa vizuri na kwa uimara wa kila hali. Fanicha chache za kizamani zailikuwa sebuleni hapo, kalenda ya mwaka 1985 ilining’inia ukutani huku juu ya meza ndogo kukiwa na gazeti la Mfanyakazi la mwaka huohuo. Amata akajitupa kitini na kushusha pumzi ndefu.

“Vipi?” Gina alkauliza.

“Haikuwa kazi ndogo…”

“Tumeshamweka kwenye mikono yetu na hawatomuona tena duniani…” Madam S akamwambia Amata.

“Kazi haijaisha, lazima tupate zile almasi, mali ya Watanzania haiwezi kupotea hivihivi!” Amata akaongea kwa uchungu. Madam S akamjibu kwa kutikisa kichwa juu-chini. “Tutakuwa hapa kwa muda kidogo, halafu tutaelekea shamba. Yule mwanaamke lazima ahojiwe, na atapike kila alicholishwa,” akawaambia.

“Haswaa!” Gina akakazia mazungumzo yale. Amata akainuka na kuelekea upande ambao kulikuwa na vyumba ya kulala. Nyumba hiyo haikuwa na vyumba vingi, ila viwili tu.

“Ok, nawaacha, nitawacheki baadae!” Madam akawaambia huku akiuelekea mlango.

Wakaagana.

# 1xii

MKUU WA NCHI aliteremshwa kwa lifti na kuingizwa ndani ya chumba chenye kila aina ya mitambo tiba kwa huduma ya kwanza. Akiwa na chupa ya maji iliyokuwa ikiendelea kuingia mwilini mwake, alikuwa kimya. Wanausalama na madaktari wa Ikulu, walihaha huku na kule kujaribu kuokoa maisha yake kwa maana walijua wazi kuwa taifa liko kwenye taharuki kwani hakuna cha kuficha. Hotuba ile ilikuwa ikienda moja kwa moja hewani na watu waliitazama kwa luninga. Walimlaza juu ya kitanda na wote wakasogea pembeni kutazama kinachoendelea maana mshangao na bumbuwazi ulikuwa dhahiri shahiri nyusoni mwao.

Ni siku chache zilikuwa zimepita tangu Rais ajiimarishie ulinzi wake binafsi kwa kuifumua idara ya usalama wa taifa kitengo cha ulinzi wa viongozi *'State Protection Squad'* na jambo hilo linatokea, kila mtu alichanganyikiwa. Ukimya ulichukua nafasi ya kila kitu katika chumba hicho, watu wachache wasiozidi watatu ukiachana na daktari walikuwa

wamebaki, wengine walitoka nje kuhakikisha mtuhumiwa anatiwa mkononi.

Polisi nao walizingira jengo lote la Ikulu na viunga vyake, barabara za kuingia na kutoka zilifungwa, halikuruhusiwa gari kuingia eneo hilo wala zilizo katika eneo hilo kutoka. Kila kona mbwa wa polisi wenye mafunzo ya hali ya juu ya kutambua wahalifu walifanya kazi ya kukagua kwa kunusa kila gari na kila mtu. Mbwa hao waliweza kutambua harufu ya kitu chochote hatari hususan milipuko.

Dakika tisini baadae, Madam S, aliingia katika chumba alichokuwa amelazwa Rais, akifuatana na Daktari Jasmini nyuma yake. Mlango mzito ukajirudishwa nyuma yao, mlango uliotengenezwa kwa madini ya kutokuingiza risasi. Walimkuta mheshimiwa amelala kimya kabisa kitandani, daktari akiwa kasimama pembeni.

“Vipi mbona hakuna kinachoendelea?” akauliza.

“Tumeshamwandaa tayari kwa safari,” yule daktari akajibu. Mkuu wanchi alikuwa na bandeji kubwa iliyotona tone la damu lenye ukubwa wa wastani kwenye eneo lake la kifua. Alitulia kimya pale kitandani.

Mwanamama huyo akamgeukia mtu wa kwanza ambaye ni afisa usalama mwenye mamlaka yote ya juu kwa

Rais. Yeye alikuwa amesimama pembeni mwa kitanda, “Kinachoendelea?”

“Usafiri unaandaliwa na muda si mrefu tutaondoka kuelekea London kwa matibabu, “ akajibu. Yule mwanausalama akamchukua Madam S kando na kumpa taarifa kuwa risasi ile haijaleta madhara kwani ilifika kwenye kizuia risasi, akaelewa. Hivyo utaratibu unaofanyka ni kumwondoa ili kuwaaminisha watu kuwa kiongozi wao yuko mahututi.

“Naweza kuongea naye?” akamuuliza.

“Bila shaka!”

Madam S akamkaribia Rais na kumwinamia, “tumemkamata aliyetaka kukuua!” akamnong’oneza. Rais akatabasamu.

“Unaweza kupona sasa mheshimiwa Rais,” madam akamwambia tena. Rais akainuka na kuketi.

“Asante sana Selina, ulililoliota ndilo haswa lililotokea…” akajiweka sawa. “Risasi hazikunifikia japo lilikuwa tukio la kuogofya sana. Sasa naomba muwaambie waandishi wa habari, wasitoe habari yoyote zaidi ya kuwa Rais amedunguliwa, basi, na hali yake ni mbaya. Waandike

hivyo hivyo," maneno hayo alimwambia mlinzi wake namba moja naye akampa taarifa msemaji wa serikali.

Huko nje waandishi walikuwa wakisubiri tamko la serikali, walipomwona msemaji huyo, wakajiweka sawa.

"Ndugu wanahabari, kwa kifupi, kama mlivyoona, Rais ameshambuliwa, ameumia vibaya na hali yake ni mbaya, hivyo Ikulu itamsafirisha mchana huu kwenda London kwa matibabu, taarifa yoyote mpya mtapewa kutoka hapa tu, asanteni." akamaliza mazungumzo yake na kunyanyuka. Waandishi wa habari waliokuwepo walianza kumgombania kumtupia maswali lakini aliondolewa mara moja na watu wa usalama. Mlango ukafungwa. Na dakika zisizopungua tano gari la wagonjwa la jeshi likawasili, kama ilivyopangwa, Rais akafungwa vizuri katika kitanda na kuondolewa.

Ni watu wasiozidi watano tu waliojua kuwa Rais ni mzima kabisa lakini wengine wote waliaminishwa hivyo kuwa mheshimiwa ana hali mbaya. Msafara wa magari ya Ikulu ukaondoka kuelekea uwanja wa ndege.

* * * *

Lile Defender likawasili ndani kabisa ya *Safe House* inayotumiwa na TSA inayojulikana kama Shamba. Upande wa dereva, Scoba akateremka akiwa na soksi lake usoni. Na

upande wa pili, Chiba naye akateremka. Walikuwa wawili tu ndani ya gari hilo. Wakafungua mlango wa nyuma na kumkuta Tracy akiwa hoi kajilaza. Wakamteremsha na kumshika huku na huku. Moja kwa moja wakamwingiza ndani ya jumba lile mpaka chumba wanachotumia kuhifadhi watu kama hao, wakamsukumia huko na kuufunga mlango ule mzito uliotengenezwa kwa shiti nene ya chuma. Akatua sakafuni kama mzigo, hajiwezi. Ujanja wote mfukoni. Hakutaka kuamini kabisa kama amewezwa na kijana huyo ambaye yeye alimwona si lolote si chochote. Mikono na miguu yake iliyofungwa barabara, ilimnyima uhuru wa kufanya lolote.

Ndani ya chumba kile alikuwa yeye tu, sakafu tupu, baridi, hakukuwa na dirisha hata moja, na kujazwa na hewa nzito. Pembeni mwa chumba hicho kulijengwa karo la kuogea ambalo tu ungeweza kuingia mzima mzima. Upande mwingine kulikuwa na kitu kama kabati kubwa lililotengenezwa kwa chuma kigumu. Lilishahabiana kabisa na yale masefu ya kuhifadhia noti katika benki. Hakuelewa na wala hakuamini kinachoendelea, maana katika kazi yake hiyo maisha yake yote aliwahi kutekwa na akafanikiwa kutoroka lakini mara hii alihisi kabisa kila kitu hakiwezekani. Alijua kuwa yupo katika chumba hatari kwani mtindo wa

chumba kama hichi anaujua. Akatulia kimya katika sakafu ile baridi.

*    *    *    *

Usiku wa saa saba, Madam S, Amata, Gina na Jasmin waliwasili katika jumba hilo maeneo ya Gezaulole, upande wa pili wa Jiji la Dar es salaam. Kwa jinsi jumba hilo la kizamani lililovyojengwa, gari huingia ndani kabisa hivyo ni vigumu kujua nani kaingia au nani katoka. Madam S na vijana wake wakateremka na kuingia ndani ya jumba hilo na kuungana na Scoba na Chiba ambao wao walimleta Tracy.

“Mtu wetu yupo?” Madam S akauliza.

“Yupo!” Chiba akajibu huku akisalimiana na bosi wake huyo, mwanamama hatari katika medani za kiusalama. Amata na Gina wakaongoza moja kwa moja kwenye kile chumba ambacho Tracy alikuwamo. Mara baada ya kubofya tarakimu maalumu za kufungua mlango huo, waliingia na kumkuta mtu wao akiwa kajikunyata kwenye moja ya kona za chumba hicho. Gina akafungua ule mlango wa kabati kwa kutumia ufunguo wake. Kutoka katika kabati lile, akavuta kitu kama meza na kufyatua kiti kilichounganishwa pamoja navyo. Tracy alibaki katoa macho, hakutegemea kama sehemu hiyo ingeweza kubeba vitu vyote hivyo. Amata akaliendea lile karo na kufungua maji, akahakikisha limejaa

vyema. Aliporudi pale kabatini, akachukua *gloves* na kuzivaa huku akimwangalia mwanamke yule.

"Tracy Tasha," akamtaja kwa jina, "… muuaji wa kukodi… unayejua kuua kwa kila mbinu, sasa upo mikononi mwangu…" Amata akasema huku akimfuata. Yule mwanamke akainua uso wake na kumtazama kijana huyo huku akihesabu hatua zake kila zinavyozidi kumkaribia. Amata akachuchumaa na kuutazama uso wa Tracy jinsi ulivyovimba kwa kipigo na ngozi yake ilivyovilia damu. "Nataka unieleze mambo matatu tu; la kwanza, kwanini ulitaka kumuua Rais wa nchi, pili… Almasi zilizoibwa Mwadui ziko wapi na tatu nani aliye juu yako na yuko wapi…"

"Hutosikia lolote kutoka kwangu nyani we'!" Tracy alijibu kwa sauti kavu na kumtemea Amata mate usoni. Kitendo kile kilimfanya kijana huyo kufura kwa hasira. Alijivuta na kumtandika kichwa kimoja kizito, Tracy akajibamiza ukutani na aliporudi akajikuta kakamatwa barabara na mikono ya kijana huyo. Amata akamburuza mwanamke huyo na kumtumbukiza kichwa chake kwenye lile karo la maji. Tracy alihangaika huku na huko kwa kuwa aliishiwa na pumzi zaidi alikuwa akinywa maji tu. Akamwibua kama sekunde tano na kumzamisha tena.

“Aaaaaagghhh, koh! Koh! Koh!” Tracy alikohoa vibaya alipoibuliwa mara ya pili.

“Nani kakutuma?... nani bosi wako!” Amata akamuuliza.

Tracy akatikisa kichwa kushoto kulia, ikiwa ishara ya kukataa kusema. Amata akarudia zoezi lile lile. Alipoona anaaza kutapatapa akamwibua.

“Nase-ma koh! Koh! Khhhoooo!” Tracy akakohoa na kutapika.

“SEMAAA! Nani bosi wako…?”

Tracy badala ya kujibu akabaki kuhema kwa nguvu huku akikoroma, mapafu yalijaa maji. Gina alikuwa kando kimya. Aina ile ya mateso hakuipenda hata kidogo ukizingatia ilikwishakatazwa kwenye jumuia za imataifa. Amata akampa ishara Gina, naye akaleta shubaka dogo. Amata akakifungua. Ndani yake kulikuwa an zana mbalimbali zenye kazi tofautitofauti.

*“No! No! let me say please..”* Tracy akakubali kusema.

“Haya sema haraka! Nani bosi wako?” Amata akamuuliza huku sura yake ikikosa chembe ya huruma.

Tracy aliendelea kukoroma na kutapika. “SEMAAA…” Amata alipaza sauti.

“Kho! Kho! Khooorrr, Ro-bi-nso-n!” Tracy akajibu huku akiendelea kutapika maji na kupumua kwa shida. Tracy alikohoa sana mpaka akaanza kutapika damu. Haikumchukua dakika hata tano, akapoteza fahamu.

Kitendo bila kuchelewa, Daktari Jasmini akawahi kuingia kwenye kile chumba na kumpa huduma ya kumfanya abaki na uhai wake. Akamhamisha na kumpeleka chumba kingine kilichojawa vifaa vya kutosha kwa huduma Zaidi.

*    *    *    *

Madam S alibaki kimya akifuatilia kila kitu kupitia runinga kubwa iliyowekwa kwenye chumba maalum cha utambuzi ndani ya jengo hilo. Mara Amata alipoingia ndani ya kile chumba akamtazama kwa jicho kavu.

“Amekufa?” akamuuliza.

“Binadamu hafi kirahisi mama!”

“Zaidi ya jina kuna jingine?” akamuuliza Amata.

“Hapana! Kamtaja bosi wake Robinson tu..”

“Lazima atafutwe, popote alipo duniani!” Madam S akamwambia Amata. Chiba alikuwa ametingwa na kufatilia kitu Fulani kutoka kwenye kompyuta yake. “Amata!” akaita. “Tracy, hakuwa peke yake, kuna watu hapa naona wanatoroka…” akamwambia huku akimpa ishara ya kumwita. Amata na Madam S akawasogelea pale na kuangalia kupitia ile kompyuta.

“Umejuaje?”

“Kila kitu nimechukua kwenye simu ya Tracy ambayo ninyi wote wala hamkuiona ilipoanguka!” akawajibu. “Tracy ilikuwa achukuliwe mara tu baada ya kukamilisha kazi baada ya hawa watu kugundua kuwa McField aliyepewa jukumu hilo hapatikani kwa simu. Hilo kwao lilikuwa jibu kuwa ameuawa. Na ni kweli, hawakukukosea. Kikosi namba mbili kilichokuwa tayari jijini Dar es salaam kwa siri kikaingia kazini. Kilifuatilia kila analolifanya Tracy kwa siri vilevile.

Katikati ya madau ya wavuvi pale Mgogoni, hawa jamaa nao waliegesha la kwao pasi na kujulikana. Mbinu ilikuwa ni kumchukua Tracy na kupotea naye. Walipojua kuwa amekamilisha kazi, ndipo wakampa ishara hiyo ya wapi akimbilie, lakini bahati haiukuwa yake. Walishuhudia, akiingia kwenye mikono ya TSA akiwa umbali wa mita tano tu na pale walipo, ndani ya soko kubwa la samaki. Tray

hakuwajua, na hakutakiwa kuwajua. Na wao hawakuweza kufanya lolote kwani walijua wangefanya jambo tu basi pangegeuka uwanja wa vita. Ikawabidi kuondoka haraka iwezekanavyo. Na walitakiwa kutoka kaabisa nje ya nchi kuelekea Afrika Kusini.

"Shiiiit!" Madam S akang'aka, "Amata, Chiba, Scoba, wawahi kabla hawajavuka mpaka! Hawapo mbali hawa…" akawaambia.

"Yeah wanaitafuta Morogoro saa hii…" Chiba akaeleza.

"Sasa hawa, tusiwasumbue, na wala pa kuwakamatia pasiwe kwenye makazi ya watu… tuwabane kwenye pori moja hivi usiku huu huu," Amata akatoa wazo.

"Ndiyo, hata polisi wasijue! Unaonaje Iyovi?" Chiba akamuuliza Amata.

"Iyovi pamekaa vibaya, labda tuwasubiri paleeee karibu na Igagala, kwenye ile kona mbaya ya Ruaha, pana eneo ambalo tunaweza kushusha chopa kirahisi!" Amata akajibu, wote wakaafikiana. Safari ikaandaliwa harakaharaka kwa Baraka zote za Madam S.

Wakiwa katika kuagana, Daktari Jasmini aliingia katika sebule ile, "Vipi?" Madama S akamuuliza.

“Tracy, Tracy amekufa!” akamjibu. Madam S akamtazama Amata kwa sekunde kadhaa kisha akawaruhusu kuendelea na mpango wao.